# Nipashe

Alhamisi Aprili 11, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579889

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Serikali yatangaza neema ya ajira 45,000 mwaka 2019/20

UKURASA 4



ama

AFYA NA MAZINGIRA

WHO: Wanawake wanaishi zaidi kuliko wanaume

Ajali ilivyompokonya mguu

Kila glasi ya kilevi inakaribisha kupooza

KLINIKI YA BABA, MAMA NA MTOTO

DARASA LA PROF. KAISI:

Kazi, dawa, mavazi ya wanaume kizuizi cha mimba kilichojificha

UKURASA 13



RIPOTI YA CAG

# Madudu kila kona

UKURASA 2 & 3

- UFISADI MAMILIONI WAIBULIWA POLISI
- HASARA MAMILIONI NEC UNUNUZI BVR
- ALIA MAPENDEKEZO KUTOFANYIWA KAZI
- ASISITIZA KUTUMIA NENO 'UDHAIFU'

## Mstaafu atafuna mamilioni mshahara

UKURASA 4

## Sala ya Mchungaji yamwokoa OCD kutumbuliwa na JPM

UKURASA 4

**MICHEZO** TFF YAIJIBU YANGA VIPORO VYA SIMBA UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Anusa hasara mamilioni ununuzi mashine NEC

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amesema amebaini hasara ya mamilioni ya shilingi katika ununuzi wa mashine za Mfumo wa Kidigitali wa Usajili wa Wapigakura (BVR) uliofanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Akitoa muhtasari wa ripoti yake ya ukaguzi ya mwaka 2017/18, CAG Assad alisema alibaini NEC ilinunua mashine za BVR 8,000 kwa ajili ya usajili wa wapigakura.

Hata hivyo, mashine 5,000 hazikukidhi vigezo vilivyoainishwa kwenye mkataba, hivyo kusababisha kutolandana kimatumizi na vile vilivyonunuliwa hapo awali na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) na Wakala wa Taifa wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Rita).

"Kutolandana huko kumeisababishia serikali hasara ya Sh. milioni 862.08 zilizotumiwa na Nida kununulia leseni mpya za 'Windows' na 'Biometric Algorithms' ili kubadilisha mashine 5,000 zilizopokewa kutoka NEC ziweze kufanya kazi na mfumo wa BVR wa Nida," alisema.

CAG Assad alisema alibaini mzabuni alilipwa Dola milioni 72.3 badala ya dola milioni 72.1, kiasi ambacho kilikuwa bei ya mkataba, hivyo kuwa na ongezeko la Dola za Marekani 148,243.73.

Alisema mafunzo ya Tehama kwa maofisa 15 wa NEC hayakufanyika licha ya mzabuni kulipwa Dola 358,650 kwa ajili ya mafunzo hayo.

Prof. Assad pia alisema katika ukaguzi wa Nida, alibaini kuwa kati ya watu 19,662,105 waliosajiliwa, ni vitambulisho 4,511,809 tu vilivyotengenezwa, sawa na asilimia 23 ya idadi ya watu walioandikishwa.

"Nilibaini kuwa Kampuni ya IRIS Corporation Berhad ya Malaysia (mkandarasi) imesimamisha shughuli zote za kutengeneza vitambulisho kuanzia tarehe 14 Machi 2018. Sababu za kusimamisha zinajumuisha kutolipwa deni la mkandarasi lenye thamani ya Dola za Marekani milioni 30.18 (Sh. bilioni 69.98), na kutoongezwa kwa muda wa mkataba kwa kipindi cha miezi 10 tangu kwisha kwa muda wa mkataba wa awali tarehe 14 Machi 2018," alisema. CAG Assad pia alisema mashauri ya kodi yanayoihusu Mamlaka ya Mapato (TRA) yameongezeka kutoka Sh. trilioni 382.6 kwenye mamlaka za rufaa za kodi mwaka 2017/18 kutoka Sh. trilioni 378.2 mwaka 2016/17.

Alisema ongezeko hilo la Sh. trilioni 4.4 limechangiwa kwa kiasi kikubwa na mashauri manne yenye thamani ya Sh. trilioni 374.7 yanayoihusu Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Acacia.

Prof. Assad pia alisema katika mwaka wa fedha 2017/2018, TRA ilikusanya Sh. trilioni 15.38 ikilinganishwa na malengo yaliyowekwa ya kukusanya Sh. trilioni 17.31, hivyo kuwa na nakisi ya makusanyo kwa Sh. trilioni 1.93 ambazo ni sawa na asilimia 11 ya malengo.

Alisema jumla ya makusanyo hayo haikujumlisha Sh. bilioni 18.95 ambazo ni vocha za misamaha ya kodi kutoka Hazina. Hivyo, makusanyo halisi ya mwaka 2017/18 ni Sh. trilioni 15.4 yakijumuisha na vocha za misamaha ya kodi kutoka Hazina.

Prof. Assad alisema ukaguzi wake pia ulibaini TRA ilishindwa kukusanya mapato zaidi ya Sh. bilioni 46.81 kutoka kwa walipakodi mbalimbali.

"Wakati wa uhakiki wa bidhaa zinazoingizwa nchini na nchi jirani ili zisafirishwe kwenda nchi nyingine, TRA ilishindwa kunipatia ushahidi kuthibitisha kuwa kodi ya Sh. bilioni 57.09 ililipwa.

"Nilibaini kuwa bidhaa zilizosafirishwa kutoka nchini kwenda nchi nyingine zilizopaswa kutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani ya Sh. milioni 649.45 ziliruhusiwa kwenda nje ya nchi bila kukamilisha taratibu za forodha.

"TRA ilishindwa kutoa ushahidi wa nyaraka za kuthibitisha kuwa kodi stahiki zilikusanywa," Prof. Assad alisema.

# Ripoti ya CAG ya ba

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

BAADA ya wingu lililogubika kwa takriban wiki moja, hatimaye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, ametoa muhtasari wa taarifa yake ya ukaguzi ulioanika 'madudu' karibu katika kila taasisi na idara alizozikagua.

Jana, ripoti hiyo iliwasilishwa bungeni na mawaziri wanaohusika na kumaliza utata ulioibuka wa ama ripoti hiyo ingewasilishwa bungeni au kutowasilishwa baada ya chombo hicho cha kutunga sheria kupitisha azimio la kutofanya kazi na Prof. Assad.

Muda mfupi baada ya ripoti hiyo kuwasilishwa bungeni, CAG alikutana na waandishi wa habari ofisini kwake, jijini Dodoma na kutumia muda wa saa moja na dakika tano kuwaeleza muhtasari wa kilichomo kwenye ripoti yake hiyo.

Katika mkutano huo, Prof. Assad alimshukuru Rais John Magufuli kwa kumpa ushirikiano, huku akiweka wazi kwamba alijua mapema hataalikwa na Bunge kushuhudia uwasilishwaji wa ripoti yake ya mwaka.

Alisema kwa kulitambua hilo, aliwaambia maofisa wake wajipange kuhakikisha muhtasari wa ripoti unaelezwa kwa waandishi wa habari kwenye Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) badala ya bungeni kama ilivyokuwa inafanyika miaka iliyopita.

Prof. Assad alisisitiza kuwa neno 'dhaifu' lililomfanya atiwe hatiani na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, halina tatizo katika matumizi ya taarifa za ukaguzi na wataendelea kulitumia.

"Ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha kwake ripoti za ukaguzi kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2018 na kuwezesha ripoti hizo kuwasilishwa bungeni kupitia mawaziri husika kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (ilivyorekebishwa mwaka 2005).

"Hii inadhihirisha Mheshimiwa Rais

# Ufisadi wa mabilioni polisi

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu (CAG), Prof. Mussa Assad, amebaini ufisadi wa mabilioni ya shilingi ndani ya Jeshi la Polisi.

Katika mkutano na waandishi wa habari kuhusu muhtasari wa ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka 2017/18, CAG Assad alisema ukaguzi maalumu uliofanywa ndani ya Jeshi la Polisi, umebaini lililipa Sh. bilioni 16.66 bila ya kuwapo ushahidi wa uagizaji na upokeaji wa sare za askari kwa Boharia Mkuu wa jeshi hilo.

Alisema ukaguzi huo pia ulibaini maoni ya kisheria ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yanayohusu uwasilishaji wa kiapo cha nguvu ya kisheria (Power of Attorney) na leseni halali ya biashara, hayakuzingatiwa wakati wa kutia saini mkataba Na. ME.014/PF/2015/2016/G/30 Lot 2, uliohusu ununuzi wa sare za askari polisi.

Vilevile, CAG alisema ukaguzi maalum wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) ulibaini mahitaji ya kitaalamu kutoka idara inayotumia mfumo huo hayakuzingatiwa wakati wa kutathmini na kutoa zabuni.

Alisema malipo ya Sh. bilioni 3.3 yalifanyika kwa mzabuni kwa ajili ya huduma ya matengenezo na msaada wa kitaalamu wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole kwenye mikoa nane ya kipolisi ya Temeke, Mwanza, Simiyu, Rukwa, Tabora, Kigoma, Geita, na Kinondoni, lakini Jeshi la Polisi lilishindwa kuthibitisha kuwa matengenezo hayo na msaada wa kitaalamu ulifanyika.

"Vifaa vya utambuzi wa alama za vidole vyenye thamani ya Sh. bilioni 1.73 havikufungwa kwenye magereza 35 yaliyoainishwa badala yake vilihifadhiwa katika Ofisi ya Upelelezi, Makao Makuu ya Jeshi la Polisi.

"Malipo ya Sh. milioni 604.3 kwa ajili ya mafunzo kwa wataalamu 30 hayakufanyika, Jeshi la Polisi lilishindwa kuionyesha timu yangu ya ukaguzi zilizoko monita 58 za kompyuta aina ya Dell zenye thamani ya Sh. milioni 159.1 zilizopelekwa kwenye Kitengo cha Uchunguzi wa Kisayansi cha Makao Makuu ya Jeshi la Polisi (Forensic Unit)," alisema.

CAG Assad pia alisema monita 213 za kompyuta aina ya Dell zililipiwa Sh. milioni 195.22 kwa mzabuni Lugumi Enterprises Limited, lakini mzabuni hakuzileta.

Alipendekeza kuchukuliwe hatua stahiki za kisheria na kinidhamu dhidi ya maofisa waliohusika katika ubadhirifu wa mali za umma.

Prof. Assad alisema kupitia Jeshi la Polisi, serikali ihakikishe kuwa vifaa vya utambuzi wa alama za vidole vinafungwa katika maeneo husika na kuanza kutumika kama ilivyokusudiwa.



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad.

# Mashirika 14

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amebainisha mashirika ya umma 14 yenye matatizo makubwa kifedha na yanatengeneza hasara na madeni makubwa.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, CAG Assad alisema kuwa katika ukaguzi wake alibaini kuwapo kwa mashirika hayo yenye matatizo makubwa ya kifedha pamoja na kupata hasara hadi kusababisha madeni kuwa zaidi ya mitaji yao kwa zaidi ya asilimia 100.

Alisema kati ya mashirika hayo, 11 yana ukwasi hasi kwa maana yanajiendesha kwa hasara kwa zaidi ya miaka miwili. Kufuatia hali hii, Prof. Assad alisema ni dhahiri kuwa mashirika hayo hayawezi kujiendesha bila kutegemea msaada kutoka serikali kuu.

Aliyataja mashirika hayo kuwa ni

# ini madudu kila kona

anavyothamini majukumu ambayo ofisi yangu imepewa kikatiba katika kusimamia rasilimali za Watanzania," alisema Prof. Assad.

Katika muhtasari wa ripoti yake, Prof. Assad alifichua 'madudu' katika taasisi na idara mbalimbali za serikali, ikiwa ni pamoja na kufanya malipo kwa kazi hewa na udhaifu katika malipo ya mafao.

CAG Assad pia alieleza kusikitishwa na kutofanyiwa kazi kwa mapendekezo ya ripoti zake zilizopita na matumizi mabaya ya fedha katika vyama vya siasa nchini.

Prof. Assad alieleza kuhusu usimamizi wa Deni la Taifa, akibainisha kuwa limeongezeka lakini bado ni himilifu. Pia alizungumzia udhaifu ulioko katika usimamizi wa mishahara na rasilimali watu na udhaifu katika ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Mtaalamu huyo wa ukaguzi wa hesabu pia alisema ripoti yake imebainisha kuwapo kwa mfumo usiofanya kazi ulionunuliwa katika Shirika la Bima la Taifa ulionunuliwa kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 3.5.

Prof. Assad pia alibainisha udhaifu katika ununuzi wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) na ununuzi wa sare za Jeshi la Polisi nchini uliogharimu Sh. bilioni 16.66 bila kuwapo kwa ushahidi wa uagizaji na upokeaji sare hizo.

Katika ripoti yake, CAG pia alibainisha malipo ya Sh. bilioni 1.43 yaliyofanyika mara mbili kwa udanganyifu kupitia maofisa wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) na Sh. bilioni 1.95 zilizolipwa bila kuwapo kwa jedwali la vipimo na hati ya madai zilizoidhinishwa na mhandisi mshauri.

Ripoti ya CAG pia imebainisha utoaji usioridhisha wa huduma za ugani kwa wakulima, udhaifu katika usimamizi wa ujenzi wa majengo mijini, udhaifu katika utoaji wa huduma za afya za rufani na dharura katika hospitali za rufani za kanda na ufanisi wa mfumo wa ununuzi wa magari serikali kwa pamoja.

Prof. Assad aliwaambia waandishi wa habari kuwa alitoa mwaliko kwa wenyeviti wa kamati za Bunge zinazoshughulikia ripoti zake (PAC na LAAC) kuhudhuria mkutano wake huo, lakini hajui sababu za kutokuwapo kwao.



## Alia mapendekezo kutofanyiwa kazi

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amesema amefanya tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa miaka iliyopita na kubaini serikali haijayafanyia kazi kwa kiwango kikubwa.

Katika mkutano na waandishi wa habari ofisini kwake jijini Dodoma jana, Prof. Assad alisema tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo hayo inaonyesha kuwa kati ya mapendekezo 350 yaliyotolewa miaka iliyopita, mapendekezo 80 (asilimia 22.9) yametekelezwa kikamilifu.

Alisema mapendekezo 124 (asilimia 35.4), utekelezaji wake unaendelea, mapendekezo 72 (asilimia) 20.6, utekelezaji wake haujaanza na mapendekezo 74 (asilimia 21.1) yamepitwa na wakati.

"Kwa ujumla, utekelezaji wa mapendekezo bado upo chini. Hivyo, ninapendekeza serikali iongeze jitihada katika kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti zangu," alisema.

CAG Assad pia alisema hati za ukaguzi zilizotolewa kwa Serikali Kuu na taasisi zake, mamlaka za serikali za mitaa na mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha 2017/18, ametoa jumla ya hati 548. Kati yake, zinazoridhisha ni 531 (asilimia 97, zenye shaka ni 15 (asilimia 2.6), moja isiyoridhisha (asilimia 0.2) na hati mbaya moja (asilimia 0.2).

Vilevile, Prof. Assad alisema ametoa jumla ya hati za ukaguzi 469 kwa miradi ya maendeleo iliyokuwa inatekelezwa na taasisi mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2017/18, kati yake, zinazoridhisha ni 455 (asilimia 97) na zenye shaka ni 14 (asilimia tatu).

# yatengeneza hasara

pamoja na Kampuni ya Ndege (ATCL), Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi, Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC), Bodi ya Utalii (TTB), Shirika la Majisafi na Usafi wa Mazingira, Dar es Salaam (Dawasco) na Kampuni ya Maendeleo ya Nishati ya Joto Tanzania (TGDC).

Mengine ni Baraza la Biashara la Taifa, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Mtwara, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Mwanza, Kampuni ya Usafirishaji na Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usambazaji wa Umeme, Kampuni ya Simu (TTCL-Pesa), Bodi ya Maziwa Tanzania na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Dar es Salaam (Dawasa).

CAG Assad pia alisema ukaguzi wake katika mishahara na rasilimali watu, ulibaini madai mbalimbali ambayo hayajalipwa ya kiasi cha Sh. bilioni 11.1, ambacho ni malimbikizo ya mishahara ya watumishi katika mamlaka za serikali za mitaa 22.

Prof. Assad pia alisema malipo ya mishahara kwa watumishi waliokoma utumishi wao ya jumla ya Sh. milioni 207.37 katika mamlaka za serikali za mitaa 17.

Alisema malipo hayo yanajumuisha Sh. milioni 128.31 kwa watumishi waliofariki, wastaafu na watoro waliofukuzwa kazi, Sh. milioni 53.94 ikiwa ni makato ya watumishi hao, na Sh. milioni 25.10 ikiwa ni mishahara iliyolipwa mara mbili katika Halmashauri ya Babati.

## Deni la Taifa lazidi kupaa

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebainisha kuwa Deni la Taifa limeongezeka kwa Sh. trilioni 4.84 (asilimia 10.5) katika kipindi cha mwaka mmoja kutoka Juni 30, 2017 hadi Juni 30, mwaka jana.

Prof. Assad aliwaambia waandishi wa habari jijini Dodoma jana kuwa Juni 30, 2017, deni hilo lilikuwa Sh. trilioni 46.08 wakati Juni, 30, mwaka jana lilikuwa Sh. trilioni 50.92, deni la ndani likiwa Sh. trilioni 14.73 na deni la nje Sh. trilioni 36.19.

Alisema alibaini upungufu katika usahihi wa taarifa kutokana na udhibiti wa ndani usiojitosheleza katika kuweka kumbukumbu na kutoa taarifa za deni la serikali.

Assad pia alisema amebaini serikali kuchelewa kulipa madeni ya Benki Kuu ya kiasi cha Sh. bilioni 212.7. Kati yake, Sh. bilioni 199.79 zinatokana na riba ya nakisi ya serikali, na Sh. bilioni 12.9 ikiwa ni sehemu ya serikali ya gharama za kudhibiti ukwasi kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2017/18.

"Pia nilibaini kutokuwapo kwa uwianishaji wa taarifa za mfumo wa malipo (Epicor) na mfumo wa utunzaji wa taarifa za Deni la Taifa wa Jumuiya ya Madola (Common Wealth Secretariat-Debt Record Management System – (CS-DRMS)).

"Hii inasababisha taarifa za fedha kutowiana na vyanzo vyake, hivyo kuhatarisha uadilifu wa taarifa za deni la serikali," CAG Assad alisema.

### MAJALADA YA MAFAO

Prof. Assad alisema katika mwaka wa fedha 2017/2018, alikagua majalada 2,868. Kati yake, 2,814 yenye jumla ya Sh. bilioni 165.44, aliyaidhinisha kwa ajili ya malipo, lakini majalada 54 alihoji na kuyarudisha kwa maofisa masuhuli husika kwa ajili ya masahihisho.

"Kati ya majalada 2,868 yaliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2017/18, mafao ya wastaafu 295 (10.5%) yalibainika kukokotolewa kimakosa. Kati ya hayo, majalada 172 yamebainika kuwa na ziada ya malipo ya Sh. milioni 577.32, huku majalada 123 yakiwa na upungufu wa malipo wa Sh. milioni 294.35.

"Nilibaini ucheleweshaji mkubwa wa waajiri katika maandalizi na uwasilishaji wa majalada ya wanufaika wa mafao kwa ajili ya ukaguzi. Ucheleweshaji huo unatokana na waajiri kutotoa kipaumbele kwenye usimamizi wa uandaaji wa mafao, hivyo kuwanyima wastaafu haki yao ya kupata mafao kwa wakati," alisema.

# Mstaafu matatani, mali zake kutaifishwa kufidia mil. 30/-

**Na Dege Masoli,** TANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Tanga, imetangaza kusudio la kufilisi mali za Aneth Makame kufidia jumla ya shilingi milioni 30 alizokuwa akizipokea kama mshahara, licha ya kustaafu utumishi wa umma.

Aidha, taasisi hiyo imeokoa wastani wa shilingi 2,190,500 zilizokuwa zimechukuliwa kinyume cha sheria na taratibu za fedha.

Akitoa taarifa ya kuanzia Januari hadi Machi 2019, Kamanda wa Takukuru Mkoa wa Tanga, Christopher Mariba, alieleza kuwa Makame alistaafu utumishi idara ya elimu miaka mitano iliyopita, lakini aliendelea kupokea mshahara kwa kipindi chote hicho na kuisababishia serikali hasara hiyo.

Alisema suala hilo liliamuliwa katika Mahakama ya Wilaya ya Muheza kwa kutakiwa kuzirejesha fedha hizo na kwamba taasisi hiyo inaangalia namna ya serikali kuzipata ikiwamo hata kwa kuuza mali za mhusika.

"Fedha hizo bado hajaanza kuzirejesha na endapo atashindwa kufanya hivyo, itabidi tutafute utaratibu mwingine wa kupata fedha hizo ...na hii itakuwa ni pamoja na kuuza nyumba au mali yake yeyote anayoimiliki," alisema Mariba.

Kuhusu fedha zilizookolewa, Mariba alisema zilichukuliwa kinyume cha sheria na taratibu na kwamba ili kuhakikisha kiasi hicho kinarejeshwa taasisi hiyo imeshawaandikia barua waajiri wa wahusika ili wachukue hatua za kinidhamu na kiutawala dhidi ya wahusika hao.

Hata hivyo, alisemaTakukuru kwa Mkoa wa Tanga imepokea jumla ya taarifa 63 za vitendo vya rushwa na uchunguzi wake unaendelea, ambapo serikali za mitaa zipo 24, Ardhi 11 na Mahakama 6. Zingine Polisi 5, Elimu 4, Biashara 3, Afya na Ushirika 2. Kilimo, Ujenzi, Siasa, Maji, Temesa na TRA zenye taarifa moja moja.

Mariba alisema kwa kipindi hicho yameendeshwa mashauri 25 mahakamani, ambapo 21 yalifunguliwa kabla ya Januari 2019 na manne ni Januari na Machi na moja kati ya hayo limefika kwenye maamuzi.



Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi Korogwe katika Halmashauri ya Mji wa Kahama, Christina Misese, akipanda mti pamoja na wanafunzi wake, wakati wa uzinduzi wa zoezi la upandaji miti 1,000 lililoandaliwa na Shirika la Compassion mjini humo jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Sala ya Mchungaji yamwokoa OCD kutumbuliwa na Magufuli

**Na Romana Mallya**

SALA iliyoendeshwa na mchungaji kuwaombea msamaha waliojihusisha na mauaji ya watoto saba mkoani Njombe, imemuokoa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Njombe, Sifael Pyuza, asitumbuliwe na Rais John Magufuli.

Kabla ya sala hiyo, Rais Magufuli alieleza sababu za kumwondoa aliyekuwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Njombe, Renatha Mzinga, kwamba alishindwa kusimamia usalama kwa wananchi wake na hapo hapo aliagiza OCD huyo naye aondoke.

"Hivi OCD wa hapa bado yupo? Kama bado yupo nayeye aondoke, nayeye kuanzia leo siyo OCD wa hapa, ni lazima watu ifike mahali katika maeneo yetu tuwe tunawajibika. Watoto saba wanakufa upo na nyota zako lazima uwajibike kwa matendo hayo," alisema.

Rais Magufuli alitangaza kumwondoa OCD huyo na baada ya dakika chache mbele, sala iliyoongozwa na mchungaji aliyekuwa kwenye mkutano huo, ilisababisha abadili uamuzi wa awali aliyokuwa ameutangaza.

Rais Magufuli alichukua uamuzi huo alipokuwa kwenye ziara ya kikazi mkoani humo kwa ajili ya uwekaji wa jiwe la msingi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Njombe na uwekaji wa jiwe la msingi wa mradi wa barabara ya Njombe-Moronga-Makete yenye urefu kilometa 107.4.

Baada ya kuelezea namna watoto hao walivyopotea, Rais Magufuli alimwita mchungaji ili aombe msamaha kwa waliohusika na vitendo hivyo na mchungaji huyo alipomaliza kusali alitamka kwamba amemsamehe OCD, hivyo aendelee kazi zake kwenye kituo chake cha kazi.

Katika mkutano huo ambao ulifanyika kwenye viwanja vya sabasaba Njombe mjini, Rais Magufuli alisema suala la mauaji ya watoto mkoani humo halikutakiwa kuchukua muda mrefu wakati kuna viongozi.

"Ndio maana RPC wa hapa niliamua kumtoa, wala msitafute sababu nyingine, nilimtoa kwa sababu

INAENDELEA UK. 8

# Neema ya ajira 44,000 serikalini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2019/20, serikali itaajiri watumishi wapya 44,807 wa kada mbalimbali.

Miongoni mwa kada zitakazoajiri watumishi wengi ni Elimu (13,526), Afya (9,467), Jeshi la Polisi (3,725).

Kada zingine ni Kilimo, Mifugo na Uvuvi (2,141), Magereza (685), Jeshi la Zimamoto na Uhamiaji (500), Hospitali za mashirika ya dini na hiari (1,262) na pia watumishi 13,002 wa kada nyingine wakiwamo wahadhiri wa vyuo vikuu vya umma.

Kauli hiyo ilitolewa bungeni jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), George Mkuchika, alipokuwa akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2019/2020.

Alisema mbali na kuajiri, pia watumishi 290,625 watapandishwa vyeo kulingana na maelekezo yatakayotolewa.

MISHAHARA

Aidha, alisema bodi itafanya utafiti wa hali ya mishahara na masilahi katika vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo ni Polisi, Magereza, Uhamiaji, Zimamoto na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) ili kushauri namna bora ya kutoa motisha.

"Utoaji motisha utazingatia viwango stahiki vya kuongeza ufanisi katika kazi za vyombo hivyo," alisema.

Mkuchika alisema Bodi ya Mshahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma inatarajia kuandaa taarifa nne za gharama ya maisha ambazo zitatumika kushauri kiwango cha mshahara unaoendana na gharama za maisha kwa watumishi wa umma.

**UHAKIKI WATUMISHI WA UMMA**

Waziri Mkuchika alisema serikali itafanya uhakiki wa watumishi kwenye sekretarieti za mikoa ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora ya rasilimali watu katika utumishi wa umma.

Kadhalika, alisema wanachambua na kuhakiki madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma 21,683 yenye thamani ya Sh. bilioni 50.7 na kuchukua hatua ipasavyo.

Sambamba na hilo, alisema watafanya uhakiki wa matamko ya rasilimali na madeni ya viongozi wa umma 2,000 na kuendelea na mchakato wa kutumia mfumo wa ujazaji wa fomu za matamko ya rasilimali na madeni kwa viongozi wa umma kwa njia ya mtandao baada ya kukamilika kwa mfumo wa kielektroniki wa menejimenti ya taarifa za kimaadili.

Mkuchika alisema pia serikali itahusisha miundo na mgawanyo wa majukumu ya taasisi za umma 100 zikiwamo ofisi, wizara zinazotegemea, wakala za serikali na mashirika ya umma na kuziwasilisha kwa Rais kwa ajili ya kupata idhini ya utekelezaji na lengo likiwa ni kuongeza ufanisi.

Wizara hiyo iliomba Bunge liipitishie Sh. bilioni 683.5, ambapo matumizi ya kawaida ni Sh. bilioni 483.6 na matumizi ya maendeleo ni Sh. bilioni 199.8.

Akizungumzia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mkuchika alisema kwa mwaka wa fedha 2019/20 itafanya utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini katika maeneo ya vijiji 4,408, mitaa 1,189 na Shehia 96 ambazo hazikufikiwa katika awamu ya kwanza ya mpango, huku kaya 355,000 zinatarajia kufikiwa.

Aidha, Mkuchika alisema Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), inatarajia kuanzisha vituo vitano vya urasimishaji biashara ili kuwawezesha wafanyabiashara kupata huduma muhimu sehemu moja katika halmashauri tano za Kahama, Tabora, Nyamagana, Songea na Babati.

**MAONI YA KAMATI**

Akisoma taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Venance Mwamoto, alisema kamati hiyo inashauri serikali kuongeza mshahara kwa watumishi wa umma ili kuwawezesha kumudu gharama za maisha ambazo zimekuwa zikiongezeka kila uchao.

"Sisi sote ni mashahidi kwamba serikali haijaongeza mshahara kwa watumishi wa umma kwa mwaka wa tatu sasa," alisema.

HABARI KITAIFA

# M'biashara Dar kortini kesi isiyo na dhamana

Na Hellen Mwango

MFANYABIASHARA Florensia Mashauri maarufu kama Florensia Membe, amefikishwa mahakamani akikabiliwa tuhuma za uhujumu uchumi.

Miongoni mwa tuhuma hizo ni kuratibu shughuli za uhalifu, kujenga kituo cha mafuta bila kibali cha Ewura, kutakatisha fedha na kuisababishia Kampuni ya Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (UDART) hasara ya Sh. bilioni 2.4.

Mashauri alisomewa mashtaka yake katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustine Rwizile.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Mawakili wa Serikali Ester Martin na Fatuma Waziri.

Martin alidai shtaka la kwanza, kati ya Januari Mosi, 2011 na Agosti 31, 2018 akiwa na wenzake kwa makusudi aliratibu makosa ya uhalifu.

Shtaka la pili, ilidaiwa kati ya Januari 2015 na Desemba, 2017 mshtakiwa akiwa kama Mkurugenzi wa Kampuni ya Zenon alijenga kituo cha mafuta katika yadi ya UDART kilichopo Jangwani bila kibali cha Ewura.

Shtaka la tatu, ilidaiwa siku na tarehe ya tukio la pili, mshtakiwa akiwa kama Mkurugenzi wa Kampuni ya Zenon, alianzisha biashara ya mafuta eneo lisiloruhusiwa katika yadi ya Kampuni ya UDART iliyopo Jangwani jijini Dar es Salaam.

Shtaka la nne, ilidaiwa kati ya Mei 25, 2015 na Desemba 31, 2016, mshtakiwa akiwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Zenon aliiba mafuta ya Sh. bilioni 1.2 mali ya Kampuni ya UDART.

Waziri alidai katika shtaka la tano na la sita, Mei 25,2015 na Desemba 31, 2016 mshtakiwa alitakatisha na kumiliki Sh. 2,414,326,260.70.

Shtaka la saba, ilidaiwa kati ya Mei 25, 2015 na Desemba 31,2016, kwa makusudi mshtakiwa aliisababishia UDART hasara ya Sh. 2,414,326,260.60.

Hakimu alisema mshtakiwa hatakiwi kujibu chochote kwa sababu mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi bila kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) au upelelezi utakapokamilika itahamishiwa Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa.

Upande wa Jamhuri ulidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika, hivyo uliomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Rwizile alisema kesi hiyo itatajwa Aprili 23, mwaka huu na mshtakiwa apelekwe mahabusu.

# Samia ataka wananchi waache kulalamika

Na Richard Makore

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amesema serikali inatambua na kuthamini utafiti mbalimbali unaofanywa nchini na itazitumia kwa ajili kuboresha maisha ya Watanzania.

Kadhalika, Samia amewataka Watanzania kuwa wabunifu na kuacha uzembe na kulalamika ili kujiletea maendeleo.

Alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, alipofungua warsha ya 24 ya watafiti wa masuala ya uchumi, watunga sera na viongozi wa serikali za mitaa iliyoandaliwa na Taasisi ya Utafiti ya Kuondoa Umaskini (Repoa).

Samia alisema utafiti wowote unaolenga kubadilisha maisha ya watu unafanyiwa kazi na serikali na kwamba bado unahitajika katika kipindi hiki cha mabadiliko makubwa ya kiuchumi.

Aliongeza kuwa serikali inatambua na kuheshimu utafiti uanaofanywa mara kwa mara na REPOA katika kukuza uchumi wa nchi.

Katika kulipa msukomo, aliahidi kwamba serikali itaendelea kuweka mazingira bora ili kuwezesha watafiti kufanya kazi kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania na kwamba utafiti wowote ulenge kuonyesha njia bora ya kufikia maendeleo ya kweli na si vinginevyo.

Kuhusu watu kuendelea kulalamika badala ya kufanya kazi, aliwataka kuacha kufanya hivyo badala yake wawe wabunifu na kujituma ili waweze kujikwamua kiuchumi. Akizungumza katika warsha hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Repoa, Dk. Donald Mmari, alisema taasisi yake itaendelea kushirikiana na wasomi wengine kufanya utafiti kwa ajili ya kukuza uchumi.

Alisema warsha hiyo inalenga kubadilishana uzoefu na viongozi wa serikali za mitaa pamoja na watunga sera ili kubaini namna bora ya kuzisaidia serikali za mitaa kujikwamua.

Katika warsha hiyo watoa mada 11 wakiwamo wa ndani na nje ya nchi walishiriki ili kueleza njia bora za kuzisaidia serikali katika kukuza uchumi.

Kwa upande wake, Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Serikali za Mitaa (Alat), Abdalah Ngodu, alisema kuna vikwazo viongozi katika ngazi za chini kufikia maendeleo ya kweli.

Alivitaja vikwazo hivyo kuwa ni pamoja na teknolojia duni ya kilimo, ukosefu wa umeme, soko la uhakika wa mazao ya wakulima.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SUMATRA
For Competitive, Efficient, Quality and Safe Transport Services
Surface and Marine Transport Regulatory Authority
Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini

TAARIFA KWA UMMA

MARUFUKU KUWATUMIA VISHOKA KUPATA HUDUMA ZA SUMATRA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) inatoa taarifa kwa wasafirishaji na Umma kuwa imebaini matukio kadhaa ya kitapeli yanayofanywa na vishoka katika baadhi ya ofisi za SUMATRA.

Wasafirishaji na watendaji wao wanaelekezwa kuhakikisha wanahudumiwa ndani ya ofisi za Mamlaka tu. Aidha hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mtu yeyote atakayebainika kushawishi kumsaidia mteja wa SUMATRA nje ya ofisi kinyume na taratibu.

Imetolewana:

Salum S. Pazzy
Kny: MkurugenziMkuu,
SUMATRA

215169902

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Bravo JPM angalizo la imani za kishirikina

**JANA** Rais John Magufuli alitoa angalizo ambalo hakika lina ujumbe mzito kwa kila Mtanzania katika jitihada za kupinga vitendo vya imani za kishirikina, ambazo zimeshamiri katika maeneo kadhaa nchini.

Rais Magufuli akiwa mkoani Njombe mchana katika hafla ya kuweka mawe ya msingi ya ujenzi wa hospitali ya rufani ya mkoa huo, pamoja na barabara kutoka Njombe-Moronga- Makete yenye urefu wa kilomita 107, aliwaonya wakazi wa Mkoa wa Njombe kuachana na imani za kishirikina ambazo zimeshamiri na kusababisha vifo vya watu wasio na hatia hususan watoto wadogo.

Katika hotuba yake, Rais Magufuli alikumbushia matukio ya hivi karibuni ya mauaji ya watoto yaliyotokea mkoani humo na kusababisha hofu kubwa, ikiwamo kuathiri shughuli za maendeleo.

Alizitaka jamii za mkoa huo kujitathmini na kuwa na roho ya huruma kwa watoto, akisema inashangaza kuona mtu anaua mtoto wa mwenzake kwa imani kuwa atapata utajiri.

Huku akionyesha kukasirishwa na vitendo hivyo, Rais Magufuli alisema ingawa hajawahi kusaini hukumu ya kifo tangu aingie madarakani, lakini anaweza kufika mahali akashindwa kuwa na uvumilivu akipelekewa hukumu za makosa ya kikatili kama mauaji ya watoto.

Aidha, Rais Magufuli aliwataka wananchi waliohudhuria kusimama na kutubu kwa Mwenyezi Mungu kutokana na matukio hayo, ambapo mmoja wa viongozi wa dini aliongoza sala ya kutubu.

Onyo la Rais dhidi ya vitendo vya mauaji ya kikatili kutokana na imani za kishirikina limetolewa kwa wakati, na halipaswi kuwalenga wakazi wa Mkoa wa Njombe pekee, bali nchi nzima.

Tunasema hivyo kwa sababu vitendo hivyo vimeendelea kushamiri nchi nzima. Vyombo vya habari kila uchao vinaripoti matukio ya kikatili ya mauaji, ubakaji wa watoto, ulawiti na kuwanajisi. Kadhalika, ripoti kadhaa za mashirika kadhaa yakiwamo ya kutetea haki za binadamu zimekuwa zikibainisha kasi ya kushamiri kwa vitendo hivyo.

Matukio mengi ya aina hii yanatokea zaidi katika maeneo ya uchimbaji madini, biashara, uvuvi na shughuli nyingine za kiuchumi kutokana na imani potofu kuwa kuua mtu na kumtoa viungo kunamwezesha mhusika kupata utajiri.

Imani hizi ni potofu na kama hazitadhibitiwa zitakwaza maendeleo ya watu binafsi na taifa kwa ujumla, hivyo jambo la msingi ni kuzingatia angalizo la Rais Magufuli.

Wananchi kamwe wasiwasikilize watu wanaojiita waganga na pamoja na wapiga ramli chonganishi, ambao ni kichocheo cha imani hizo potofu na zisizo na tija.

Tunaamini kuwa baada ya toba ya Njombe jana, wale wote wanaoendekeza imani potofu za kishirikina watajirudi na kurejea kwenye mstari.

Tunaamini kuwa wenye masikio wameusikia ujumbe wa Rais, hivyo hawatajihusisha tena na vitendo hivyo kwa kuwa hata hukumu ngumu zinazotolewa na mahakama hususani ya kifo itafika mahali Rais Magufuli atazisaini.


Kwa jamii ambazo hazitakubali kubadilika katika hili, itafika mahali zitaonekana za ajabu na sizizostaarabika.

Tunampongeza sana Rais Magufuli kwa kutumia fursa ya mkutano wake kuzungumzia matukio ya aibu yaliyotokea Njombe na kuacha simanzi kubwa kwa baadhi ya wazazi ambao walipoteza watoto wao, pamoja wananchi ambao shughuli zao ziliathirika.

Viongozi wengine wa serikali, dini, vyama vya siasa na wengine waone mfano wa Rais wa kuwa na ujasiri wa kukemea hadharani vitendo vyote vyenye mlengo wa kutishia amani na usalama.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



## Ndivyo vijiwe vinavyowaweka pabaya vijana wetu shuleni

Na Sabato Kasika

**MAKONDAKTA** na madereva wa daladala jijini Dar es Salaam, wanalalamikiwa kwamba wananyanyasa wanafunzi kwa kuwazuia kupanda magari hayo na kusababisha ama kutowahi masomo shuleni au kurudi nyumbani.

Hivyo ndivyo vimekuwa vikieleweka na ndivyo baadhi yao wamekuwa wakinyanyasa wanafunzi na kuwasababishia usumbufu usio wa lazima kwa madai kwamba nauli wanayoitoa ya Sh. 200 ni ndogo.

Pamoja na hilo, kuna vituko ambavyo huenda wazazi na walezi hawavijui, vimekuwa vikifanywa na baadhi ya wanafunzi na inawezekana wanachelewa kufika shuleni au nyumbani, wakisingizia kukosa usafiri wa daladala.

Wapo baadhi ya wanafunzi wa kike na kiume, ambao hukaa kwenye vituo vya daladala 'wakipiga soga' hata kama wakiitwa kupanda daladala kwenda shule au kurudi nyumbani, huwa wanasuasua.

Katika mazingira hayo, ni lazima watachelewa kuhudhuria masomo shuleni au kuchelewa kufika nyumbani na labda hujitetea kwamba wanakosa usafiri kwa kuzuiwa na makondakta na madereva.

Kwa mfano, kwenye barabara itokayo Masana kwenda Goba hadi Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam, baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakiitwa kupanda daladala, lakini wanakataa, hali inayotia shaka.

**Wanafunzi hao huwa na mazungumzo ya aina gani vituoni hadi wasipande magari kuwahi nyumbani? Kwa hali kama hii nitakuwa sikosei nikisema hao ndio wanaosingizia kukosa usafiri, ili kuhalalisha mambo yao.**

Wanafunzi hao huwa na mazungumzo ya aina gani vituoni hadi wasipande magari kuwahi nyumbani? Kwa hali kama hii nitakuwa sikosei nikisema hao ndio wanaosingizia kukosa usafiri, ili kuhalalisha mambo yao.

Kuna haja ya wazazi kuwafuatilia kwa karibu kwa kuwa vinginevyo wanaweza kujikuta kwenye matatizo yasiyotarajiwa, ikiwamo kupata mimba na wengine kujiingiza kwenye makundi yasiyofaa.

Wakijiingiza huko, wanaweza kuwa katika hatari kubwa kiafya, zitokanazo na mimba za utotoni. Pia, waliojiingiza kwenye makundi ya kihuni, watajikuta wanavuta bangi na dawa za kulevya, inayowaathiri kiafya.

Kwa mustakabli huo, sasa wakishafikia mazingira hayo, ni wazi wako kwenye hatari kubwa, hivyo wazazi na walezi wawe makini wasikubali kuambiwa na watoto wao kwamba wamechelewa kwa sababu ya kukosa usafiri.

Wapo kweli wanaochelewa kwa sababu hiyo, pia wengine hukataa kupanda magari na kubaki vituoni, wakiendelea 'kupiga soga', ambazo sijui zinazohusu masomo au mambo wanayojua wenyewe.

Kimsingi mwanafunzi anatakiwa kwenda shule na kurudi nyumbani kwa wakati, lakini anapochelewa na kusingizia ukosefu wa usafiri kwamba anazuiwa na makondakta na madereva, anakuwa anawaonea.

Mtindo wa kusingizia ukosefu wa usafiri ina maana kuna mambo mengine wanayofanya bila wazazi na walezi kujua, hivyo ni muhimu wafuatilie hali hiyo, kwani wanaweza kugundua uozo unaofanywa na watoto wao.

Hata kama wanashinda vituoni kwa lengo zuri, lakini wajue mazingira ya aina hiyo ya kurudi nyumbani muda mbaya siyo salama kwao, kwa kuwa wanaweza kukutana na vishawishi vya kuwaingiza katika hatari zaidi.

Wanapopata mimba za utotoni au kujiingiza katika makundi ya uvutaji bangi na dawa za kulevya, maana yake ni kwamba hatima ya maisha yao ya baadaye inaweza kuwa mbaya. Dawa ni kuviacha vijiwe hivyo mapema.

Mara nyingi vijiwe vinawapoteza, havina mwisho mzuri kwa wanaoviendekeza, kwa hiyo wazazi na walezi wasiridhike na watoto wao wanaowaambia kuwa wanachelewa kwa sababu ya usafiri, bali watafute njia ya kujiridhisha, ingawa kuwa ukweli, baadhi ya daladala ni kero kwa wanafunzi.

## BARUA/MJADALA

# Barabara Nyerere daladala 'zinatanua'

**Mhariri,**

*KATIKA siku chache zilizopita tunaendelea kushuhudia mvua zinazonyesha katika sehemu mbalimbali nchini. Ni neema, kwani inaambatana moja kwa moja na ustawi wa uchumi kitaifa.*

*Hiyo maana yake ni kwamba, mvua ambayo tulikuwa tukiiomba katika sura ya kimazingira na kiuchumi, ina maana kubwa, ingawaje baadhi ya wakazi wa mijini wanaiona hiyo kama si habari njema kwao.*

*Tutakumbuka kuna wakati mvua zilipogoma, wengi tulihaganika sana katika kutafuta mvua hiyo. Leo hoja yangu iko barabarani katika nidhamu ya uendeshaji magari.*

*Mara zote inajulikana katika eneo la barabara, kunyesha mvua, imekuwa na uhusiano wa moja kwa moja na hatari ya ajali, hasa kutokana na kuwepo tope jingi, pia barabara kuteleza kila wakati.*

*Kingine ambacho kinanisikitisha hivi sasa, nikitoa uzoefu wa uendeshaji katika Barabara ya Nyerere kila mvua zinaponyesha, mengi yananabia ya 'kutanua' hasa wakigundua askari wa usalama barabarani wamepisha mvua, madereva nao wanatumia mwanya kuasi sheria za barabarani kwa maslahi yao.*

*Nimeliona hilo na hasa muda wa usiku, daladala kati ya Daraja na Mfugale na Njia Panda za Jet, daladala 'zinatanua' na baadhi zinapita njia za kando, ambako haruhusiwi kupita.*

*Ni mambo ambayo yalishadhibitiwa na nina pongezi za kipekee kwa askari trafiki ambao wanafanya kazi nzuri sana.*

*Katika hilo linalofanyika kupitia barua hii, naomba nifungue macho wajue kinachofanyika, sasa imekuwa tabia inayotawala kwa kina. Dalili za ajali na kuzalisha foleni zinarudishwa.*

**Mahamudi Jumbe,**
**Chanika, Dar es Salaam.**

## WASILIANA NASI:

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Tunaendaje na 'baibai' ya mifuko ya plastiki?

**Na Lazaro Mateko**

BAADA ya kilio cha muda mrefu kuhusu madhara ya kiafya yatokanayo na mifuko ya plastiki, hatimaye serikali imeweka rasmi, kuanzia Juni Mosi mwaka huu haitakiwi tena ama kutengeneza au kuuzami fuko hiyo.

Tarehe hiyo ilitangazwa juzi na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiweka bayana mwisho wa mifuko hiyo kutumika kubebea bidhaa mbalimbali. Malalamiko kuhusu madhara yatokanayo na mifuko hiyo ni ya muda mrefu na serikali imekuwa ikifanya jitihada za kuikomesha,lakini bado hazijazaa matunda.

Kwa ng'ambo ya pili huko Unguja na Pemba, nako Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) ni marufuku siku nyingi. Lengo lililoanikwa na serikali liko bayana, ni kunusuru afya za Watanzania, kuanzia sura ya mazingira.

Wataalamu wa afya wanasema, licha ya mifuko hiyo kutumika kwa mengi, ikiwamo kuhifadhi vitu, inamadhara makubwa kwa afya ya binadamu. Kwa mujibu wa utafiti uliowahi kufanywa na Jumuiya ya Madaktari wa Marekani, ulitoa tahadhari kuhusu matumizi ya vyombo vya plastiki vinavyotumika kufungashia na kubebe vyakula.

Wanasema plastiki inamadhara makubwa endapo ikikutana na joto kali na kutoa kemikali iitwayo BPA au 'Bisphenol A.' Aidha, wanasema plastiki hizo zimetengenezwa kwa kemikali zaidi ya 200, zinazoweza kusababisha aina 100 za saratani, pia kwa kina inachangia kuharibu ukuaji wa mfumo wa uzazi,hususan kwa watoto ambao bado hawajazaliwa. Mengine ni mabadiliko ya 'kijenetiki' na kushindwa kuona, uyeyushaji chakula tumboni kuwa tabu au kutokamilika, halikadhalika kushindwa kufanya kazi vizuri.

Ni kweli, watu wengi wanatumia vifaa vya plastiki, bila ya kujua madhara yake. Mtu akienda katika nyumba mbalimbali, atakuta wanachemsha maji na kuyahifadhi katika ndoo za plastiki ya moto.

Wengine wanatumia mifuko hiyo kubebea vyakula vya moto. Yote hayo ni hatari kwa afya zao na inawezekana wakafanya hivyo,kwa kutojua madhara ya mifuko hiyo, kwasababu hawajaelimishwa au wakati mwingine ni tabia ya kutozingatia maelekezo.

Nakumbuka,Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, January Makamba,alishakaririwa na vyombo vya habari,kwamba mifuko hiyo imekuwa na changamoto kubwa ya mazingira. Sababu kuu ipo wazi, inatolewa bure, inasambaa na kusababisha mafuriko na athari nyingine kubwa za kimazingira.

Umefika wakati, wahusika kuzingatia marufuku iliyotangazwa na waziri mkuu na tusiegemee kuangalia biashara tu.

Inawezekana Juni Mosi ikafika, wakajitokeza wazalishaji. Hilo halikubaliki! Tuna mifano hai, wapo wauzaji nguo za mitumba za ndani zilipopigwa marufuku,wakaja na njia zingine kutaka kuzirejesha.

Hiyo ilikuwa mwaka 2013, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) liliwaongezea muda. Muda wa marufuku ulishafika, lakini wapo walioendelea kuingiza nchini nguo hizo hadi leo. Zipo baadhi ya nchi zaAfrika, zikiwamo Kenya na Rwanda, ambazo zimefanikiwa katika kukomesha uzalishaji wa mifuko ya plastiki, Hapo ndipo najiuliza, kwanini Tanzania ishindwe? Jambo la msingi, ni kwamba wahusika wazingatie maelekezo yaliyotolewa na serikali, pia watumiaji wa mifuko hiyo waelewe kuwa,siyo kwamba inachafua mazingira tu,bali inamadhara kwa afya zao.

Inawezekana, wakawapo wanaohoji kama kweli mifuko hiyo inamadhara, kwanini kuna viwanda vinaitengeneza?Swali la aina hiyo, linahojiwa na wavutasigara kama zinamadhara, kwanini kilimo cha tumbaku kinaendelea na kuna viwanda vya kutengeneza sigara?

Maswali aina hiyo yanaweza kuwa na maana kwa lengo la kujua madhara yatokanayo na bidhaa hizo, lakini jambo la msingi ni kwamba, ni vyema kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya ili kuepuka madhara.


MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD

## NOTISI/TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD** tunatangaza kuuza dhamana za wadaiwa sugu walioshindwa kulipa mikopo yao katika Benki tajwa hapo juu kama watashindwa kulipa madeni yao ndani ya siku 14 tangu kutolewa kwa tangazo hili. Minada hii itafanyika kama inavyoonesha hapa chini;

| S/N | JINA LA MTEJA | UMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIKO | TAREHE NA MUDA WA |
|---|---|---|---|---|
| 001 | VICKIY SILIVESTI MUSHI (TAWI LA TANDALE) | VICKIY SILIVEST MUSHI | KIWANJA CHENYE HATI YA MAUZIANO, KILICHOKO MTA WA KIFURU WILAYA YA ILALA | 25/04/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 002 | MOHAMED RAMADHANI NKUSA (TAWI LA BUGURUNI) | MOHAMED RAMADHANI NKUSA | KIWANJA KICHOENDELEZWA CHENYE HATI YA MAUZIANO KILICHOKO KINYEREZI SONGASI—WILAYA YA ILALA | 25/04/2019 SAA 08:00 MCHANA |
| 003 | FRIDA AMON KAAYA (TAWI LAKINONDONI) | LISAMARIA JOSEPH | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA MADALE – WILAYA KINONDONI | 29/04/2019 SAA: 04:00 ASUBUHI |
| 004 | BEATRICE ANDREW MMASSY (TAWI LA TANDALE) | BEATRICE A. MMASSY | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MBEZI KWA YUSUFU- WILAYA YA UBUNGO | 29/04/2019 SAA 09:00 MCHANA |
| 005 | REVOCATUS LUCAS BIKEEZA (TAWI LA KINONDONI) | REVOCATUS LUCAS BIKEEZA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA KIPUNGUNI – WILAYA YA ILALA | 03/05/2019 SAA 09:00 MCHANA |
| 006 | ELLY JOHN MJEMA | ELLY JOHN MJEMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA YANGEYANGE KATA YA MSONGOLA – WILAYA YA ILALA | 06/05/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 007 | MZINGA ONE SERVICES AND GENERAL SUPPLIES | RICHARD KWEYAMBA RUGALABAMU | KIWANJA CHENYE HATI MILIKI NO.139603 PLOT 242 BLOCK 8 KILICHOKO MTAA WA MWONGOZO– WILAYA YA KIGAMBONI | 09/05/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |

**Masharti ya mnada**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote, ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki, na zingine zinazoambatana na hili ni juu ya mnunuzi.

**KWA TAARIFA ZAID WASILIANA NA:**

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, AU
MKURUGENZI MTENDAJI,
P.O BOX 669,
DAR ES SALAAM
Tel+255 02221183403

Maseto Auctioneer,
MKURUGENZI MTENDAJI,
P.O BOX 75087,
DAR ES SALA
+255 765 999 000 AU +255 787 288 442
AU +255 762 260 787

113860902



CAPITAL RADIO

**POPOTE ULIPO SIKILIZA CAPITAL RADIO KATIKA MASAFA YAFUATAYO**




www.capitalradioco.tz @capitalradiotanzania @CapitalRadiotz @capitalradiotz



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kabla ya kukabidhi pikipiki saba kwa Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Lazoro Mambosasa zitakazotolewa kama motisha kwa askari wa jeshi hilo, kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. **PICHA: NBC**

# Bodi ya Mikopo yashindwa kubaini wakopaji Tril. 1.46/-

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imeshindwa kufahamu waliko wakopaji wa mikopo ya elimu ya juu yenye thamani ya Sh. trilioni 1.46.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, aliyasema hayo jijini Dodoma jana alipokutana na waandishi wa habari kutoa mukhtasari wa ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2017/18.

"Kiasi hiki cha fedha ni kikubwa sana ikizingatiwa kuwa Kifungu cha 4(h) cha Sheria ya Bodi kinaitaka Bodi kutengeneza mtandao na kushirikiana na taasisi na mashirika mbalimbali ili kuwatambua wadaiwa na kuwezesha kupata marejesho ya mikopo hiyo," alisema.

Prof. Assad alisema HESLB inapaswa kushirikiana na taasisi na vyanzo vingine vya taarifa ili kuiongezea nguvu kwenye kanzidata yake kuwatambua wakopaji ambao hawajulikani waliko.

Kuhusu madeni ya watumishi wa elimu ya juu, Prof. Assad alisema kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2017/18, madeni yanayohusiana na malipo ya posho ya majukumu kwa wahadhiri wa Vyuo Vikuu vya Mzumbe na Ardhi yameongezeka.

Alisema katika Chuo Kikuu cha Mzumbe, madeni yameongezeka kutoka Sh. bilioni 1.49 hadi Sh. bilioni 3.41 na kwa Chuo Kikuu cha Ardhi, madeni yameongezeka kutoka Sh. bilioni 1.48 hadi Sh. bilioni 2.26.

"Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Mzumbe vilikuwa na madeni ya kiinua mgongo ya Sh. bilioni 5.59 na Sh. milioni 525 mtawalia kwa wafanya kazi ambao wamemaliza mikataba yao," alisema.

Alibainisha kuwa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kilikuwa na madeni ya Sh. bilioni 6.78 ikiwa ni posho za nyumba na madeni mengineyo ya wafanyakazi tangu Juni mwaka 2017. CAG alisema hali hiyo inaweza kusababisha kushuka kwa kiwango cha elimu ya juu kutokana na wahadhiri kukosa morali ya kazi.

**MALIPO HEWA BIMA YA AFYA**

Prof. Assad pia alisema uchunguzi wa vitabu vya fedha, taarifa za benki na hati za malipo za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, ulibainika kuwapo kwa malipo ya kiasi Sh. bilioni tatu.

Kati yake, Sh. bilioni 2.61 ni malipo hewa, Sh. milioni 350.8 ni malipo ambayo walipwaji hawakubainika na Sh. milioni 42.6 hazikuthibitika kupokewa na walipwaji.

CAG alisema malipo hayo yalitakiwa kulipwa kwa watoa huduma za afya kwa kutumia hundi zilizofungwa, lakini yalifanywa kwa fedha taslimu kinyume cha Kanuni za Fedha za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Pia, makusanyo ya mwaka yanaendelea kuwa makubwa zaidi ya malipo ya huduma za bima ya afya, ambapo kwa sasa malipo ya huduma za afya yanakua kwa uwiano mkubwa mwaka hadi mwaka, zaidi ya uwiano wa kukua kwa mapato.


Land Form No. 64 A

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
THE LAND ACT, 1999
(NO. 4 OF 1999)

NOTICE OF DEFAULT
[Under Section 127]

C.T. NO 17617-MBYLR,
L.O. NO.377882,
PLOT NO. 123, IYUNGA AREA, MBEYA CITY.

C.T. NO 164226-MBYLR,
L.O. NO. 528879,
PLOT NO. 293, KWEMBE AREA, KINONDONI MUNICIPALITY

To: Atupakisye Josiah Mwamgogwa,
P.O. Box 898,
Mbeya, Tanzania

This is to notify on your default to honour obligations covenanted under the mortgage deed dated 17th October 2016 and 25th October 2017, namely to assure the payment of the credit facilities granted to Juliana Input Co. via the offer letter dated 13th November 2017, which was secured by a mortgage created over the properties stated herein above. Juliana Input Co. have defaulted in their obligation to pay the amount in excess, arrears and the interest thereon totalling TZS 271,237,592.38/= (Tanzania Shillings Two Hundred Seventy One Million Two Hundred Thirty Seven Thousand Five Hundred Ninety Two Thirty Eight Cents Only) as of 05th April 2019. Further to that, the said credit facility was secured by a mortgage deed created over properties registered in your name, registered on 17th October 2016 and 26th October 2017 under File Document No.24881-MBYLR and 192235 on the properties stated herein above.

Be further notified that in the event Juliana Input Co. does not rectify the default stated above within SIXTY (60) DAYS from receipt of this notice, we may exercise our right to sell the mortgaged property cited above, or appoint a receiver, or lease the property or enter possession.

Dated at NMB BANK PLC HQ this 05th day of April 2019

NMB BANK P.LC
(MORTGAGEE)

Received this at .................... this ......... day of .................... 2019

ATUPAKISYE JOSIAH MWAMGOGWA
(MORTGAGOR)

21517060?


## Sala yamwokoa OCD Njombe

INATOKA UK. 4

alishindwa kusimamia hii kazi, nimemleta RPC mpya, Salum Hamduni," alisema.

"Ninataka mambo yawe yanatendeka haraka, mtoto anapotea wa kwanza, wa pili mpaka wanafikia saba, wewe RPC mbona watoto wako hawajapotea angepotea mke wako au mume wako usingechangamka.

"Ni lazima watu tuchukue hatua, haiwezekani tulete polisi kutoka Dar es Salaam kwa ajili ya operesheni kuja kusimamia usalama hapa Njombe askari wa hapa wapo, halafu RPC una nyota, haiwekani," alisema.

Rais Magufuli alisema wanawake ambao wamepotelewa na watoto wao wameumia na mkoa huo umepata doa kubwa.

"Siku nyingine yakitokea matukio ya aina hii Mkuu wa Mkoa unaondoka, DC (Mkuu wa Wilaya) unaondoka DAS (Katibu Tawala) unaondoka, Katibu Tarafa unaondoka, mpaka Mwenyekiti wa Kijiji, ikiwezekana na Katibu wa CCM wote wanaondoka, ili kusudi ifike mahali tuwe tunachukua hatua haraka," alisema.

Rais Magufuli aliwaeleza wananchi wa mkoani humo kuwa hawawezi kutajirika kwa kuua watoto.

"Saa nyingine unaua mtoto wako ni mambo ya ajabu sana, sijatia saini mtu kunyongwa, lakini nikiletewa kesi kama hizi nitamuomba malaika wangu inawezekana nikasaini. Haiwezekani tukaendeleza mambo ya kishirikina kwamba nikiua mtoto ndipo nitapata mahindi mengi, ni ujinga mwingine unaua mpaka mtoto wa ndugu yako," alisema.

Aliwaeleza wananchi hao kuwa mambo ya ushirikiana hayana tija na kuwaomba viongozi wa dini waendelee kuhubiri mapendo ya kweli kwa waumini.

Alisema katika mkoa wa Njombe mambo mengine ni supa, lakini mauaji ya watoto hao yameweka doa.

"Mtu anakuuliza umetoka wapi unajibu Njombe, hata kama hajakwambia anakumbuka vifo vya watoto. Muone aibu kwenye hili na watu wa kupiga vita ni nyinyi wenyewe, tutawaonea polisi tutawahamisha, lakini tatizo lipo kwenu wakati mwingine hamtoi ushirikiano, kitendo hiki kisijirudie tena, watoto badala ya kwenda shule wakiwa na raha wanacheza, mpaka wanasindikizwa na mama yao mtalima saa ngapi, siku anasindikiza baba siku anasindikiza mama, ni mateso," alisema.

Rais Magufuli alisema Njombe wameweka doa ambalo lazima wasali, watubu ili Mungu awasamehe.

"Ninaomba kama kuna mchungaji hapa au sheikh tusimame wote aongoze toba sisi wote kama taifa pamoja na mimi kuongoza watu wanaouana na mimi ninatubu, tusimame wote wasiyesimama ndiye miongoni mwa wauaji," alisema.

**MKANDARASI KUCHUNGUZWA**

Katika hatua nyingine, Rais Magufuli, ameiagiza Bodi ya Makandarasi kumchunguza Mkandarasi Masasi ambaye alipewa kazi ya kujenga stendi na baadaye kuondolewa kutokana na kazi zake kuchukua muda.

# Takukuru ilivyorejesha shamba la wananchi

**Na Khadija Kalili,** KIBAHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Pwani, imefanikiwa kulirejesha shamba kwa wanakijiji ambalo liliuzwa kwa mwekezaji bila kufuata utaratibu wa kijiji katika Wilaya ya Kisarawe.

Hayo yalisewama na Kamanda Wa Takukuru Mkoa wa Pwani, Susan Raymond, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alilitaja jina la mwekezaji huyo kuwa ni Ibrahim Ismal, ambaye alikuwa anataka kuwekeza kwenye shamba hilo lenye thamani ya Sh. milioni 80 lililokuwa katika kijiji cha Kibwemwende wilayani Kisarawe Mkoa wa Pwani.

Alisema baada ya uchunguzi uliofanywa na Takukuru, shamba hilo limerudishwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe na kisha litarejeshwa katika himaya ya kijiji hicho.

"Mbali na tukio hilo, ofisi yetu kwa kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu imefanikiwa kuokoa fedha kiasi cha Sh. 63, 611,110 ambazo zilitokana na faini na kodi zilizolipwa serikalini baada ya kukamata mazao ya misitu yaliyokuwa yakisafirishwa kinyume cha utaratibu," alisema Raymond.



Rais John Magufuli (kushoto) akimsikiliza Mkurugenzi Mkuu wa Unilever Tea Tanzania, Ashton Eastman, wakati wa uzinduzi wa kiwanda cha kuchakata chai cha Kabambe mkoani Njombe juzi. Kiwanda hicho ni moja ya viwanda vinavyomilikiwa na Unilever Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Msitu wa Pugu mbioni kuwa hifadhi

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), uko katika mkakati wa kuupandisha hadhi Msitu wa Hifadhi wa Pugu kuwa msitu wa hifadhi ya mazingira asilia.

Meneja Masoko wa TFS, Mariam Kobelo, alisema hayo mbele ya waandishi wa habari na wanafunzi wa Shule za Sekondari za Minaki na Pugu, waliotembelea msitu huo.

Alisema endapo utapandishwa hadhi, utatoka katika hatua ya hifadhi ya msitu na kuwa msitu wa hifadhi ya mazingira asilia, hivyo kutumika kwa utalii zaidi kwa ajili ya utafiti, elimu na ikolojia na hautatumika tena kwa shughuli za kibinadamu. "Ukiwa chini ya msitu wa mazingira asilia utakuwa chini ya uangalizi madhubuti, haitoruhusiwa shughuli zozote za kibinadamu kufanyika ndani ya msitu huu, isipokuwa shughuli za kitafiti, elimu na Ikolojia," alisema Mariam na kuongeza:

"Nawaambia Watanzania kwamba wanakosa kufahamu vitu muhimu kwa kushindwa kutembelea hifadhi za misitu. Kuna faida nyingi katika misitu ambazo watu wengi hawazijui na msitu huu ndiyo 'mapafu' ya Jiji la Dar es Salaam, kwa hiyo ni vema kujenga tabia ya kuitembelea, wasikariri kwamba utalii ni wanyama tu."

Alisema hifadhi ya msitu wa Pugu mbali na kuwa na vivutio vya miti adimu, lakini vivutio vingine vilivyomo katika msitu huo ni mapango ya popo ambayo zamani yalikuwa yanatumika katika shughuli za uchimbaji wa madini.

"Ndani ya misitu hii kuna vitu vya kufurahisha, kuna mabwawa humu, tuna ndege wa kuvutia, vipepeo wa kipekee, digidigi, kuna mapango ya popo ambayo zamani yalikuwa yakitumika kuchimba madini," alisem Mariam.

Alisema TFS imetoa fursa kwa wawekezaji kujitokeza kuchangamkia fursa ya kuwekeza katika sehemu za hifadhi za misitu kwa kujenga hoteli na kuanzisha huduma mbalimbali za jamii katika maeneo hayo.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha huduma zote za kijamii zinapatikana katika maeneo hayo ili kuepusha usumbufu kwa watalii wanaokwenda kufanya utalii katika hifadhi za misitu.

Afisa Misitu Mkuu wa kitengo cha Ugani na Uenezi TFS, Shabani Kiula, alisema utalii mwingine ambao ni maarufu katika msitu huo ni pamoja na uwapo wa mapango ambayo yamekuwa yakitumika katika ibada.

# Magufuli akifagilia kiwanda kipya chai

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

RAIS John Magufuli ameipongeza Kampuni ya Unilever Tea Tanzania kwa kujenga kiwanda cha kisasa cha kuchakata majani ya chai mkoani Njombe, na kuwataka watendaji Serikali kupunguza urasimu na vikwazo kwa wawekezaji wanaotaka kuwekeza nchini.

Aliyasema hayo mkoani hapa alipofanya uzinduzi wa kiwanda cha chai cha Kabambe na kuwataka watendaji wa Serikali kutowabughudhi wawekezaji wenye nia ya kuwekeza nchini.

Alisema mwekezaji atakayekwamishwa na mtendaji yeyote wa serikalini atoe taarifa katika ofisi yake ili hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya huyo mtumishi ambaye anakuwa kikwazo cha uwekezaji nchini.

Aliongezea kuwa Serikali inapaswa kuandaa mpango kazi utakaotoa mwongozo wa namna bora ya kulinda mazingira ya uwekezaji nchini na mikakati ya kuvilinda viwanda vitakavyojengwa kama cha Kabambe cha kuchakata chai.

"Zaidi ya Bilioni 49 zimewekezwa katika kiwanda hiki hivyo ni lazima kuwe na mazingira bora ya kukilinda kiwanda hichi kwa hali yoyote ili kiendelee kutoa ajira kwa Watanzania na kupeleke azma ya Serikali ya kujenga viwanda kutekeleza kwa vitendo," alisema Rais Magufuli.

Aidha, Alipongeza Ubalozi wa Uingereza nchini, The Wood Foundation, Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu, Balozi Phillemon Luhanjo, Spika wa Bunge mstaafu, Anna Makinda, Kituo cha Kuendelea Kilimo Nyanda za juu kusini mwa Tanzania (SAGCOT) kwa kuwezesha kuwapo kwa kiwanda hicho mkoani Njombe.

"Niwatake wakulima wa chai mkoani Njombe kulima zao hili kwa wingi kutokana na uwapo wa kiwanda cha kisasa cha kuchakata chai zaidi ya tani 150,000 ambapo asilimia 70 ya majani mabichi yanategemewa kutoka kwa wakulima hali inayoibua fursa ya soko la majani mabichi," alisema.

Alisema kiwanda cha Kabambe kitapelekea kipato kwa mkulima mdogo kuongezeka na kuchochea ukuaji wa uchumi wa mkoa na taifa kwa ujumla kupitia kodi zitakazolipwa na kiwanda, hali itakayopelekea nchi kupiga hatua kiuchumi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Unilever Tanzania, David Minja, alisema kampuni imetoa ajira zaidi ya Watanzania 7,000 na kunufaisha watu zaidi ya 40,000 kupitia kampuni za Unilever Tanzania kikiwapo kiwanda cha kuchakata chai cha Kabambe.

"Tumejipanga katika kutoa mafunzo na elimu ya kilimo bora cha chai ili wakulima waweze kulima chai yenye ubora utakao kubalika na kupelekea soko la chai kuwa nzuri na kuwanufaisha wakulima kwa kupata vipato vya juu," alisema Minja.

Alisema changamoto kubwa ni miundombinu ya barabara ya kutoa chai mashambani na kufikisha kiwanda kwa wakati hali inayopelekea chai nyingi kuharibika kabla ya kufika kiwanda kwa ajili ya kuchakatwa hivyo kumpelekea mkulima hasara.

Balozi wa Uingeraza nchini, Sarah Cooke, alisema kufanikiwa kwa uwapo wa kiwanda cha kuchakata chai kutachochea wawekezaji wengi zaidi kutoka Uingereza kuja kuwekeza Tanzania kutokana na uongozi mzuri wa Rais Magufuli katika kusimamia sera ya viwanda.

# Serikali: Mafuta ghafi ni suala la Muungano

BUNGE limeelezwa kuwa kwa mujibu wa Katiba iliyopo, suala la utafutaji na uzalishaji mafuta ghafi ni la Muungano.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alitoa kauli hiyo alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Bumbwini (CUF), Muhamed Amour Muhammed.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema kwa kuwa suala la mafuta ni la Muungano na kwamba kumekuwapo na taratibu mbalimbali zinazofanywa ili kutafuta mafuta nchini.

"Je, ni taratibu zipi zilizopaswa kufanyika ili kuthibitisha mafuta yatapatikana katika eneo husika?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Mgalu alisema serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, mwaka 2015 kwa nia njema ya kuongeza ufanisi na tija katika shughuli za kutafuta na uzalishaji mafuta ghafi.

Aidha, alisema zilikubaliana kuwa kila upande usimamie, shughuli hizo Kwan kutumia sheria na taasisi zake.

Hata hivyo, alisema ili kuthibitisha mafuta yanapatikana katika eneo husika, taratibu mbalimbali hufanyika.

Alitaja taratibu hizo ni utafiti wa awali wa kukusanya sampuli za kijiolojia na kijiochemia, kukusanya data za kijiofizikia, kufanya tathmini ya data za kijiolojia na kijiofizikia.

Pia, alisema kutambua maeneo ya mashapo katika miamba tabaka ambapo mafuta au gesi inaweza kukusanyika kufuatia matokeo ya tathmini ya data za kijiolojia na kijiofizikia na kuchimba visima vya utafiti katika maeneo yalikotambulika mashapo ili kuthibitisha uwapo wa mafuta ghafi au gesi asilia.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Watu Wenye Ulemavu, Stella Ikupa, akitoa ufafanuzi bungeni juzi wakati wa kujibu hoja mbalimbali za wabunge kuhusu uboreshwaji wa kitengo cha watu wenye ulemavu. **MPIGAPICHA WETU**

# Matuta 300 tishio usalama barabarani

WIZARA ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) imepitia upya matuta yote yaliyojengwa katika barabara kuu nchini na kubaini matuta 323 siyo rafiki kwa vyombo vya usafiri.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Elias Kwandikwa, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Temeke (CCM), Abdallah Mtolea.

Mtolea katika swali lake alisema serikali inajitahidi kujenga barabara ili kupunguza foleni pamoja na kurahisisha usafiri na usafirishaji, lakini barabara zinawekwa matatu ambayo si rafiki kwa vyombo vya usafiri.

"Jambo linalosababisha baadhi ya watumiaji wa barabara hizo kuzikimbia kwa mfano, matuta yaliyowekwa katika barabara Msata-Bagamoyo.Je, matuta ni sehemu ya alama za barabarani?"alihoji.

Akijibu swali hilo, Kwandikwa alisema kazi ya uboreshaji wa matuta hayo inaendelea ambapo hadi sasa matuta 281 yamerekebishwa.

"Baadhi ya barabara ambazo matuta yamerekebishwa ni Kibaha-Mlandizi (6), Morogoro-Iringa (12), Mara-Simiyu (12), Igawa-Songwe (3), Uyole-Kasumulu (2), Mwanza- Simiyu (9), Shelui-Nzega (5), Singida-Manyara (23), Mutukula-Bukoba-Kigoma (7) pamoja na maeneo mengine 202," alisema.

Naibu Waziri Kwandikwa alisema kwa kutambua kuwa baadhi ya matuta ya barabarani siyo rafiki kwa vyombo vya usafiri, Serikali iliandaa mwongozo wa usanifu wa barabara wa mwaka 2011 ambao pamoja na mambo mengine, umeweka viwango bora vya ujenzi wa matuta barabarani.

Alisema alama za barabarani hutumika kutoa ujumbe wa matumizi sahihi ya barabara katika eneo husika.

"Alama hizo huwekwa kwenye milingoti pembezoni mwa barabara au huchorwa katika uso wa barabara kutoa tafsiri sahihi ya matumizi ya barabara," alisema.

Hata hivyo, alisema kutokana na baadhi ya madereva kutozingatia alama za barabarani hususan alama za ukomo wa mwendo, serikali hulazimika kujenga matuta katika maeneo ambayo ni hatarishi ili kuwalazimisha madereva kupunguza mwendo.

Alimhakikishia Mbunge huyo na wananchi kwa ujumla kuwa matuta yote ambayo hayastahili kuwapo barabarani yataondolewa na yale ambayo hayakidhi viwango yatajengwa upya.

Alitoa wito kwa madereva wote nchini kuzingatia alama za barabarani ikiwamo alama za mwendo.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

## Wosia changamoto wanawake, watoto

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM) Fatma Toufiq, amesema miongoni mwa sababu kubwa zinazosababisha wanawake na watoto kuporwa mali zao na ndugu za waume zao ni kukosekana kwa wosia. Akiuliza swali bungeni jana, Mbunge huyo alisema jambo hilo jamii haijaona umuhimu huo wakiamini kuwa kuandika wosia ni kujitakia kifo.

"Je, serikali ina mkakati gani endelevu wa kukabiliana na kadhia hii, je, Serikali itakuwa tayari kuielimisha jamii umuhimu wa kuandika wosia kama njia mojawapo ya kulikabili tatizo hilo ambalo ni kubwa katika jamii?" alihoji. Akijibu maswali hayo, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga, alisema serikali inatambua umuhimu wa kuandika wosia kama njia mojawapo ya kukabiliana na migogoro katika jamii inayohusiana na mgawo wa mali za marehemu.

Kwa kutambua hilo, Dk. Mahiga alisema mwaka 2008 Wizara kupitia Wakala wa Usajili, Udhamini na Ufilisi (RITA), ilianzisha huduma ya kuandika na kuhifadhi wosia ikiwa ni pamoja na kuuelimisha umma kuhusiana na huduma hiyo.

"Tangu wakati huo, Wizara yangu kupitia RITA imeendelea kubuni na kutekeleza mikakati ya aina mbalimbali ili kuhamasisha na kufikisha elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuandika na kuhifadhi wosia," alisema.

Alibainisha kuwa wamekuwa wakitumia njia mbalimbali kutoa elimu ya kuandika wosia ikiwa ni pamoja na mikutano ya hadhara, redio, televisheni, vipeperushi, magazeti na mitandao ya kijamii.

"Pamoja na jitihada hizo mpaka sasa tumeweza kuandika na kuhifadhi wosia 578, kati ya hizo wosia 33 tayari zimeshatumika," alisema.

Hata hivyo, alisema idadi hiyo ni ndogo ikilinganishwa na idadi kubwa ya Watanzania waliopo kwa sasa na bado kuna changamoto ya uelewa kwa wananchi wengi juu ya umuhimu wa suala hilo. Alisema Wizara itaendelea kubuni njia mbalimbali za kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuandika wosia ikiwa ni jitihada mojawapo ya kukabiliana na migogoro ya mgawo wa mali za marehemu.

Aliwaomba wabunge wote kuchangia katika juhudi zinazofanywa na serikali za kuhamasisha wananchi kujijengea tabia ya kuandika na kuhifadhi wosia sehemu maalum hadi utakapohitajika.

"Endapo wananchi watahamasika, tutakuwa tumeondokana na migogoro isiyo ya lazima na hivyo kuruhusu maendeleo na ustawi wa jamii,"alisema.

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

### OFISI YA RAIS,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, MHESHIMIWA SELEMANI SAIDI JAFO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAPITIO, MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20**

# VIONGOZI WA OFISI YA RAIS-TAMISEMI



WAZIRI WA NCHI, OR-TAMISEMI
MHE.SELEMANI S. JAFO (MB)



NAIBU WAZIRI, OR-TAMISEMI
MHE.JOSEPHAT KANDEGE (MB)



NAIBU WAZIRI, OR-TAMISEMI
MHE.MWITA WAITARA (MB)



KATIBU MKUU, OR-TAMISEMI
ENG. JOSEPH NYAMHANGA



NAIBU KATIBU MKUU (E), OR-TAMISEMI
TIXON NZUNDA



NAIBU KATIBU MKUU (A), OR-TAMISEMI
DKT.DOROTHY GWAJIMA

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, MHESHIMIWA SELEMANI SAIDI JAFO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAPITIO, MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20

**A. UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika;*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Ofisi ya Rais-TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2018/19. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.

**2.** ***Mheshimiwa Spika;*** napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kuiongoza Ofisi ya Rais-TAMISEMI ambayo ina wajibu wa kuwahudumia wananchi kiuchumi na kijamii.

**3.** ***Mheshimiwa Spika;*** kwa heshima kubwa naomba kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake imara, wenye weledi na umakini katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 ambao umeiwezesha nchi yetu kupiga hatua ya maendeleo katika utoaji wa huduma kwa Sekta zote. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna wanavyomsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia na kuongoza shughuli zote za Serikali ya Awamu ya Tano.

**4.** ***Mheshimiwa Spika;*** kipekee nakupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa hekima na busara mnazotumia kuongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, napenda kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa inayoongozwa na Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kuchambua na kujadili Bajeti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Maoni, ushauri na ushirikiano uliotolewa na Kamati umewezesha Wizara yangu kukamilisha maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 kwa ufanisi.

**5.** ***Mheshimiwa Spika;*** naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kwenye Chaguzi Ndogo akiwemo Mheshimiwa Mwita Waitara, Mbunge wa Ukonga, ambaye kwa sasa ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI anayeshughulikia huduma za Elimu na Utawala; Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli; Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini; Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti; Mheshimiwa Mhandisi Christopher Kajoro Chizza, Mbunge wa Buyungu; Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe; Mheshimiwa James Kinyasi Millya, Mbunge wa Simanjiro; Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Babati Mjini; na Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea, Mbunge wa Temeke.

**6.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika Mwaka 2018, Bunge lako Tukufu lilipata simanzi kutokana na kifo cha Mheshimiwa Stephen Hilal Ngonyani aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini na Mheshimiwa Kasuku Bilago aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Buyungu. Natoa pole kwako Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge na familia za marehemu kwa kuondokewa na wapendwa wao. Aidha, kwa masikitiko makubwa natumia fursa hii kuwapa pole wote waliopatwa na majanga ya ajali na kufiwa na ndugu, jamaa na wapendwa wao katika matukio mbalimbali hapa nchini. Mwenyezi Mungu awapokee na kuwahifadhi mahali pema peponi. Amina.

**7.** ***Mheshimiwa Spika;*** baada ya kusema hayo, sasa napenda kutoa maelezo ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 na Mpango na Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.

**B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19**

**8.** ***Mheshimiwa Spika;*** utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/19, ulizingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Pili wa Mwaka 2016/17 hadi 2020/21, Agenda ya Dunia ya Malengo Endelevu ya Maendeleo ya Mwaka 2030, Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, katika Mkutano wa 11 wa Bunge wa Novemba 2015, Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 na dhana ya Upelekaji Madaraka kwa Umma na Sera mbalimbali za Serikali.

**9.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri iliidhinishiwa kutumia **Shilingi trilioni 6.58** kwa ajili ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, jumla ya **Shilingi trilioni 4.13** ni Mishahara, **Shilingi bilioni 649.3** ni Matumizi Mengineyo na **Shilingi trilioni 1.80** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo kiasi cha **Shilingi trilioni 1.27** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 527.1** ni fedha za nje. Hadi Februari, 2019, jumla ya **Shilingi trilioni 3.43** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 52** ya Bajeti iliyoidhinishwa kwa mafungu yote ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

**Maduhuli ya OR-TAMISEMI na Mikoa**

**10.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Mikoa iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi bilioni 22.7.** Kati ya fedha **Shilingi milioni 20.0** ni Maduhuli ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI, **Shilingi bilioni 22.6** ni Maduhuli ya Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI na **Shilingi milioni 130.5** ni maduhuli ya Mikoa. Hadi Februari, 2019, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imekusanya jumla ya **Shilingi milioni 7.9** sawa na **asilimia 40** ya lengo, Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI zimekusanya **Shilingi bilioni 9.8** sawa na **asilimia 43** na Mikoa imekusanya jumla ya **Shilingi milioni 118.6** sawa na **asilimia 85** ya lengo.

**Mapato ya Ndani ya Halmashauri**

**11.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 735.6** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya ndani. Hadi kufikia Februari, 2019, Halmashauri zilikuwa zimekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 392.90** sawa na asilimia **53** ya makadirio ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.1).*** Kiasi kilichokusanywa ni ongezeko la **Shilingi bilioni 111.6** ikilinganishwa na kiasi cha **Shilingi bilioni 281.3** zilizokusanywa hadi Februari, 2018. Ongezeko la makusanyo limechangiwa na kuimarishwa kwa usimamizi na udhibiti, elimu na hamasa kwa walipa kodi na matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato. Aidha, mkakati uliowekwa na OR-TAMISEMI wa kuzishindanisha Halmashauri kila robo mwaka umesaidia kuongeza juhudi ya ukusanyaji wa mapato ya ndani miongoni mwa Halmashauri.

**Matumizi**

**12.** ***Mheshimiwa Spika;*** majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI yanatekelezwa katika ngazi ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI Makao Makuu, Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ofisi ya Rais-TAMISEMI Makao Makuu na Mikoa ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji unaofanyika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**13.** ***Mheshimiwa Spika;*** hadi Februari 2019, Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake zilikuwa zimepokea jumla ya **Shilingi bilioni 181.7** sawa na **asilimia 45.2** ya bajeti ya **Shilingi bilioni 402.3.** Vilevile, hadi Februari 2019, Tume ya Utumishi wa Walimu ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 5.6** sawa na **asilimia 45** ya Bajeti ya **Shilingi bilioni 12.5** zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Aidha, Mikoa 26 imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 144.3** kati ya bajeti ya **Shilingi bilioni 298.3** sawa na **asilimia 48.4.** Kadhalika, Halmashauri 185 zimepokea jumla ya **Shilingi trilioni 3.10** kati ya **Shilingi trilioni 5.88** zilizoidhinishwa sawa na **asilimia 52.7.**

**Utawala Bora na Demokrasia**

**14.** ***Mheshimiwa Spika;*** utawala bora ni nyenzo muhimu katika kuharakisha maendeleo endelevu ya nchi kwa kuzingatia misingi ya Sheria, uwazi na uwajibikaji ili kutoa huduma bora kwa wananchi. Malengo ya kijamii na kiuchumi hayawezi kufikiwa endapo itakosekana misingi ya haki, usawa, uwazi na uwajibikaji. Ofisi ya Rais-TAMISEMI inasimamia utekelezaji wa shughuli za utawala bora kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 146(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inayohusu Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi ili kuboresha utoaji wa huduma za kijamii na maendeleo. Mamlaka za Serikali za Mitaa ni vyombo vya wananchi vyenye Mamlaka ya kushiriki na kuwashirikisha wananchi katika mipango na utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika maeneo yao. Dhana ya ugatuaji wa Madaraka kwa Umma inatekelezwa kupitia misingi mikuu minne ambayo ni ugatuaji wa madaraka ya Kisiasa, Ugatuaji wa Rasilimali Watu, ugatuaji wa rasilimali fedha na mahusiano baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

**15.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kuimarisha utawala bora na demokrasia ikiwa ni pamoja na maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019, ujenzi wa majengo ya utawala katika Mikoa, Halmashauri, Tarafa, Kata, Mitaa na Vijiji ili kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Viongozi na Watendaji kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuimarisha misingi ya uwazi, usawa na uwajibikaji katika matumizi ya fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019**

**16.** ***Mheshimiwa Spika;*** Ibara ya 146 (1) na (2)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya Mwaka 1977 inaelekeza uimarishaji wa Demokrasia kwa Wananchi kuwawezesha Wananchi kushiriki katika kujiletea maendeleo. Ofisi ya Rais-TAMISEMI inatekeleza matakwa hayo ya Kikatiba kwa kuhakikisha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unafanyika kila baada ya

# HOTUBA OFISI YA RAIS TAMISEMI

miaka mitano kwa kuzingatia Sheria za Serikali za Mitaa Sura 287 na 288. Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 utakuwa wa sita tangu ulipofanyika kwa mara ya kwanza chini ya Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa Mwaka 1994. Viongozi watakaochaguliwa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 ni Wenyeviti na Wajumbe wa Halmashauri za Vijiji, Wenyeviti wa Mitaa, Wajumbe wa Kamati za Mitaa na Wenyeviti wa Vitongoji.

17. ***Mheshimiwa Spika***; Ofisi ya Rais-TAMISEMI imekamilisha zoezi la uhakiki wa maeneo ya utawala ambayo yatashiriki katika uchaguzi huo katika Halmashauri zote 184 ukiondoa Jiji la Dar-es-Salaam kwa kushirikisha Wizara za Kisekta, Mikoa na Halmashauri. Lengo la zoezi hilo lilikuwa ni kujiridhisha na usahihi wa maeneo hayo kwa idadi na majina kabla ya kutoa Tangazo la Serikali kupitia Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa. Usahihi wa takwimu hizo ni muhimu kwa ajili ya maandalizi ya bajeti ya uchaguzi na mahitaji mengine muhimu kwa ajili ya uchaguzi.

18. ***Mheshimiwa Spika;*** vilevile Ofisi ya Rais–TAMISEMI imekamilisha maandalizi ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 ambazo zimeandaliwa kwa kuwashirikisha Wadau mbalimbali wakiwemo Wakuu Mikoa 26, Makatibu Tawala wa Mikoa 26, Wakurugenzi wa Halmashauri 184, Maafisa Uchaguzi 184, Vyama vya Siasa vyenye usajili wa kudumu na Taasisi za Dini na Asasi Zisizo za Kiserikali. Kanuni hizo zitatumika kusimamia uchaguzi huo ambao utafanyika Novemba, 2019. Ofisi ya Rais-TAMISEMI inatoa wito kwa wadau mbalimbali na wananchi kujiandikisha, kuchukua fomu za kugombea na kujitokeza kwa wingi wakati wa kupiga kura ili kutumia haki yao ya kidemokrasia ya kuchagua au kuchaguliwa katika uchaguzi huo muda utakapofika.

**Kuzijengea Uwezo Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

19. ***Mheshimiwa Spika;*** jukumu la msingi la Ofisi ya Rais-TAMISEMI ni kuzijengea uwezo Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Mafunzo yametolewa kwa Wakuu wa Wilaya 27 walioteuliwa Oktoba, 2018 katika nyanja za mifumo, taratibu za mawasiliano Serikalini na mahusiano baina ya Taasisi za Serikali. Mafunzo hayo yameimarisha utendaji kazi wa Wakuu wa Wilaya katika usimamizi wa miradi ya maendeleo, utawala bora na utatuzi wa kero za Wananchi. Vilevile, Mwezi Desemba 2018, Wakuu wa Mikoa **26** na Makatibu Tawala wa Mikoa 26, Wakurugenzi wapya wa Halmashauri **39** walioteuliwa walifanyiwa mafunzo juu ya utawala bora kupitia Taasisi ya Uongozi kuhusu utekelezaji wa majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Serikali. Vilevile, Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mipango na Uratibu **26** wa Mikoa na Maafisa Mipango **185** wa Halmashauri walipatiwa mafunzo kuhusu mipango na Bajeti. Mafunzo hayo yamesaidia kuboresha utendaji ndani ya Serikali na kutatua kero za wananchi ili kuboresha utoaji wa huduma.

20. ***Mheshimiwa Spika;*** mafunzo mengine yametolewa kwa Wataalam **2,602** wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wakiwemo Maafisa Utumishi, Maafisa Mipango, Maafisa Elimu, Waganga Wakuu, Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Lishe, Wakaguzi wa Ndani na Maafisa Ugavi. Mafunzo yametolewa pia kwa Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa **1,614**. Mafunzo hayo yalihusu uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma na Sheria mbalimbali, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Utumishi wa Umma, misingi ya utawala bora, utoaji huduma, usimamizi na uendeshaji, tathmini ya utekelezaji wa mipango na bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 na maandalizi ya mipango na bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.

**Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA**

21. **Mheshimiwa Spika;** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kuboresha mifumo ya TEHAMA iliyopo na kubuni mifumo mipya ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Serikali. Mifumo iliyobuniwa ni pamoja na Mfumo wa Usajili wa Maeneo ya Utawala kwa ajili ya utambuzi wa maeneo ya utawala ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za utoaji wa huduma kwa wananchi, Mfumo wa Kusajili Wadau wa Maendeleo na Vibali vya Tafiti ambao unatumika kuratibu Wadau wa Maendeleo ili kuwatambua na kujua kazi wanazotekeleza.

22. **Mheshimiwa Spika;** mifumo mingine iliyosanifiwa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI ni pamoja na Mfumo wa Daftari la Wakazi *(Electronic Population Register System)* ambao umeanza kutumika kwa majaribio kusajili taarifa za wakazi katika Mikoa ya Songwe na Pwani na Mfumo wa Kuchagua Kidato cha Kwanza na Tano ambao unafanya kazi. Aidha, Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inakamilisha maandalizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Uhamisho wa Watumishi. Mfumo huo utaimarisha uwazi, uwajibikaji na kuondoa usumbufu kwa mtumishi kulazimika kusafiri kwa ajili ya kushughulikia uhamisho.

23. **Mheshimiwa Spika;** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imesanifu mfumo wa kielektroniki wa ufuatiliaji na tathmini ambao umejumuisha viashiria kutoka kwenye sekta zote ambazo utekelezaji wake unafanyika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mfumo huo utaiwezesha Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Wizara za kisekta kupata taarifa kuhusu utekelezaji wa masuala ya kisera na kiutendaji kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mfumo uko katika hatua za mwisho za maandalizi ili uanze kutumika.

24. **Mheshimiwa Spika;** mfumo wa kusimamia huduma za afya wa GoTHOMIS unatumika katika vituo vya kutolea huduma za afya **381** ambavyo vinajumuisha Hospitali za Rufaa za Mikoa **23,** Hospitali za Halmashauri **89,** Vituo vya Afya **178** na Zahanati **91.** Lengo ni kuwa na taarifa sahihi za afya, kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kuboresha utoaji wa huduma za afya.

25. **Mheshimiwa Spika;** mifumo imeunganishwa ili iwasiliane na kubadilishana taarifa kupitia *Muungano Gateway* ukiwemo Mfumo Funganishi wa Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha (Epicor), Mfumo wa Mipango na Utoaji wa Taarifa (PlanRep), Mfumo wa kukusanyia Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGRCIS), Mfumo wa Kihasibu wa Mapato na Matumizi na Utoaji Taarifa na Mfumo wa GoT-HOMIS unaotumika katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato yanayotokana na uchangiaji wa huduma za afya.

26. **Mheshimiwa Spika;** mifumo ya kielektroniki inayotumika katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa imechangia kuboresha hali ya upatikanaji wa taarifa kwa wakati, kuongeza ukusanyaji wa mapato, kuimarika kwa uwazi na uwajibikaji katika utendaji kazi ndani ya Serikali.

**Ujenzi wa Majengo ya Utawala na Nyumba za Viongozi Katika Mikoa na Halmashauri**

27. ***Mheshimiwa Spika;*** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Tawala za Mikoa zimetumia jumla ya **Shilingi bilioni 31.64** kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa Ofisi na nyumba za Viongozi katika Mkoa, Wilaya na Tarafa. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi bilioni 20.6** zimetumika kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Tarafa na **Shilingi bilioni 11.04** zimetumika kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa nyumba za Viongozi kwenye Mikoa, Wilaya na Tarafa.

28. ***Mheshimiwa Spika;*** ujenzi na ukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa umefanyika katika Mikoa ya Katavi, Simiyu, Njombe, Geita, Pwani, Arusha, Ruvuma, Dodoma na Singida kwa gharama ya **Shilingi bilioni 7.2.** Aidha, ujenzi na ukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya umefanyika katika Wilaya **29** ambazo ni Busega, Wanging'ombe, Nyang'hwale, Mbogwe, Dodoma Mjini, Buhigwe, Hai, Ruangwa, Malinyi, Gairo, Nyamagana, Tunduru, Mtwara, Mbinga, Pangani, Kilindi, Korogwe, Muleba, Biharamulo, Kaliua, Kigoma, Ubungo, Nyasa, Kalambo, Muheza, Igunga, Mkalama, Lushoto na Kinondoni ambazo zimegharimu jumla ya **Shilingi bilioni 10.1.** Aidha, Ofisi **60** za Maafisa Tarafa zimejengwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 3.3.**

29. ***Mheshimiwa Spika;*** vilevile zimejengwa nyumba za Viongozi 72 katika Mikoa na Wilaya kwa ajili ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Wilaya, Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Wilaya na Maafisa Tarafa. Hadi Februari 2019, ujenzi na ukarabati wa nyumba hizo umegharimu jumla ya **Shilingi bilioni 11.04.**

30. ***Mheshimiwa Spika;*** Mkoa wa Njombe umepokea jumla ya **Shilingi milioni 401.01** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa, Ofisi na nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe. Nyumba ya Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala wa Mkoa zipo katika hatua ya umaliziaji. Aidha, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Wanging'ombe imekamilika na inatumika na nyumba ya Mkuu wa Wilaya ipo katika hatua ya umaliziaji. Mkoa wa Geita umepokea **Shilingi bilioni 2.5** kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Mkandarasi amepatikana na kazi ya ujenzi wa Ofisi hizo itaanza Aprili, 2019.

31. ***Mheshimiwa Spika;*** Mkoa wa Katavi umepokea jumla ya **Shilingi milioni 675.00** ambazo zimetumika kuanza ujenzi wa nyumba ya Katibu Tawala wa Mkoa, nyumba ya Mkuu wa Wilaya, nyumba ya Katibu Tawala wa Wilaya na nyumba ya Afisa Tawala wa Wilaya ya Mlele. Ujenzi uko katika hatua ya msingi. Mkoa wa Songwe umepokea **Shilingi bilioni 1.3** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala wa Mkoa, ukamilishaji wa nyumba ya Mkuu wa Wilaya, Katibu Tawala wa Wilaya na nyumba za Maafisa Waandamizi katika Wilaya ya Momba, ujenzi wa nyumba za Maafisa Waandamizi wa Wilaya upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji. Nyumba ya Katibu Tawala wa Wilaya na Maafisa Waandamizi zinajengwa kwa kutumia utaratibu wa *Force Account.* Aidha, ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe uko katika hatua ya kutangaza Zabuni.

32. ***Mheshimiwa Spika;*** Mkoa wa Simiyu unaendelea na ukamilishaji wa nyumba ya Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala wa Mkoa, ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Busega na nyumba za Makatibu Tawala wa Wilaya za Busega na Itilima kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.48** ambapo ujenzi umekamilika katika nyumba ya Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala wa Mkoa. Aidha, ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Busega na nyumba za Makatibu Tawala wa Wilaya za Busega na Itilima upo katika hatua ya kutangaza zabuni.

33. ***Mheshimiwa Spika;*** Halmashauri **78** zinaendelea na ujenzi wa majengo ya utawala zikiwemo Halmashauri **55** zilizotengewa bajeti ya **Shilingi bilioni 61.7** kuanzia Mwaka wa Fedha 2015/16 hadi 2017/18. Ujenzi wa majengo hayo upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Halmashauri 23 zilizoanzishwa Mwaka 2014 ziliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 52.9** katika Mwaka wa Fedha 2018/19 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya utawala ya Halmashauri. Hadi Februari, 2019 Halmashauri **23** zimepokea jumla ya **Shilingi bilioni 23** sawa na **asilimia 43.4** kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa majengo ya utawala ya Halmashauri.

**Huduma za Afya**

34. **Mheshimiwa Spika;** huduma bora za afya ni msingi wa kuondoa umaskini na kuharakisha maendeleo ya wananchi. Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 inayoelekeza kuwa na Hospitali kila Wilaya, Kituo cha Afya kila Kata na Zahanati kila Kijiji. Lengo la mpango huo wa maendeleo ni kuongeza upatikanaji wa huduma za Afya za msingi katika ngazi zote ili kuboresha maisha ya wananchi na kuchochea ukuaji wa uchumi.

# HOTUBA OFISI YA RAIS TAMISEMI

**Ujenzi wa Hospitali za Halmashauri**

**35. Mheshimiwa Spika;** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, ziliidhinishwa jumla ya **Shilingi bilioni 100.5** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali 67 za Halmashauri. Hadi Februari 2019, fedha zote zilikuwa zimepokelewa kwenye Halmashauri na ujenzi unaendelea kwa kutumia utaratibu wa "*Force Account"* kwa kuzingatia Kanuni ya 167 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 pamoja na marekebisho yake ya Mwaka 2016. Matumizi ya utaratibu wa "Force Account" yamezingatia uzoefu uliopatikana katika ujenzi wa vituo vya Afya kwenye Halmashauri ambao umeleta manufaa makubwa katika kupunguza gharama endapo Makandarasi wangetumika kutekeleza miradi hiyo. Aidha, utaratibu huo umeongeza hamasa kwa wananchi kushiriki kwa hali na mali katika kujenga miundombinu ya huduma za kijamii katika maeneo yao na hivyo kujenga dhana ya kujitegemea, kumiliki na kuwa na sauti katika maendeleo ya huduma za afya.

**36.** ***Mheshimiwa Spika;*** ujenzi wa Hospitali za Halmashauri unahusisha majengo saba (7) ambayo yanajengwa kwa kutumia **Shilingi bilioni 1.5** zilizotolewa kwa kila Halmashauri. Majengo hayo ni ya utawala, wagonjwa wa nje, stoo ya dawa, maabara, jengo la mionzi (X-Ray), jengo la kufulia nguo na jengo la wazazi. Aidha, ujenzi huo utakamilika ifikapo Juni, 2019.

**Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya Afya na Zahanati**

**37. Mheshimiwa Spika;** ujenzi na ukarabati wa Vituo vya afya nchini ni mkakati wa Serikali kuboresha huduma za afya ya msingi (Primary Health Care) ili kupunguza msongamano katika Hospitali za Rufaa za Mikoa na Hospitali za Taifa za Kanda. Hivyo, mpango huo unaboresha mfumo wa rufaa kwa wagonjwa kuanzia ngazi ya Zahanati, Vituo vya afya, Hospitali za Halmashauri, Hospitali za Rufaa za Mikoa na Hospitali za Rufaa za Kanda.

**38.** ***Mheshimiwa Spika;*** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea na ukamilishaji wa ujenzi, ukarabati na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya. Mpango wa uboreshaji wa vituo hivyo, unazingatia upatikanaji wa huduma za upasuaji kwa mama wajawazito ili kupunguza vifo vya mama na mtoto. Ujenzi na ukarabati huo unahusisha vituo vya kutolea huduma za afya **352**, zikiwemo Hospitali **9**, Vituo vya Afya **304** na Zahanati **39.** Vilevile, ujenzi na ukarabati wa nyumba za watumishi **301** unaendelea. Kipaumbele kiliwekwa katika kukamilisha maboma yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi.

**39.** ***Mheshimiwa Spika;*** utekelezaji wa mpango huo wa ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya na zahanati umegharimu jumla ya **Shilingi bilioni 184.67.** Vigezo vilivyotumika kubainisha vituo vitakavyokarabatiwa vilijumuisha umbali kutoka Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya, gharama za vifaa vya ujenzi katika eneo husika, hali au uwepo wa miundombinu na makubaliano na Wafadhili waliotoa fedha za ukarabati. Ujenzi na ukarabati huo umejumuisha ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto, nyumba moja ya mtumishi, jengo la wagonjwa wa nje na chumba cha kuhifadhia maiti. Serikali imeweza kuokoa fedha nyingi kwa kutumia utaratibu wa "*Force Account"* ambapo gharama zimepungua kutoka **Shilingi bilioni 2.5** hadi **Shilingi milioni 400 au 500** kwa kituo. Sambamba na ujenzi na ukarabati, Serikali imetoa jumla ya **Shilingi bilioni 41.6** kwa ajili ununuzi wa vifaa na vifaa tiba. Vilevile, Wataalam wa Usingizi zaidi ya **200** wamepatiwa mafunzo kwa ajili ya kuimarisha huduma za upasuaji kwenye vituo vipya vya afya vilivyojengwa na kukarabatiwa.

**40.** ***Mheshimiwa Spika;*** ukarabati wa Vituo vya afya unafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Awamu ya Kwanza ilifanyika Oktoba 2017 hadi Aprili, 2018 ambayo ilihusisha ukarabati wa vituo vya afya **44** vilivyogharimu jumla ya **Shilingi bilioni 22.0.** Vituo hivyo vimekamilika na vimeanza kutoa huduma. Awamu ya Pili ilifanyika Januari hadi Juni, 2018 na kuhusisha vituo vya afya **139** vilivyogharimu jumla ya **Shilingi bilioni 59** ambavyo vimekamilika kwa zaidi ya **asilimia 90.** Awamu ya Tatu imefanyika kuanzia Mei hadi Novemba, 2018 na kuhusisha vituo **27** vilivyokarabatiwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 12.5** na Awamu ya Nne na ya Tano imehusisha ukarabati wa vituo **114** vilivyopokea jumla ya **Shilingi bilioni 42.45.** Fedha hizo zimepelekwa moja kwa moja kwenye vituo kupitia Akaunti za vituo kwa kutumia Mfumo wa kihasibu wa Mapato na Matumizi kwenye Vituo vya Kutolea Huduma (*FFARS)* ambao umeimarisha uwazi, uwabijikaji, ushirikishwaji na ukusanyaji wa mapato.

**Watumishi wa Kada ya Afya**

**41.** ***Mheshimiwa Spika;*** ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya unafanyika sambamba na ajira za watumishi ili kuviwezesha vituo hivyo kuanza kutoa huduma. Kati ya Mwaka wa Fedha 2016/17 hadi 2018/19, Serikali iliajiri watumishi wa kada za afya **8,447** waliopangwa kufanya kazi katika vituo vilivyoko kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Idadi hiyo inajumuisha watumishi **2,267** walioajiriwa Mwaka wa Fedha 2016/17 na watumishi **6,180** walioajiriwa katika Mwaka wa Fedha 2018/19. Vilevile, Taasisi ya Benjamini Mkapa imeajiri watumishi **300** na kuwapanga katika maeneo ya kipaumbele kwenye vituo vilivyokarabatiwa ili vianze kutoa huduma. Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaendelea kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kuhakikisha watumishi wengi zaidi wa afya wanaajiriwa kukidhi viwango vya utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

**Upatikanaji wa Dawa, Vifaa na Vifaa Tiba**

**42.** ***Mheshimiwa Spika;*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeratibu uanzishwaji wa Mfumo wa Mshitiri katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara ikiwa ni utekelezaji wa Awamu ya Nne ya Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015. Mfumo wa Mshitiri unaviwezesha vituo vya kutolea huduma za afya kupata mahitaji ya vifaa, vifaa tiba, dawa na vitendanishi kutoka kwa Wauzaji Binafsi walioteuliwa pindi mahitaji yanapokosekana katika Bohari Kuu ya Dawa (*MSD).* Vituo vya kutolea huduma za afya nchini vitaendelea kuagiza mahitaji ya bidhaa za afya kutoka MSD kama ulivyo utaratibu na pale vituo vitakapokosa mahitaji hayo MSD ndipo vinaruhusiwa kuagiza kutoka kwa Mshitiri Mteule wa Mkoa kwa kutumia mapato ya ndani au fedha za makusanyo za uchangiaji za papo kwa papo. Mshitiri atavipatia vituo vya afya bidhaa za afya kulingana na uhitaji kwa bei ambazo zimekubalika kwa mujibu wa mkataba.

**43.** ***Mheshimiwa Spika;*** ili kuimarisha usimamizi na matumizi sahihi ya mfumo wa Washitiri, mafunzo yametolewa kwa Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri na Wataalam ngazi ya Wizara kuhusu matumizi ya mfumo huo ambao umeanza kufanya kazi. Vilevile, watoa huduma za afya **103** ngazi ya Kitaifa, **431** kutoka ngazi ya Mkoa, **540** kwenye Hospitali za Halmashauri na Wafanyabiashara **142** wanaojihusisha na biashara ya bidhaa za dawa za walipatiwa mafunzo.

**Huduma za Lishe**

**44.** ***Mheshimiwa Spika;*** nchi yetu bado inakabiliwa na matatizo ya lishe duni ambapo viwango vya udumavu katika Mikoa mingi bado siyo ya kuridhisha. Kwa mujibu wa utafiti wa Hali ya Afya Nchini (TDHS) wa mwaka 2015/16 zinaonesha hali ya udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano ni **asilimia 34.** Serikali kwa kushirikiana na jamii na wadau mbalimbali wa maendeleo inatekeleza Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe wa Miaka Mitano ambao umejielekeza katika kutekeleza afua mbalimbali za lishe likiwemo tatizo la utapiamlo. Serikali imeweka kipaumbele na kuongeza rasilimali fedha za kutekeleza afua za lishe kutoka **Shilingi bilioni 11.0** zilizoidhinishwa Mwaka wa Fedha 2017/18 hadi **Shilingi bilioni 15** katika Mwaka wa Fedha 2018/19 sawa na ongezeko la **asilimia 3.6.** Vilevile, katika kipindi hicho Wadau wa Maendeleo walitoa kiasi cha **Shilingi bilioni 4.96** zilizotumika kutekeleza afua za lishe katika baadhi ya Mikoa na Halmashauri nchini. Ongezeko la rasilimali fedha limesaidia kuongeza kiwango cha utoaji wa huduma ya matone ya vitamini A kutoka **asilimia 93** Mwaka 2017 hadi **97** Mwaka 2018 na utoaji wa dawa za minyoo umeongezeka kutoka **asilimia 92** Mwaka 2017 hadi **asilimia 96** Mwaka 2018. Vilevile, **asilimia 79** ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano walipimwa hali zao za lishe, **asilimia 75** ya akina mama wajawazito wamepatiwa vidonge vya kuongeza wekundu wa damu kwa lengo la kupunguza vifo vya akina mama wakati wa kujifungua vinavyosababishwa na upungufu wa damu.

**45.** ***Mheshimiwa Spika;*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imesaini mkataba wa utendaji kazi na Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri ili kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika utekelezaji wa afua za lishe nchini. Mikataba hiyo inafanyiwa tathmini kila baada ya miezi sita ili kupima kufikiwa kwa malengo ya utokomezaji wa utapiamlo. Vilevile, Serikali imeimarisha eneo la rasilimali watu hasa wataalam wa lishe ambapo jumla ya wataalam wa lishe **113** wameajiriwa ili kuboresha mkakati wa utekelezaji wa afua za lishe kama utoaji wa matone ya Vitamin A, utoaji wa madini ya chuma, vyakula tiba, na elimu ya lishe kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Huduma za Ustawi wa Jamii**

**46.** ***Mheshimiwa Spika;*** utekelezaji wa shughuli za ustawi wa jamii kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa unafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Mtoto Na.21 ya Mwaka 2009, Sheria ya Ndoa Na. 5 ya Mwaka 1971, Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na.9 ya Mwaka 2010, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Binadamu 2008, Sheria ya makosa ya kujamiana Na. 4 ya mwaka 1998, Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003, Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya 2004, na Mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI Mwaka 2017 kuhusu ustawi wa jamii.

**47.** ***Mheshimiwa Spika;*** maeneo ya utekelezaji wa huduma za Ustawi wa Jamii ni pamoja na familia na watoto; malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto; marekebisho ya Tabia na Haki za Mtoto kisheria; huduma kwa Wazee na Watu Wenye Ulemavu na Uimarishaji wa Mifumo ya kielektroniki ya ustawi wa jamii. Serikali imeweka kipaumbele na kuongeza rasilimali fedha za kutekeleza utoaji huduma za Ustawi wa Jamii katika maeneo tajwa kutoka **Shilingi bilioni 9** zilizoidhinishwa Mwaka wa Fedha 2017/18 hadi **Shilingi bilioni 11.4** katika Mwaka wa Fedha 2018/19 sawa na ongezeko la **asilimia 6.6.**

**Ulinzi na Usalama wa Mtoto**

**48.** ***Mhesimiwa Spika*****;** katika hatua ya kuendelea kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Mtoto kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kamati za Ulinzi na Usalama wa Mtoto na Mwanamke zimeundwa katika Mikoa **26,** Halmashauri **184**, Kata **2,490** kati ya **4,420,** Vijiji **7,900** kati ya **16,626** ili kutekeleza kampeni za kutokomeza mimba na ndoa za utotoni. Aidha, Wataalam wa Ustawi wa Jamii 505 kati ya 738 wamepatiwa mafunzo kuhusu namna ya kutoa huduma ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto katika maeneo yao

**49. Mheshimiwa Spika;** juhudi za kutokomeza ukatili dhidi ya Watoto na Wanawake umeamsha mwitikio chanya kwa wananchi hivyo kuongeza kesi za utakili wa Watoto na Wanawake zinazotolewa taarifa katika Ofisi za Ustawi wa Jamii, Dawati la Polisi la Jinsia na Ofisi za Watendaji wa Mitaa/Vijiji. Aidha, mashauri ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto yaliyoripotiwa kuhusu akina mama ni **4,187** na watoto ni **6,782** ambayo yamefanyiwa kazi. Kati ya mashauri hayo, jumla ya kesi **1,973** zilifikishwa mahakamani na kesi **711** zilitolewa hukumu.

**Huduma kwa Watoto Walio Katika Mazingira**

# HOTUBA OFISI YA RAIS TAMISEMI

**Hatarishi**

**50.** ***Mheshimiwa Spika***; hadi kufikia Februari, 2019, tumefanikiwa kuongeza idadi ya utambuzi wa watoto walio katika mazingara hatarishi, ambapo watoto **389,012** wametambuliwa ukilinganisha na watoto **201,382** waliotambuliwa katika kipindi cha Machi, 2018 hivyo kufikisha idadi ya Watoto **1,495,049** wanaoishi katika mazingira hatarishi walitambuliwa, wanawake wakiwa ni **724,105** na wanaume **770,944** na kupatiwa huduma mbalimbali ikiwemo kuunganishwa na familia zao, vifaa vya shule na ada ya kujiunga vyuo vya Mafunzo ya Ufundi ikiwemo chuo cha VETA .

**Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu**

**51.** ***Mheshimiwa Spika;*** Watu Wenye Ulemavu waliotambuliwa ni **405,426** ambapo wanawake **191,116** wanaume **214,220** katika Halmashauri **184**. Kamati za Watu Wenye Ulemavu zimeundwa katika Vijiji **11,954** kati ya Vijiji **12,545** sawa na **asilimia 95** na Mitaa **4,011** kati ya Mitaa **4,420** sawa na **asilimia 90.7**. Jumla ya Watu Wenye Ulemavu **217,932** kati ya **405,426** ya waliotambuliwa walipatiwa huduma za Afya kwa gharama ya **Shilingi milioni 102.1** na kati ya hao **3,226** walipatiwa kadi za Bima ya Afya ya Jamii (CHF).

**Huduma za Wazee**

**52.** ***Mheshimiwa Spika***; hadi Februari, 2019 jumla ya Wazee **750,622** wametambuliwa ikilinganishwa na Wazee **300,000** waliotambuliwa hadi Februari, 2018. Kati ya hao, wazee **247,705** wamepatiwa vitambulisho vya matibabu bure, sawa na asilimia **33** ya wazee wote waliotambuliwa. Aidha, kati ya hao, wazee **502,917** wamepatiwa kadi za matibabu za Afya ya Jamii (CHF) sawa na asilimia **67.**

**Mpango wa Uimarishaji wa Mifumo ya Taarifa ya Ustawi wa Jamii**

**53.** **Mheshimiwa Spika;** hadi Machi, 2019 tumefanikiwa kusambaza na kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji na utunzaji wa taarifa za watoto walio katika mazingira hatarishi na wale wanaoishi na kufanya kazi mtaani katika Halmashauri **147** kati ya **184**. Mfumo umesaidia kuwa na takwimu sahihi za matukio ya ukatili dhidi ya watoto na kuongeza uwazi katika usimamizi wa shughuli za watoto. Kupitia Mradi wa USAID Kizazi Kipya zimenunuliwa na kusambazwa Kompyuta, *Printer,* na Modem **101** zenye thamani ya **Shilingi milioni 257.6** kwa Mikoa **23** na Halmashauri **78** Awamu ya Kwanza kwa ajili ya matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Taarifa za Ustawi wa Jamii.

**Mfuko wa Pamoja wa Afya**

**54.** ***Mheshimiwa Spika;*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeboresha utaratibu wa usimamizi wa fedha za Mfuko wa Pamoja wa Afya kwa kuzipeleka moja kwa moja kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ambapo wananchi wanashirikishwa kupitia kamati za usimamizi wa vituo vya kutolea huduma za afya. Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imeanzisha mfumo wa kielektroniki unaojulikana kama *FFARS* ambao unatumika kusimamia fedha hizo na kurahisisha upatikanaji wa taarifa za matumizi ya fedha hizo. Katika Mwaka wa Fedha 2017/18, jumla ya vituo 5,136 vya kutolea huduma vilipokea kiasi cha **Shilingi bilioni 69.0** zilizotumwa moja kwa moja kupitia kwenye mfumo huo. Vilevile, katika Mwaka wa Fedha 2018/19, jumla ya **Shilingi bilioni 19** kati ya bajeti ya **Shilingi bilioni 104.7** zimepelekwa kwenye vituo **5,437.** Ili kuimarisha usimamizi wa fedha hizo, Serikali imeajiri Wahasibu Wasaidizi **535** ambao wanasimamia matumizi ya mfumo katika ngazi ya vituo na kutoa taarifa kila Robo Mwaka.

**Mpango wa Malipo Kulingana na Ufanisi *(Result Based Financing)***

**55.** ***Mheshimiwa Spika;*** Mpango wa Malipo Kulingana na Ufanisi (Result Based Financing-RBF) ulianza kutekelezwa Mwaka 2015 katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu Mkoani Shinyanga kwa majaribio na baadaye Mwaka 2016, Programu hiyo ilianza kutekelezwa katika Halmashauri zote za Mkoa wa Shinyanga. Kwa sasa Mpango wa Malipo Kulingana na Ufanisi unatekelezwa katika Mikoa nane (8) ya Shinyanga, Mwanza, Pwani, Simiyu, Tabora, Kagera, Geita na Kigoma yenye jumla ya Halmashauri **59** na vituo **1,655** vya kutolea huduma za afya. Mikoa hiyo ilichaguliwa kutokana na uwepo wa vifo vya Mama Wajawazito vilivyosababishwa na kukosekana na huduma za msingi pamoja na idadi ndogo ya wataalam wa afya kwenye maeneo hayo. Mpango huo unahusisha ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya na kujenga uwezo wa Timu za Usimamizi wa huduma za afya ngazi ya Mkoa na Wilaya. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2018 hadi Februari, 2019 jumla ya **Shilingi bilioni 26.10** zimetumika kutekeleza mpango huo katika shughuli za usimamizi ngazi ya Mkoa na uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma za afya kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**56.** ***Mheshimiwa Spika;*** utekelezaji wa mpango huo umesaidia kuboresha huduma za afya ambapo Mikoa hiyo sasa inafanya vizuri katika viwango vya utoaji wa huduma za afya kutoka mwaka 2015 hadi 2018. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na kuimarika kwa ushirikishwaji wa wananchi kupitia kuongezeka kuundwa kwa Bodi za Afya za Halmashauri kutoka **asilimia 50** hadi **asilimia 86.2**. Aidha, upatikanaji wa dawa umeongezeka kutoka **asilimia 41.06** hadi **asilimia 86.2.** Vituo vya afya vyenye nyota **0** vimepungua kutoka **asilimia 42.5** hadi **asilimia 3.1** na vituo vyenye nyota zaidi ya **3** vimeongezeka kutoka **asilimia 0.8** hadi **asilimia 23.2.** Aidha, kiwango cha ubora wa takwimu kimeongezeka kutoka asilimia 70 hadi asilimia 89.5 kwenye Mikoa nane (8) ya utekelezaji wa mpango.

**Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)**

**57.** ***Mheshimiwa Spika;*** Ofisi ya Rais- TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya pamoja na Wadau wa Maendeleo imefanya maboresho ya mfuko huo ili wananchi waweze kupata huduma za matibabu ya rufaa hadi kwenye hospitali za rufaa za Mikoa. Utengenezaji wa kanzidata kwa ajili ya utunzaji wa kumbukumbu za wanachama nchi nzima umekamilika. Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa umeanza rasmi kutumika Aprili, 2018. Hadi Machi, 2019, Mikoa iliyoanza kusajili wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa imefikia **13** na zoezi hilo linaendelea.

**Mfuko wa Dunia wa UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria**

**58.** ***Mheshimiwa Spika;*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaendelea na utekelezaji wa shughuli za UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu katika kipindi cha Mwaka 2018-2020 baada ya kufikia ukomo katika kipindi cha Mwaka 2015-2017. Kazi kubwa zinazofanyika zinahusisha shughuli za uratibu, usimamizi shirikishi, mikutano na mafunzo kupitia timu za uendeshaji huduma za afya kwenye Mikoa na Halmashauri (RHMTs na CHMTs), ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za UKIMWI na kuimarisha mifumo ya kutolea taarifa za fedha katika vituo vya kutolea huduma za afya. Katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Ofisi ya Rais-TAMISEMI iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 2.88** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za UKIMWI na Kifua Kikuu. Kati ya Fedha hizo **Shilingi bilioni 2.76** sawa na **asilimia 96** zilikuwa zimepokelewa hadi Februari, 2019 kwa ajili ya utekelezaji wa programu kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari**

**59.** ***Mheshimiwa Spika;*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuboresha, kuimarisha na kuinua kiwango cha Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari kwa lengo la kuhakikisha elimu katika ngazi zote inakuwa na ubora unaostahili. Lengo ni kuwa na jamii iliyoelimika yenye maarifa, uzalendo na ujuzi wa kutosha kumudu ustawi wa maisha yao, na kuhimili ushindani wa ndani na kimataifa.

**Elimu ya Awali na Msingi**

**60.** ***Mheshimiwa Spika***; uandikishaji wa wanafunzi wapya katika mfumo rasmi wa elimu nchini unaonesha kuwa hadi Machi, 2019 wanafunzi wa elimu ya awali walioandikishwa ni **1,278,816** sawa na asilimia **92.48** ya lengo la kuandikisha wanafunzi **1,382,761.** Aidha, kati ya hao walioandikishwa, wanafunzi **1,372** ni wenye mahitaji maalum. Uandikishaji huo umepungua kwa **asilimia 0.4** ikilinganishwa na wanafunzi **1,283,790** walioandikishwa mwaka **2018**. Vilevile, wanafunzi wapya walioandikishwa kuanza Darasa la Kwanza ni **1,670,919** hadi kufikia Machi, 2019 ikilinganishwa na wanafunzi **1,751,221** walioandikishwa hadi Mwaka **2018** sawa na upungufu wa asilimia **4.5**. Kati ya hao, wanafunzi wenye mahitaji maalum walioandikishwa ni **3,028**. Upungufu wa uandikishaji unatokana na mafanikio ya Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo ambao katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2016 hadi 2018 umewezesha wanafunzi wenye umri wa kwenda shule kuandikishwa kila mwaka kutokana na kuondolewa kwa vikwazo vya ada na michango mbalimbali.

**61.** ***Mheshimiwa Spika;*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kushirikiana na Wananchi na Wadau wa Maendeleo katika kuboresha miundombinu ya shule za awali na msingi. Hadi Februari, 2019 ujenzi wa vyumba vya madarasa **2,840** kwa shule za msingi umefanyika na kuongeza idadi ya vyumba vya madarasa kutoka **119,647** vilivyokuwepo Machi 2018 hadi madarasa **122,487** kufikia Februari, 2019 sawa na ongezeko la **asilimia 2.3.** Aidha, vyumba vya madarasa **2,637** viko katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Vilevile, jumla ya matundu ya vyoo **7,067** (vyoo vya wanafunzi matundu **6,445** na vyoo vya Walimu matundu **622**) yamejengwa katika shule za msingi na kuongeza matundu ya vyoo kutoka **190,674** yaliyokuwepo Machi, 2018 hadi kufikia matundu ya vyoo **197,741** mwezi Februari, 2019 hili ni ongezeko la **asilimia 3.5**. Aidha, matundu ya vyoo **3,004** yanaendelea kujengwa na yanatarajiwa kukamilika kabla ya Juni, 2019.

**62.** ***Mheshimiwa Spika;*** kazi nyingine za uboreshaji miundombinu ya elimu zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa nyumba za walimu **720** na kuongeza idadi ya nyumba hizo kutoka **44,320** mwaka **2018** hadi nyumba **45,040** Februari, 2019. Aidha, madawati ya wanafunzi watatu watatu yameongezeka kutoka madawati **2,858,982** yaliyokuwepo Machi, 2018 hadi madawati **2,994,266** Februari, 2019 sawa na ongezeko la madawati **135,284**. Aidha, kupitia Programu ya *Equip-T,* Serikali imetoa jumla ya **Shilingi bilioni 18.5** kwa ajili ya ujenzi wa vituo shikizi **251** ambapo jumla ya vyumba vya madarasa **502**, ofisi za walimu **251**, matundu ya vyoo **1,255**, maktaba **34**, matanki ya maji **1,255** pamoja na ukamilishaji wa maboma **263** ya vyumba vya madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi yametekelezwa katika Mikoa **9** yenye Halmashauri **63**.

**Ajira za Walimu wa Shule za Msingi**

**63.** ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali imeajiri walimu **4,811** katika Mwaka wa Fedha 2018/19 ambao walipangwa kufundisha katika shule za msingi nchini. Walimu hao wamepangwa katika Halmashauri zenye upungufu mkubwa isipokuwa shule zilizoko katika Halmashauri za Majiji, Manispaa na Miji ambazo zina walimu wengi ikilinganishwa na maeneo ya vijijini. Ajira hizo zimeongeza idadi ya walimu wa shule za msingi waliopo kutoka **164,618** waliokuwepo Februari, 2018 hadi **179,429** waliopo Februari, 2019. Aidha, Serikali imetoa kibali cha ajira ya walimu **3,175** wa shule za msingi ambapo mchakato wa ajira unaendelea na mara baada ya zoezi hilo kukamilika watapangwa katika

maeneo yenye upungufu mkubwa wa walimu na hasa yale ya vijijini. Ajira hizo zitatoa kipaumbele kwa walimu wenye mahitaji maalum na kwa walimu waliosomea Elimu Maalum.

64. ***Mheshimiwa Spika;*** katika kuongeza ari ya utendaji kazi, Serikali inatoa posho ya madaraka kwa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi **16,159** na Maafisa Elimu Kata **3,895** kila mwezi. Aidha, Maafisa Elimu Kata wamepewa pikipiki **2,894** ili kuimarisha uratibu, usimamizi na ufuatiliaji wa elimu kwenye maeneo yao.

**Upimaji na Mtihani wa Taifa**

65. ***Mheshimiwa Spika*;** katika mwaka 2017, watahiniwa **1,192,655** walisajiliwa kufanya Mtihani wa Taifa wa Upimaji wa Darasa la Nne. Wanafunzi **1,158,499** walifanya Mtihani huo ambapo kati ya hao, wanafunzi **1,086,156** walifaulu sawa na **asilimia 93.57** ikilinganishwa na wanafunzi **1,362,642** waliosajiliwa kufanya Mtihani Mwaka 2018 ambapo kati yao wanafunzi **1,302,461** sawa na **asilimia 93.14** walifaulu mtihani huo. Aidha, jumla ya wanafunzi **957,904** walisajiliwa kufanya Mtihani wa Taifa wa Kuhitimu Darasa la Saba mwaka 2018 na wanafunzi **733,103** sawa na **asilimia 77.72** kati ya wanafunzi **944,218** waliofanya Mtihani huo walifaulu ikilinganishwa na wanafunzi **662,035** waliofaulu Mtihani huo kwa mwaka 2017 sawa na **asilimia 72.76.** Ufaulu wa mtihani umeongezeka kwa **asilimia 4.96** kutoka **asilimia 72.76** Mwaka 2017 hadi **asilimia 77.72** mwaka **2018.** Kuimarika kwa ufaulu huo kumetokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia, usimamizi mzuri wa viongozi wa elimu, ushiriki wa wazazi, wadau na mwamko wa walimu kufanya kazi kwa misingi ya weledi ikiwa ni pamoja na kukamilisha muhtasari ndani ya muda uliopangwa.

**Elimu ya Sekondari**

66. ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2019 jumla ya wanafunzi **710,436** walichaguliwa kujiunga Kidato cha Kwanza ikilinganishwa na wanafunzi **595,427** waliojiunga Kidato cha Kwanza mwaka 2018 sawa na ongezeko la wanafunzi **115,009** ambao ni **asilimia 16.2**. Hadi Februari, 2019 wanafunzi **575,187** sawa na **asilimia 80.96** walikuwa wameripoti katika shule walizopangiwa.

67. ***Mheshimiwa Spika;*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kuboresha miundombinu ya shule ili kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa wanapata fursa ya kuendelea na masomo ya sekondari. Hadi Februari, 2019 Serikali kupitia mpango wa Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R) imetoa jumla ya **Shilingi bilioni 52.22** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa **938**, matundu ya vyoo **2,141**, mabweni **210**, nyumba za walimu **47**, majengo ya utawala **13**, maabara za sayansi **22**, maktaba **39**, mabwalo ya chakula **76**, ukarabati na umaliziaji wa vyumba vya madarasa **219** na ujenzi wa visima **10** vya maji.

68. ***Mheshimiwa Spika***; Aidha, jumla ya vyumba **1,607** vya madarasa vimejengwa na kuongeza idadi kutoka vyumba vya madarasa **40,720** Machi, 2018 hadi **42,327** Februari, 2019 na ukamilishaji wa madarasa **1,223** unaendelea**.** Vilevile, jumla ya matundu ya vyoo **1,978** yamejengwa na kuongeza idadi ya matundu ya vyoo kufikia **56,466** ikilinganishwa na matundu **54,488** yaliyokuwepo Machi, 2018.

69. ***Mheshimiwa Spika***; kazi nyingine za uboreshaji miundombinu ya elimu zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa nyumba za walimu **159**, maabara za sayansi **123**, ununuzi wa viti **605** na meza **727** kwa ajili ya wanafunzi. Aidha, Serikali imetoa jumla ya **Shilingi bilioni 29.9** kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma **2,392** ya madarasa yatakayowezesha kuongeza idadi ya wanafunzi **133,747** wa Kidato cha Kwanza waliokosa nafasi.

**Ajira za Walimu wa Shule za Sekondari**

70. **Mheshimiwa Spika;** Serikali imeajiri walimu **2,189** katika Mwaka wa Fedha 2018/19 ambao walipangwa kufundisha katika shule za sekondari nchini. Kati ya walimu hao, walimu wenye mahitaji maalum ni **29,** walimu wa hisabati na sayansi **1,900,** walimu wa lugha (Literature in English) **100**, na mafundi sanifu wa maabara **160**. Walimu hao wamepangwa katika Halmashauri zenye upungufu mkubwa wa walimu. Ajira hizo zimeongeza idadi ya walimu wa shule za sekondari kutoka **82,023** waliokuwepo Februari, 2018 hadi **84,212** waliopo Februari, 2019. Aidha, Serikali imetoa kibali cha ajira ya walimu **1,374** wa shule za sekondari ambapo mchakato wa ajira unaendelea na mara baada ya zoezi hilo kukamilika watapangwa katika maeneo yenye upungufu mkubwa na kipaumbele kitatolewa kwa walimu wenye mahitaji maalum na waliosomea Elimu Maalum.

**Upimaji na Mitihani ya Taifa**

71. ***Mheshimiwa Spika;*** idadi ya wanafunzi waliofaulu mtihani wa Taifa wa Upimaji wa Kidato cha Pili imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2017, jumla ya wanafunzi **486,423** walifanya mtihani ambapo kati yao wanafunzi **433,453** sawa na asilimia **89.05** walifaulu ikilinganishwa na ufaulu wa **asilimia 89.68** wa wanafunzi waliofanya mtihani huo mwaka 2018 ambapo jumla ya wanafunzi **506,235** walifanya mtihani huo na waliofaulu walikuwa wanafunzi **452,273.**

72. ***Mheshimiwa Spika;*** idadi ya wanafunzi waliosajiliwa kufanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne mwaka 2017 walikuwa **385,767** ambapo waliofanya mtihani huo walikuwa wanafunzi **317,777** na wanafunzi **245,274** walifaulu sawa na **asilimia 77.18**. Aidha, mwaka 2018 walisajiliwa wanafunzi **368,037** ambapo, waliofanya mtihani huo walikuwa wanafunzi **360,510,** wanafunzi waliofaulu walikuwa **284,126** sawa na **asilimia 78.81**. Vilevile, ufaulu wa wanafunzi waliofanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita umeendelea kuimarika. Kati ya wanafunzi **62,725** waliofanya mtihani mwaka 2017, wanafunzi **61,533** walifaulu sawa na **asilimia 98.1** ikilinganishwa na wanafunzi **83,581** waliofaulu mtihani huo mwaka 2018 kati ya wanafunzi **86,105** waliofanya mtihani sawa na ufaulu wa **asilimia 97.07.** Kuimarika kwa ufaulu huo kumetokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia, kuimarika kwa usimamizi wa elimu, ushiriki wa wazazi na wadau mbalimbali na mwamko wa walimu kufanya kazi kwa misingi ya weledi ikiwa ni pamoja na kukamilisha muhtasari ndani ya muda uliopangwa.

**Utoaji wa Elimumsingi Bila Ada**

73. ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Ada ulioanza Desemba, 2015. Katika mwaka wa fedha 2018/19 hadi kufikia Februari, 2019, Serikali ilikuwa imetoa fedha kiasi cha **Shilingi bilioni 166.44** kutekeleza Mpango wa Elimumsingi Bila Ada. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi bilioni 77.20** zilipelekwa katika Shule za Msingi na **Shilingi bilioni 89.23** zimetumika kutekeleza mpango katika Shule za Sekondari. Maeneo yanayohusika na fedha za Elimumsingi Bila Ada ni ruzuku ya uendeshaji kwa kila mwanafunzi, fedha za chakula kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wa shule za msingi na wanafunzi wa bweni wa shule za sekondari kidato cha 1 hadi 6, fidia ya ada kwa wanafunzi wa kutwa na bweni kidato cha 1 hadi 4, na posho ya madaraka kwa Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari na Maafisa Elimu Kata. Mpango wa Elimumsingi Bila Ada umewezesha wanafunzi wapya wanaoingia kwenye elimu ya mfumo rasmi kuongezeka mwaka hadi mwaka.

**Elimu ya Watu Wazima na Nje ya Mfumo Rasmi**

74. ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali inaendelea na utekelezaji na usimamizi wa Elimu ya Watu Wazima kwa njia ya vikundi vya uzalishaji mali. Katika mwaka 2018 jumla ya vikundi **208** vilifikiwa kwa ajili ya masomo ya ujasiriamali, na ujifunzaji wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Idadi ya wanakisomo **63** walipatiwa vyeti vya kuhitimu mafunzo yao. Wanakisomo **13,008** wanatarajiwa kufuzu mafunzo hayo mwezi Agosti, 2019.

75. ***Mheshimiwa Spika;*** idadi ya wanafunzi **14,033** wa MEMKWA kundirika la kwanza wanapatiwa masomo sawa na wanafunzi walio katika mfumo rasmi. Kati ya hao waliosajiliwa kufanya mtihani wa darasa la nne mwaka 2018 ni **6,019**, waliofanya mtihani ni **5,900** na waliofaulu kuingia darasa la tano ni **3,217**. Hadi Machi, 2019 jumla ya wanakisomo walioandikishwa ni **17,024.** Aidha, Programu ya Elimu Changamani kwa vijanabalehe wenye umri wa miaka 14 – 19 kundirika la pili, imeanzishwa kwa majaribio katika Mikoa **8** ambayo ni Kigoma, Tabora, Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe, Dodoma na Dar es Salaam inatarajia kuanza Julai, 2019. Programu hii inatarajiwa kuwanufaisha walengwa **10,000.**

76. ***Mheshimiwa Spika;*** walengwa wa programu hiyo ni Vijana ambao hawakuwahi kwenda shule, Wanafunzi walioacha shule ya Msingi, waliomaliza darasa la saba na kukosa fursa ya kuendelea na masomo, waliomaliza kupitia programu ya MEMKWA, wasichana walioacha shule kwa changamoto mbalimbali kama vile ujauzito na ndoa za utotoni.

**Elimu Maalum**

77. ***Mheshimiwa Spika***; hadi Februari, 2019 wanafunzi **49,655** wenye mahitaji maalum wameandikishwa ikilinganishwa na wanafunzi **42,786** walioandikishwa Februari, 2018 wakiwemo, wanafunzi ***viziwi, wasioona, wenye uoni hafifu, wenye usonji, wenye ulemavu wa viungo, na wenye ulemavu wa akili.*** Aidha, mwaka 2019 jumla ya wanafunzi **1,407** sawa na asilimia **71.9** ya wanafunzi **1,956** wenye mahitaji maalum walihitimu elimu ya msingi na kuchaguliwa kujiunga Kidato cha Kwanza.

**Elimu kwa Michezo**

78. ***Mheshimiwa Spika;*** OR-TAMISEMI imeendelea kuratibu na kusimamia michezo katika Shule za Msingi na Sekondari kuanzia ngazi ya shule hadi Taifa. Katika mwaka 2018 OR-TAMISEMI iliendeleza jitihada za kuimarisha uendeshaji wa mashindano ya michezo ya UMITASHUMTA na UMISSETA. Katika kipindi hicho jumla ya wanafunzi **2,120** wa Shule za Msingi, wanafunzi **2,360** wa Shule za Sekondari na zaidi ya walimu na viongozi **1,500** walishiriki mashindano ya michezo ya UMITASHUMTA na UMISSETA iliyofanyika Mkoani Mwanza.

79. ***Mheshimiwa Spika;*** kuimarika kwa mashindano hayo kumeendelea kuonesha mafanikio makubwa kwa Timu ya Taifa ya Soka kwa vijana wenye umri chini ya miaka **17** (Serengeti Boys) ambayo mwaka 2017 ilifanikiwa kushiriki fainali za Afrika zilizofanyika nchini Gabon. Aidha, Timu hiyo itakuwa mwenyeji kwenye fainali za **Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON)** kwa vijana yatakayofanyika nchini Tanzania mwaka 2019. Timu hiyo ya Vijana wa Serengeti inaundwa na wachezaji waliotokana na mashindano ya michezo ya UMITASHUMTA na UMISSETA kwa zaidi ya asilimia **85.** Vijana hao wamekuwa wakichaguliwa wakati wa michezo hiyo inayofanyika kila mwaka tangu Mwaka 2014. Michezo hiyo imekuwa ni chachu ya kupata wachezaji bora ambao wanajiunga kwenye vilabu vya michezo na hatimaye kwenye Timu ya Taifa.

80. **Mheshimiwa Spika;** Tanzania inatarajiwa kuwa mwenyeji wa mashindano ya michezo ya shule za sekondari na shule za msingi (FEASSSA) kwa nchi za Afrika ya Mashariki yaliyopangwa kufanyika Mkoani Arusha Agosti, 2019. Zaidi ya washiriki **5,000** kutoka katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanatarajiwa kuwepo Arusha kushiriki michezo hiyo. Michezo itakayoshindaniwa ni pamoja na soka, netiboli, mpira wa kikapu, mpira wa mikono, mpira wa kengele, riadha, *Rugby* na kuogelea.

81. ***Mheshimiwa Spika;*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaendelea na kuimarisha michezo kwa kuandaa mkakati wa Taifa na maendeleo ya elimu ya michezo katika shule. Aidha, Mwaka 2019, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kuendesha



HOTUBA OFISI YA RAIS TAMISEMI

mashindano ya UMMISETA na UMITASHUMTA yatakayofanyika Mkoani Mtwara ili kutoa fursa kwa vijana kuonesha vipaji vyao katika fani mbalimbali za michezo na soka. Michezo itakayoshindaniwa ni pamoja na soka, netiboli, mpira wa kikapu, mpira wa mikono, mpira wa wavu, riadha, mpira wa kengele, kwaya na ngoma. Jumla ya wanafunzi **2,000** wa shule za msingi na **2,200** wa shule za sekondari wakiwemo wenye mahitaji maalum, wanatarajiwa kushiriki mashindano hayo Mkoani Mtwara.

**Mkataba wa Utendaji Kazi kwa Walimu**

82. ***Mheshimiwa Spika***; katika uimarishaji na uendeshaji wa elimu OR - TAMISEMI imeandaa utaratibu wa mkataba wa utendaji kazi kwa walimu (Performance Contract) ambapo kupitia mkataba huo walimu watapimwa kwa kuangalia idadi ya vipindi walivyofundisha kulingana na ratiba ya masomo shuleni, ukamilishaji wa mihtasari, ufaulu kwenye masomo, uandaaji wa masomo na maazimio ya kazi. Lengo la mikataba hii ni kuongeza uwajibikaji na nidhamu ya kazi kwa Walimu.

**Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo**

83. **Mheshimiwa Spika;** Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili ulianza kutekelezwa Julai, 2018 kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi mwaka wa fedha 2022/23. Utekelezaji wa mpango huo unafanyika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(District Agricultural Development Projects).*

84. **Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari, 2019 OR – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara zinazoratibu Sekta ya Kilimo imeandaa Mwongozo wa kuandaa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs) ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II). Mwongozo huo umesambazwa katika Mikoa 26 na Halmashauri 185. Aidha, OR TAMISEMI kwa kushirikiana na Shirika la Mapinduzi ya Kijani Afrika (Alliance for Green Revolution in Africa- AGRA) imeandaa Mkakati uliowezesha kupata fedha kiasi cha **Shilingi bilioni 3.34** kwa ajili ya kuwajengea uwezo Maafisa Ugani katika mafunzo na vitendea kazi, Waratibu ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Viwanda, Biashara na Uwekezaji**

85. **Mheshimiwa Spika;** ujenzi wa viwanda unafanyika kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inayolenga kuifikisha Tanzania katika uchumi wa kati uliofungamanishwa na maendeleo ya watu ifikapo Mwaka 2025. Mamlaka za Serikali za Mitaa zina jukumu la kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kujenga misingi itakayorahisisha na kuvutia ukuaji wa sekta ya viwanda. Katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Ofisi ya Rais-TAMISEMI ilipanga kutenga ekari **228,543** kwa ajili ya viwanda vidogo, vya kati na vikubwa kwenye Mikoa 26. Hadi kufikia Desemba 2018, jumla ya hekta **777,110.48** zilikuwa zimeainishwa zikiwemo hekta **367,077.21** kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vikubwa, viwanda vya kati na viwanda vidogo; hekta **204,488.28** kwa ajili ya shughuli za kilimo na skimu za umwagiliaji, hekta **143,000** kwa ajili ya malisho ya mifugo na hekta **62,545** kwa ajili ya uwekezaji mwingine. Serikali imeunda timu ya wataalam kwa ajili ya kuhakiki maeneo hayo kama yanafaa kwa ajili ya uwekezaji na hayana migogoro.

86. **Mheshimiwa Spika;** OR-TAMISEMI ilizindua Kampeni ya ujenzi wa viwanda katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini ikiwa na kaulimbiu ya *Mkoa Wetu, Viwanda Vyetu.* Lengo kuu la kaulimbiu hiyo ilikuwa ni kutoa hamasa kwa Viongozi na wananchi kushiriki kikamilifu kuwezesha uwepo wa viwanda katika maeneo yao ili kukuza uchumi na ustawi wa maisha ya wananchi. Kaulimbiu ya Mkoa Wetu, Viwanda Vyetu imeleta msukumo mpya wa ujenzi wa viwanda na kuongeza idadi ya viwanda vikubwa, vya kati na vidogo kufikia **4,877** sawa na **asilimia 187.6** ya lengo la kujenga viwanda **2,600** kuanzia Novemba, 2017 hadi Februari, 2019. Viwanda vikubwa vilivyojengwa kwa kipindi hicho ni **108**, viwanda vya kati **236**, viwanda vidogo **2,522** na viwanda vidogo sana **2,011.**

87. **Mheshimiwa Spika;** Mkoa wa Dar es Salaam ndio ulioongoza kwa kujenga viwanda vikubwa **46** ukifuatiwa na Mkoa wa Pwani wenye viwanda **8.** Vilevile, Mkoa wa Dar es Salaam umeongoza kwa kujenga viwanda vidogo **245** ukifuatiwa na Mkoa wa Pwani wenye viwanda **219**. Mkoa wa Geita umeongoza kwa kujenga viwanda vya kati **57** ukifuatiwa na Mkoa wa Mbeya uliofanikiwa kujenga viwanda **40.** Viwanda vya kati vilivyojengwa katika Mikoa ya Mbeya na Geita ni vile vinavyojishughulisha na uchenjuaji wa madini ya dhahabu ambayo hupatikana kwa wingi katika Mikoa hiyo. Vilevile, Mkoa wa Lindi umefanya vizuri katika ujenzi wa viwanda vidogo kwa kuanzisha viwanda **452** vinavyojihusisha na ubanguaji wa korosho ukifuatiwa na Mkoa wa Mara wenye viwanda **377.** Kwa ujumla kumekuwa na mwitikio mkubwa wa uanzishaji wa viwanda katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambavyo vimeajiri watu **35,796.**

**Miradi ya Kimkakati Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

88. ***Mheshimiwa Spika;*** utaratibu wa utekelezaji wa Miradi ya kimkakati ulianza katika Mwaka wa Fedha 2017/18. Kupitia utaratibu huo, Halmashauri zinaandaa maandiko ya miradi ambayo inapatiwa fedha za utekelezaji baada ya kukidhi vigezo. Miradi hiyo inapaswa kuwa na sifa ya kuiwezesha Halmashauri kuongeza mapato ya ndani ya Halmashauri ili kuziwezesha kujitegemea kimapato na kupunguza utegemezi wa Ruzuku ya Serikali Kuu. Hadi Februari, 2019 jumla ya Halmashauri **29** zenye miradi **37** zimekidhi vigezo vya kupatiwa jumla ya **Shilingi bilioni 268.84** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kimkakati.

89. ***Mheshimiwa Spika;*** katika Awamu ya Kwanza, Halmashauri 18 zenye miradi **23** zilikidhi vigezo vya kupatiwa jumla ya **Shilingi bilioni 131.46.** Kati ya Fedha hizo, **Shilingi bilioni 31.36** zimepokelewa kwenye Halmashauri hizo ambazo zimesaini mikataba ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati. Fedha hizo zitatumika kutekeleza miradi ya ujenzi wa masoko, viwanda, machinjio, vituo vya mabasi na maghala ya kuhifadhia mazao.

90. ***Mheshimiwa Spika;*** katika Awamu ya Pili, Halmashauri nyingine 12 zenye miradi 15 zimekidhi vigezo vya kupatiwa jumla ya **Shilingi bilioni 137.37** mwezi Januari, 2019. Halmashauri zimesaini mikataba ya utekelezaji wa miradi hiyo itakayohusisha ujenzi wa masoko ya kisasa, machinjio ya kisasa, vituo vya mabasi, uendelezaji wa ufukwe wa Oysterbay, kiwanda cha kusindika korosho na ujenzi wa kitega uchumi kwenye kituo cha mabasi Kange Mkoani Tanga. Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango inaendelea kujenga uwezo kwa Halmashauri kuziwezesha kuibua miradi, kufanya upembuzi yakinifu ili miradi hiyo iweze kukidhi vigezo na kupata fedha na kuitekeleza kwa ufanisi.

**Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi**

91. **Mheshimiwa Spika;** kufuatia marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 Kifungu cha **37A** Mikopo inayotokana na **asilimia 10** ya mapato ya ndani sasa inatolewa bila riba kuanzia Julai, 2018 kwa kuzingatia mgawanyo wa **asilimia 4** kwa Wanawake, **asilimia 4** kwa Vijana na **asilimia 2** kwa Watu Wenye Ulemavu. Uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi umeendelea kufanyika ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 Sura ya Tano (5) inayohusu Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi. Hadi Februari, 2019, jumla ya **Shilingi bilioni 13.2** kati ya **Shilingi bilioni 54.08** sawa na **asilimia 24.4** zimetolewa kama mikopo kwa vikundi **5,628** kati ya vikundi **28,025** vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 8.04** zimetolewa kwa vikundi **3,835** vya Wanawake, Shilingi **bilioni 4.7** zimetolewa kwa vikundi **1,606** vya Vijana na **Shilingi milioni 415.96,** zimetolewa kwa vikundi **187** vya Watu Wenye Ulemavu.

92. **Mheshimiwa Spika;** kupitia Programu ya Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (*Local Investment Climate -LIC)*, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kuwezesha wananchi kiuchumi katika Sekta za Kilimo, Biashara na Uvuvi katika Mikoa ya Kigoma na Dodoma. Maeneo ya kipaumbele ni uzalishaji na uchakataji wa mazao ya Michikichi, Zabibu, Mbogamboga, Muhogo, Mpunga, Alizeti na Ufugaji wa Samaki. Miradi 44 imeibuliwa katika Halmashauri za Mikoa ya Dodoma na Kigoma yenye thamani ya **Shilingi bilioni 6.2.**

93. **Mheshimiwa Spika;** miradi hiyo inahusisha ukarabati wa miundombinu ya skimu za umwagiliaji 7 zikiwemo 4 za Mkoa wa Dodoma maeneo ya Mpunguzi na Bahi na skimu 3 za Mkoa wa Kigoma katika maeneo ya Nyindera na Mgambazi, masoko 7, minada 6, machinjio 7 ya kisasa, viwanda vidogo 5 na ujenzi wa Vituo 13 vya kutolea huduma za pamoja za biashara *(One Stop Business Centres).* Vituo hivyo vimesaidia kuongeza ufanisi ambapo leseni za biashara zinatolewa kwa wastani wa siku 1 au 2 ikilinganishwa na wastani wa siku 7 za awali. Hadi Februari 2019, jumla ya wafanyabiashara **16,173** wamepatiwa leseni za biashara katika Halmashauri za Mkoa wa Dodoma na wafanyabiashara **5,051** wamepatiwa leseni katika Halmashauri za Mkoa wa Kigoma. Vilevile, mradi wa LIC umesaidia upatikanaji wa vifaa vya kukusanyia mapato *(Point of Sale Machine -POS)* **505** katika Mikoa ya Dodoma na Kigoma ili kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri.

94. **Mheshimiwa Spika;** utekelezaji wa miradi hiyo umechochea ukuaji wa uchumi kwenye maeneo husika pamoja na kuongeza ajira zipatazo **18,896** ambapo Wanawake ni **6,586** na Wanaume **12,310**. Aidha, Wafugaji na Wakulima wapatao **2,300** wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali kuhusu kuandaa maandiko ya miradi na kuwaunganisha na Taasisi mbalimbali za Fedha kwa lengo la kupata mikopo ili kukuza mitaji yao na ajira. Aidha, utoaji wa Vitambulisho kwa Wafanyabiashara Wadogo unaendelea ambapo hadi tarehe 25 Machi, 2019 vitambulisho **1,850,000** vimetolewa kwa Wakuu wa Mikoa. Kati ya vitambulisho hivyo, vitambulisho **820,104** tayari vimetolewa kwa wafanyabiashara wadogo sawa na **asilimia 44** ambapo hadi Machi, 2019 jumla ya **Shilingi 16,402,080,000.00** zilikuwa zimekusanywa kutokana mauzo ya vitambulisho hivyo.

**Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma**

95. **Mheshimiwa Spika;** Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo inaendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tano ya Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma katika Mikoa 26 kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi mwaka wa fedha 2021/22. Wadau wanaoshirikiana na Serikali katika utekelezaji wa programu ni Shirika la Maendeleo la Uingereza (DfID) na Nchi za Norway na Sweden.

96. **Mheshimiwa Spika;** utekelezaji wa programu unahusisha shughuli za kuimarisha mifumo ya upangaji mipango na bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, usimamizi wa mapato na matumizi na ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri, utekelezaji wa bajeti na uandaaji wa taarifa, usimamizi wa matumizi ya fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuimarisha mifumo ya usimamizi, udhibiti na uwazi.

97. **Mheshimiwa Spika;** hadi Februari 2019, programu imeimarisha Mfumo Funganishi wa Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha ambao umefungwa katika Halmashauri 184 ili kuhakikisha mfumo huo unakuwa endelevu. Aidha, umeandaliwa mwongozo wa ukusanyaji mapato ya ndani ya Halmashauri na kusambazwa kwenye Halmashauri hizo ili kuziwezesha kubuni vyanzo vipya vya mapato na kusimamia makusanyo katika vyanzo vilivyopo.

# HOTUBA OFISI YA RAIS TAMISEMI

Vilevile, Mashine **6,000** za kukusanyia mapato *(Point of Sale Machine-POS)* zimenunuliwa ili kuziwezesha Halmashauri zenye uwezo mdogo kuweza kukusanya mapato zaidi.

**Uendelezaji wa Vijiji na Miji**

**98. Mheshimiwa Spika;** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, ustawi wa jamii yetu uliendelea kuimarika sambamba na uendelezaji uliofanyika Vijijini na Mijini. Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaendelea na jukumu la kuhakikisha kuwa Mamlaka za Upangaji (Majiji, Manispaa, Halmashauri za Wilaya, Miji na Mamlaka za Miji Midogo) na Vijiji zinaandaa Mipango ya Uendelezaji wa maeneo hayo kwa kuzingatia Sera na Sheria zinazohusu Uendelezaji wa Vijiji na Miji.

**99. Mheshimiwa Spika;** miji nchini inakua kwa kasi na mingine mipya inachipukia. Uendelezaji na uendeshaji wa miji unaimarika japokuwa zipo changamoto za utoaji wa huduma kutokana na maeneo mengi kutopangwa vizuri. Takriban asilimia 60 ya nyumba mijini zimejengwa kwenye maeneo yasiyo rasmi ambapo asilimia 80 ya wakazi wa miji wanaishi kwenye maeneo hayo. Wakazi mijini wameongezeka kutoka watu **555,535 (5.3%)** mwaka **1961** hadi kufikia **12,694,875 (29.1%)** mwaka **2012.** Idadi hiyo ina nguvukazi yenye uwezo wa kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii nchini na ambayo inahitaji iwekewe mazingira mazuri ili ilete mabadiliko chanya ya kimaendeleo kwa nchi.

**100.*Mheshimiwa Spika;*** Ofisi ya Rais – TAMISEMI inatambua mchango wa utekelezaji wa programu, miradi na mikakati ya uendelezaji wa miji kupitia uimarishaji wa miundombinu, Mifumo ya Taarifa za Kijiografia na TEHAMA, ukusanyaji na udhibiti wa mapato, usafi na takangumu, utunzaji wa mazingira, ukuzaji kipato na ustawi wa jamii. Katika kuendeleza juhudi hizo Serikali inaiwezesha Miji kuwa na jamii iliyoelimika vizuri, shirikishi, shindani na yenye utangamano na Vijiji katika kuleta maendeleo nchini.

**101.*Mheshimiwa Spika;*** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilikamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Utoaji wa Vibali vya Ujenzi na Usimamizi wa Ukaguzi wa Majengo wa Machi, 2018 na kuusambaza kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara. Kila Halmashauri imeanzisha kituo kimoja *(One Stop Centre)* cha utoaji wa Vibali vya Ujenzi kupitia Kamati Ndogo za Wataalam. Tathmini ya matokeo kwenye Halmashauri 184 yamebainisha kupungua kwa muda wa kutoa Vibali vya Ujenzi kutoka siku **60** hadi siku **7** kwa majengo ya kawaida na siku **30** kwa majengo makubwa. Katika kipindi cha Julai 2018 hadi Februari 2019 Vibali vya Ujenzi **9,469** vilitolewa kwenye Halmashauri. Idadi hiyo imeongezeka kwa wastani wa mara 4 ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 ambapo Vibali **2,341** vilitolewa.

**102.*Mheshimiwa Spika;*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Anwani za Makazi na Postikodi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Kazi zinazofanyika kwenye Halmashauri zote **185** ni kutoa elimu na kuihamasisha jamii, kuainisha na kuyahakiki majina ya barabara na mitaa, na namba za nyumba. Uwekaji miundombinu ya Mfumo wa Anwani za Makazi umefanyika katika Halmashauri **13** za Majiji ya Mwanza, Dodoma na Tanga, Halmashauri za Manispaa za Morogoro, Moshi na Shinyanga, Halmashauri za Miji ya Kibaha na Geita na Halmashauri za Wilaya za Chato, Chamwino, Bahi, Buchosa na Sengerema zimechaguliwa kuanza kuweka miundombinu hiyo. Manufaa ya mpango huu ni kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi kwa kuyatambua maeneo mbalimbali na kuyafikia kwa urahisi.

**103.*Mheshimiwa Spika;*** katika kuendeleza Vijiji na Miji, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuimarisha matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Kijiografia *(Geographical Information System - GIS)* kwenye Mikoa na Halmashauri zote nchini. Mfumo huu umeongeza ufanisi na uwazi katika ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu za kijiografia, ukusanyaji wa mapato, kusimamia masuala ya uendelezaji Vijiji na Miji. Hadi sasa Mamlaka za Serikali za Mitaa **148** kati ya **184** sawa na asilimia **80** zinatumia Mfumo huu. Mfumo umewezesha kuainisha **Miji Midogo Inayochipukia 1,165** ili iweze kuendelezwa kutoka Vijiji kuwa Miji Midogo kwa kuwa ina fursa za maendeleo na ndiyo ngazi ya msingi ya ukuaji wa Miji na ustawi wa Vijiji.

**104.*Mheshimiwa Spika*;** Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliendelea kuratibu uandaaji wa Mipango ya Jumla (General Planning Schemes) ya Uendelezaji Miji ambapo hadi kufikia Februari 2019, Mipango Kabambe ya Miji 10 ya Manispaa za Singida, Musoma, Mtwara, Iringa, Tabora na Songea; Miji ya Korogwe, Kibaha, Tunduma, na Bariadi imekamilika. Mipango hiyo itaongoza uendelezaji wa Miji na kudhibiti ujenzi holela. Mipango Kabambe ya Majiji ya Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Mwanza na Arusha pamoja na Halmashauri zilizobaki iko kwenye hatua za uandaaji. Serikali inatumia mbinu na utaalam mbalimbali wa kisasa katika kufanya marekebisho ya uendelezaji wa miji iwe himilivu na ya kisasa.

**Utekelezaji wa Mpango wa Serikali Kuhamia Dodoma**

**105.*Mheshimiwa Spika;*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imesimamia utungwaji wa Sheria ya Kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi ambapo Muswada wa Sheria hiyo ulijadiliwa na Bunge lako Tukufu katika Mkutano wa 12 wa Bunge mwezi Septemba, 2018 na kupitishwa kuwa sehemu ya Sheria za Nchi. Kutungwa kwa Sheria hiyo ni utekelezaji wa uamuzi wa Serikali uliotolewa Mwaka 1973 wa kuhamisha Makao Makuu ya Nchi kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma. Aidha, huu ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 katika Ibara ya 151 (a) iliyoielekeza Serikali Kutunga Sheria itakayotambua Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi. Uamuzi huo uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano umeleta hamasa kubwa ya maendeleo kwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma na Watanzania wote kwa kuanza kujenga nyumba bora za makazi, kuongezeka kwa uwekezaji wa huduma mbalimbali za jamii na uboreshaji wa miundombinu ya kiuchumi ya barabara, viwanja vya ndege na ujenzi wa Mji wa Serikali.

**106. *Mheshimiwa Spika;*** Halmashauri ya Jiji la Dodoma imekabidhiwa dhamana ya kusimamia uendelezaji na uendeshaji wa Makao Makuu ya Nchi. Kazi kubwa zilizofanyika ni kuongeza kasi ya upimaji wa maeneo ili kuhakikisha uendelezaji unafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Mipango Miji ya Mwaka 2007. Vilevile, Halmashauri kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) inaendelea kujenga barabara za lami na changarawe kurahisisha upitikaji katika maeneo yote likiwemo eneo la Mji wa Serikali.

**107.*Mheshimiwa Spika*;** katika kutekeleza azma ya Serikali kuhamia Dodoma, Ofisi ya Rais – TAMISEMI inashiriki katika kutekeleza Mpango wa Kuendeleza Makao Makuu ya Nchi. Mpango Kabambe wa Jiji la Dodoma unafanyiwa mapitio ili kuandaa Mpango Kabambe ambao utakidhi na kuendana na uendelezaji wa Makao Makuu ya Nchi.

**C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA OFISI YA RAIS-TAMISEMI**

**Tume ya Utumishi wa Walimu**

**108.*Mheshimiwa Spika;*** Tume ya Utumishi wa Walimu kupitia vikao vya Kisheria ilipokea na kujadili mashauri ya kinidhamu **1,917** na kuyatolea uamuzi kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Kati ya mashauri hayo **529** yalihitimishwa, **812** yapo katika hatua ya uchunguzi na **576** yatahitimishwa kabla ya Juni, 2019. Aidha, rufaa **114** zilipokelewa na kujadiliwa ambapo rufaa **62** zilihitimishwa na rufaa **52** zipo kwenye hatua za uhitimishwaji.

**109.*Mheshimiwa Spika;*** katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Tume imefanya ufuatiliaji katika Wilaya za Tanga, Muheza, Ubungo, Ilala, Temeke, Kinondoni, Kisarawe na Kibaha ili kuangalia utekelezaji wa majukumu yake na changamoto zinazoikabili katika ngazi ya Wilaya. Matokeo ya ufuatiliaji huo umeiwezesha Tume kuratibu upatikanaji wa taarifa za kiutumishi za Walimu **95,578** ambapo Walimu wa Shule za Msingi ni **70,768** na Walimu wa Shule za Sekondari ni **24,810**. Jumla ya walimu **1,652** walithibitishwa kazini wakiwemo wa Shule za Msingi **1,124** na Shule za Sekondari **528.** Aidha, Walimu wanaojiendeleza ni **8,643** ambapo kati yao, Walimu wa Shule za Msingi ni **5,911** na Walimu wa Shule za Sekondari ni **2,732.**

**Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)**

**110.Mheshimiwa Spika;** Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini unasimamia mtandao wa barabara zenye urefu wa **kilometa 108,946.19** ambazo zinajumuisha barabara za lami **kilometa 1,449.55,** barabara za changarawe **kilometa 24,405.40** na barabara za udongo **kilometa 83,091.24** pamoja na ujenzi wa **madaraja 2,760** na **makalvati 52,454.**
Lengo la Wakala ni kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja ili kufungua fursa za kiuchumi na kijamii Vijijini na Mijini.

**Mapokezi ya Fedha za Mfuko wa Barabara**

**111.Mheshimiwa Spika;** hadi kufikia Machi, 2019 Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ulikuwa umepokea **Shilingi bilioni 136.02** kati ya **Shilingi bilioni 243.27** za Mfuko wa Barabara zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2018/19 sawa na **asilimia 56**. Aidha, TARURA imeweza kujenga **kilomita 5,565.30** za barabara, **madaraja 167**, Makalvati makubwa (Box Culverts) 27, *drift* **59** na mifereji ya maji yenye urefu wa **mita 51,347**. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2018/19, TARURA imenunua magari **22** ili kuimarisha usimamizi wa barabara katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. TARURA pia inaendelea na ujenzi wa jengo la utawala la Makao Makuu katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba Jijini Dodoma.

**112.Mheshimiwa Spika;** TARURA imefanikiwa kununua Mashine (POS) **664** za kukusanyia ushuru wa matumizi ya maeneo ya hifadhi za barabara na maegesho ya magari ili kuongeza mapato yatakayowezesha Wakala kumudu utekelezaji wa majukumu yake. Hadi Machi, 2019, TARURA imekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 8.71** sawa na **asilimia 78.20** ya lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 11.14** kutokana na matumizi maeneo ya hifadhi ya barabara zilizo chini ya TARURA na maegesho ya magari. Mafanikio hayo yanatokana na ushirikiano madhubuti kati ya TARURA na Wadau kupitia Kamati za Ushauri za Wilaya na Mikoa. TARURA inaendelea kufanya mipango ya kujiimarisha ili kuongeza maeneo mengine ya ukusanyaji wa mapato. Ofisi ya Rais-TAMISEMI inaendelea kuimarisha ufuatiliaji na usimamizi ili kuhakikisha TARURA inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Programu ya Uboreshaji wa Barabara Vijijini**

**113.Mheshimiwa Spika;** kupitia Programu ya Uboreshaji wa Barabara Vijijini inayofadhiliwa na DfID, jumla ya barabara zenye urefu wa **kilometa 151** zimejengwa kwa kiwango cha changarawe pamoja na madaraja **3** na makalvati makubwa **42** katika Halmashauri za Wilaya za Iramba, Kyela, Kyerwa, Rungwe, Bahi, Gairo, Kishapu, Babati, Mpwapwa, Magu, Busokelo, Bariadi, Kondoa, Kisarawe, Kibiti, Ushetu, Songwe na Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa gharama ya **Shilingi bilioni 28.88.** Aidha, Halmashauri ya Manispaa ya Iringa inaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa daraja la Tagamenda na Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero imekamilisha ujenzi wa barabara ya Chita hadi Melela.

**114.Mheshimiwa Spika;** kupitia Programu inayofadhiliwa na Umoja wa Ulaya *(Road Transport Sector Policy Support Programme*

## HOTUBA OFISI YA RAIS TAMISEMI

*RTSPSP II)*, jumla ya **kilometa 219.6** za barabara zimejengwa ambapo kati ya hizo **kilometa 21.3** zimejengwa kwa kiwango cha lami na **kilometa 198.3** zimejengwa kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya **Shilingi bilioni 16.07.** Mradi unatekelezwa katika Halmashauri za Wilaya za Chamwino, Kilolo, Kondoa, Kisarawe, Songea, Mbinga, Mwanga, Mbulu, Kongwa, Mbogwe, Busokelo, Kalambo, Iringa, Ludewa, Hanang, Kiteto na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke. Mara baada ya kukamilika kwa barabara hizo zitarahisisha usafiri na usafirishaji.

115.**Mheshimiwa Spika;** Serikali kwa kushirikiana na USAID kupitia Programu ya *Feed the Future* inatekeleza miradi ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara katika Halmashauri za Wilaya za Kongwa, Kiteto, Mvomero na Kilombero. Hadi Februari 2019, kilometa **152.1** za barabara zimejengwa kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya **Shilingi bilioni 7.56.** Mradi huo utakapokamilika utawezesha wakazi wa Halmashauri hizo kusafirisha mazao kwa urahisi hadi kwenye masoko na hivyo kukuza kipato.

**Mradi wa Kuendeleza Jiji la Dar es Salaam (DMDP)**

116.**Mheshimiwa Spika;** kupitia mradi huu, Serikali imeweza kujenga jumla ya kilometa **75.5** kati ya kilometa **210** za barabara zinazotarajiwa kujengwa kwa kiwango cha lami na Ofisi 3 zenye maabara ya kisasa. Aidha, umeandaliwa Mpango Kabambe wa Maji ya Mvua na Maji taka utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka kumi na saba (17) kuanzia Mwaka 2018 hadi 2035 kwa ajili ya kutatua changamoto za mafuriko katika Jiji la Dar es Salaam.

117.**Mheshimiwa Spika;** kazi nyingine zilizofanyika ni kuweka taa **5,000** za barabarani za mfumo wa jua na mitaro ya maji ya mvua kilomta **2.8**, ujenzi wa madaraja makubwa mawili ya Vimbili na Ulongoni katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, masoko **10**, vizimba **54**, vituo **7** vya huduma ya vyoo, vituo **6** vya maeneo ya mapumziko, vituo **12** vya huduma ya maji safi na ujenzi wa njia za waenda kwa miguu zenye urefu wa **kilometa 5,** ununuzi wa samani, ujenzi wa Kituo cha Afya cha Buza katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke na masoko kumi (**10**) ya kisasa ambayo yapo katika hatua za ujenzi. Utekelezaji wa miradi hii unagharimu jumla ya **Shilingi bilioni 207.**

118.**Mheshimiwa Spika;** hivi sasa Ofisi ya Rais-TAMISEMI inakamilisha maandalizi ya mikataba kwa ajili ya kujenga barabara zenye urefu wa kilometa **61.3,** mifereji mikubwa (storm water drains) yenye urefu wa kilometa **40** kwenye maeneo ya mto ya Sinza, Kiboko, Gerezani na Kizinga; Bonde la Sungura, Mafuriko, Yombo, Buguruni Kisiwani, Msimbazi Tenge-Liwiti pamoja na ujenzi wa mabwawa makubwa **4** ya kuhifadhi maji ya mvua. Aidha, vizimba **12** vitajengwa kwa kwa ajili ya kuhifadhi taka ngumu, kuweka huduma za maji katika vituo **8** na kuweka taa za barabarani **1,054.**

**Mradi wa Uendelezaji Miji ya Kimkakati Tanzania (TSCP)**

119.**Mheshimiwa Spika;** kupitia mradi huo unaotekelezwa katika Majiji ya Tanga, Arusha, Mbeya, Dodoma, Mwanza na Halmashauri za Manispaa za Mtwara-Mikindani, Kigoma Ujiji na Ilemela, miradi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa kilometa **80.22** inaendelea kutekelezwa. Miradi mingine inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa madampo ya kisasa mawili (2), ujenzi wa maeneo ya kuwekea makontena ya kukusanyia taka ngumu kwenye mitaa, ujenzi wa maeneo mawili ya mapumziko (Public Parks), ujenzi wa mitaro mikubwa ya maji ya mvua kilometa **16.47** na ujenzi wa kituo kimoja cha kuegesha malori.

120.**Mheshimiwa Spika;** kazi nyingine zilizotekelezwa kupitia Mradi wa Uendelezaji wa Miji ya Kimkakati Tanzania (TSCP) ni ujenzi wa vivuko sita (6) vya waenda kwa miguu, ujenzi wa kituo kikubwa kimoja cha mabasi katika Jiji la Dodoma, stendi mbili (2) za daladala katika Manispaa ya Mtwara-Mikindani na masoko makubwa mawili ya kisasa katika Jiji la Dodoma na Manispaa ya Mtwara Mikindani. Gharama za miradi hiyo ni **Shilingi bilion 214.74.**

**Programu ya Kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa za Miji 18 (ULGSP)**

121.**Mheshimiwa Spika;** kupitia Programu hii Serikali imeweza kujenga barabara zenye urefu wa kilometa **116.6** kati ya kilometa **155.7** zinazotarajiwa kujengwa kwa kiwango cha lami katika Halmashauri za Manispaa za Morogoro, Tabora, Moshi, Sumbawanga, Shinyanga, Songea, Iringa, Mpanda, Lindi, Singida, Musoma na Bukoba na Halmashauri za Miji ya Kibaha, Babati, Geita, Korogwe, Bariadi na Njombe. Aidha, magari makubwa 26 yamenunuliwa kwa ajili kusombea taka ngumu; mitambo mikubwa minane (8) kwa ajili ya kupakilia taka na ukarabati wa dampo moja (1). Vilevile, vituo tisa (9) vya mabasi vinajengwa ambapo kati ya hivyo, vituo vitano (5) vimekamilika. Vituo hivyo, vinajengwa katika Halmashauri za Manispaa za Songea (2), Singida (2) na Iringa na Halmashauri za Miji ya Njombe Bariadi, Korogwe, Kibaha na machinjio nne (4) za kisasa katika Halmashauri za Manispaa za Lindi, Songea, Shinyanga na Halmashauri ya Mji wa Geita.

122.**Mheshimiwa Spika;** kazi nyingine zinazotekelezwa chini ya Programu hii ni ujenzi wa masoko matatu (3) ya kisasa katika Manispaa za Morogoro, Iringa na katika Mji wa Njombe na ujenzi wa kituo kimoja cha malori katika Manispaa ya Sumbawanga. Vilevile mradi umewezesha ununuzi wa picha za anga (Satellite Images) za Miji 18 kwa ajili ya kuboresha mfumo wa Mipango Miji na Mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Miji.

**Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam**

123.**Mheshimiwa Spika;** Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam (DART) umekamilisha maandalizi ya utekelezaji wa Awamu ya Pili ya ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka itakayohusisha barabara za Kilwa, Kawawa, Sokoine, Gerezani, Bandari na Chang'ombe yenye urefu wa kilometa **20.3.** Utekelezaji wa mradi huo unafanyika kwa mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Wananchi na Taasisi **90** kati ya **105** wamelipwa fidia ya **Shilingi bilioni 28.52** kati ya **Shilingi bilioni 34.19** zilizopangwa kulipwa ili kupisha utekelezaji wa mradi.

124.**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam (DART) umeanza maandalizi ya utekelezaji wa Awamu ya Tatu itakayohusisha barabara za Azikiwe na Maktaba, Bibi Titi na Nyerere kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) hadi Gongo la Mboto; kituo kikuu cha mabasi Kariakoo Gerezani kupitia Mtaa wa Lindi, Shaurimoyo na Uhuru kupitia Buguruni hadi TAZARA zenye urefu wa kilometa **23.6.** Aidha, wananchi wapatao **78** (PAPs) wanaoguswa na mradi mali zao zimethaminiwa kwa ajili ya kulipwa fidia. Vilevile, Serikali imetoa eneo la Gongo la Mboto kwa ajili ya ujenzi wa karakana ya mabasi *(bus depot),* eneo ndani ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere kwa ajili ya kujenga kituo cha mabasi kuunganisha uwanja huo na huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam na eneo la kujenga kituo mlisho cha Banana karibu na eneo zilipo ofisi za TCAA.

**Chuo cha Serikali za Mitaa - Hombolo**

125.***Mheshimiwa Spika;*** Chuo cha Serikali za Mitaa kilichopo Hombolo kimedahili wanafunzi wapatao **5,943** ikilinganishwa na lengo la kudahili wanafunzi **3,500** sawa na **asilimia 169.8.** Ongezeko la udahili huo limetokana na Serikali kuamua wanafunzi waliokosa nafasi ya kujiunga na Kidato cha Tano Mwaka 2018 kujiunga na Vyuo mbalimbali kikiwemo Chuo cha Serikali za Mitaa-Hombolo. Vilevile, Chuo kimepata ithibati ya kuanza kufundisha Shahada mbili za Utawala na Rasilimali Watu na Utawala na Uongozi katika Serikali za Mitaa ambazo zitaanza kudahili wanafunzi katika mwaka wa masomo 2019/20.

126.***Mheshimiwa Spika;*** Chuo kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi wa Chuo na Watendaji na Viongozi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari 2019, Chuo kimegharamia mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 39 na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 106 ili kujenga uwezo wa Chuo kutekeleza majukumu yake. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo kwa watumishi **266** kutoka katika Halmashauri **18** kuhusu utawala bora, uendeshaji wa miradi ya ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi, ukusanyaji wa mapato, uendeshaji wa vikao vya kisheria, usimamizi wa miradi na uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika mipango na bajeti.

127.***Mheshimiwa Spika;*** ili kuboresha mazingira ya utoaji wa mafunzo, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari, 2019, Chuo kimenunua viti **458** vikiwemo viti **168** visivyohamishika na viti **290** vinavyohamishika, *projector* **8** na *braille* mashine **4** kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Vilevile, katika kipindi hicho Chuo kimenunua eneo la ekari **2.7** katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa gharama ya **Shilingi milioni 74.7** kwa ajili ya kujenga kituo cha mihadhara na mafunzo ya muda mfupi katika eneo la Iyumbu.

128.***Mheshimiwa Spika;*** Chuo kimefanya tafiti katika nyanja za ukusanyaji wa mapato, uchumi wa viwanda, ukatili na unyanyasaji wa jinsia pamoja na dawati la kushughulikia malalamiko kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Tafiti hizo zimesaidia kutoa mchango katika mipango ya Serikali kwa ajili ya kuboresha ustawi wa wananchi na maendeleo ya kiuchumi.

**Shirika la Elimu Kibaha**

129.**Mheshimiwa Spika;** Shirika kupitia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha linatoa mafunzo na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa lengo la kulijengea uwezo Shirika. Chuo kimeendelea kutoa mafunzo katika fani za kilimo na ufugaji, majengo na ujenzi, uchomeleaji na uundaji wa vifaa vya chuma, ufundi umeme, ushonaji, usimamizi wa hoteli, ufundi wa magari pamoja na udereva. Chuo kina uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi **400** kwa mwaka. Shirika limeanzisha shamba la mifugo lenye Ng'ombe **71** wenye uwezo wa kuzalisha lita **13,640** za maziwa ghafi kwa miezi mitatu.

130.**Mheshimiwa Spika;** Shirika lina shule moja ya msingi iitwayo Tumbi yenye wanafunzi **916**. Vilevile, Shirika lina shule tatu za sekondari ambazo ni Kibaha Sekondari (wavulana) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **840**, Shule ya Sekondari Tumbi (Mchanganyiko) yenye wanafunzi **659** na Shule ya Sekondari ya Kibaha (Wasichana) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **320.** Shirika linaendelea kusimamia shule hizo ikiwa ni mpango wa kupambana na adui ujinga kwa kuhakikisha fursa mbalimbali za elimu zinatolewa kwa jamii.

**Shirika la Masoko Kariakoo**

131.**Mheshimiwa Spika;** Shirika la Masoko Kariakoo katika kipindi cha kuanzia Julai 2018 hadi Februari, 2019 limekusanya mapato kiasi cha **Shilingi bilioni 1.7** kati ya lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 3.49** sawa **asilimia 48.7** ya makadirio. Vilevile, katika kipindi hicho, Shirika limefanikiwa kujenga maduka **94** kuzunguka jengo la Soko Kuu ili kuongeza makusanyo ya mapato ya Shirika. Ujenzi wa maduka hayo umeongeza uwezo wa Shirika kukusanya mapato **Shilingi milioni 602.98** kwa mwaka.

132.**Mheshimiwa Spika;** Shirika limefanikiwa kufunga mfumo wa kielektroniki *(Local Government Revenue Collection Information System- **LGRCIS**)* na kununua mashine mpya (*Point of Sale Machine-POS*) 27 zinazotumika kukusanya mapato. Matumizi ya mfumo wa kielektroniki yamechangia kuimarisha makusanyo kufikia **Shilingi bilioni 1.7** hadi Februari, 2019 ikilinganishwa na makusanyo

# HOTUBA OFISI YA RAIS TAMISEMI

halisi ya **Shilingi bilioni 1.62** yaliyokusanywa hadi Februari, 2018 sawa na ongezeko la **Shilingi milioni 80**. Makusanyo ya mapato hayo yanatokana ushuru wa mazao, ada ya kutumia soko na ada ya maegesho katika eneo la soko. Mapato hayo yametumika kuboresha hali ya soko na kuliwezesha Shirika kukusanya mapato zaidi kutokana na vyanzo hivyo.

**133. Mheshimiwa Spika;** Shirika limeandaa mkakati wa uwekezaji katika viwanja vilivyoko Mbezi Beach, Tabata na eneo la Soko Kuu kwa kufanya uwekezaji mkubwa ambapo tayari Shirika limeyatangaza maeneo hayo kwa shughuli za uwekezaji kwa mfumo wa ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi. Makampuni mbalimbali yameonesha nia ya kuwekeza katika viwanja hivyo. Utekelezaji wa mpango huo utaliwezesha Shirika kuongeza mapato na kuboresha utoaji wa huduma kwa wadau wake.

**Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

**134. Mheshimiwa Spika;** kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari, 2019 Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imesimamia na kuratibu urejeshwaji wa mikopo kutoka Halmashauri ambapo Halmashauri zimerejesha mikopo kiasi cha **Shilingi milioni 616.63** kutokana na mikopo iliyotolewa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 177.8** ni makusanyo ya mapato ya ndani yanayojumuisha riba ya mikopo, kodi ya nyumba za Bodi na gawio la hisa, **Shilingi milioni 244.8** ni marejesho ya mikopo kutoka kwenye Halmashauri zilizokopeshwa na **Shilingi milioni 194.03** ni Michango ya Akiba kutoka kwenye Halmashauri. Aidha, Bodi imewekeza kiasi cha **Shilingi bilioni 2.1** katika akaunti za amana za muda maalum kwenye Benki za Biashara ili kukuza mtaji wa Bodi kutoa huduma ya mikopo kwa wadau wake.

**D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20**

**135. Mheshimiwa Spika;** Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20, maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati wa kuzindua Bunge Mwaka 2015 na maelekezo ya Viongozi wengine wa Kitaifa, Sera na Nyaraka mbalimbali za Serikali na Mipango Mikakati ya Taasisi.

**Ofisi ya Rais-TAMISEMI**

**136. Mheshimiwa Spika;** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i) Kuratibu shughuli za Wizara za Kisekta na Wadau wengine, na kusimamia shughuli za Serikali katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
ii) Kuratibu na kusimamia shughuli za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwishoni mwa mwaka 2019;
iii) Kuratibu na kusimamia Utekelezaji wa shughuli za utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
iv) Kuratibu na kusimamia Utekelezaji wa shughuli za utoaji wa Elimumsingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
v) Kuandaa Sera na Mkakati wa kusimamia na kutekeleza dhana ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma;
vi) Kufanya marekebisho mbalimbali ya Sheria za Mamlaka za Serikali za Mitaa;
vii) Kutekeleza mkakati wa kudhibiti rushwa;
viii) Kudhibiti maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI na kuendelea kuwasaidia walioathirika;
ix) Kuratibu na kusimamia shughuli za Uendelezaji Vijiji na Miji iwe yenye ufanisi hususan Miji Midogo Inayochipukia;
x) Kuratibu shughuli za lishe katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
xi) Kukamilisha ujenzi wa Ofisi mpya ya OR-TAMISEMI katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba Jijini Dodoma;
xii) Kufanya ukaguzi, ufuatiliaji na tathimini kuhusu upelekaji wa fedha na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
xiii) Kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato na matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo kila Mkuu wa Idara amepewa Mkoa wa kusimamia;
xiv) Kuratibu na kusimamia mifumo ya TEHAMA katika ngazi zote za OR-TAMISEMI;
xv) Kuratibu na kusimamia masuala ya kiutumishi katika ngazi zote za OR-TAMISEMI;
xvi) Kuratibu shughuli na utendaji kazi wa Taasisi zilizopo chini ya OR- TAMISEMI;
xvii) Kuratibu shughuli za uboreshaji wa mazingira ya biashara katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwemo utoaji wa vitambulisho kwa wafanyabiashara wadogo;
xviii) Kuratibu na kusimamia uibuaji na utekelezaji wa miradi ya kimkakati katika Halmashauri zote nchini; na
xix) Kuratibu na kusimamia mkakati wa ujenzi na uanzishaji wa viwanda **100** kwa kila Mkoa.

**Tawala na Mikoa**

**137. Mheshimiwa Spika;** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Tawala za Mikoa zinazojumuisha Sekretarieti za Mikoa, Wilaya na Tarafa zitatekeleza shughuli zifuatazo:-

i) Kudumisha amani, utulivu na usalama;

ii) Kuratibu utoaji wa huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Sekta za Afya, Elimu na sekta nyingine;

iii) Kuendeleza ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa Ofisi na Makazi ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya na Maafisa Tarafa;

iv) Kuendelea kusimamia na kuimarisha Utawala Bora katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

v) Kuratibu Maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa ajili ya viongozi wa ngazi za msingi za Vijiji, Mitaa na Vitongoji utakaofanyika mwishoni mwa mwaka 2019;

vi) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kuhusu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi na Sera nyingine za kisekta ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi;

vii) Kuratibu, kusimamia na kutoa ushauri katika ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za kiuchumi na kijamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

viii) Kuratibu na kusimamia uibuaji na utekelezaji wa miradi ya kimkakati katika Halmashauri;

ix) Kuratibu na kusimamia shughuli za lishe katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

x) Kuziwezesha na kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake;

xi) Kuratibu Masuala Mtambuka yanayotekelezwa kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

xii) Kuratibu uanzishwaji wa viwanda na ushiriki wa sekta binafsi kwa kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara mijini na vijijini;

xiii) Kutatua migogoro inayotokana na matumizi ya ardhi na mipaka kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na
xiv) Kuratibu na kusimamia Mkakati wa ujenzi na uanzishaji wa viwanda 100 katika Mkoa.

**Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**138. Mheshimiwa Spika;** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i) Kusimamia utawala bora, amani na utulivu katika ngazi zote za Halmashauri;

ii) Kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Mwaka 2019;

iii) Kuendelea kuwawezesha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kutenga na kutoa mikopo kutokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri;

iv) Ukamilishaji wa miradi viporo ikiwemo majengo ya Ofisi na makazi ya viongozi na watumishi hasa katika maeneo mapya ya utawala;

v) Ujenzi, Ukarabati na ukamilishaji wa miundombinu ya kutolea huduma za kijamii na kiuchumi katika sekta zote husuan Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya, zahanati, maabara, nyumba za watumishi, matundu ya vyoo na vyumba vya madarasa;

vi) Kuendesha mikutano ya kisheria na kutekeleza maazimio ya vikao;

vii) Kusimamia rasilimaliwatu na fedha katika Halmashauri;

viii) Kubuni na kutekeleza miradi ya kimkakati itakayosaidia kuongeza mapato ya ndani ya Halmashauri ili kupunguza utegemezi;

ix) Kusimamia shughuli za lishe katika Halmashauri;

x) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa makusanyo katika vyanzo vya mapato;
xi) Kusimamia Mpango wa utoaji wa Elimumsingi Bila Ada katika Shule za Msingi na Sekondari;
xii) Kutenga maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya viwanda vidogo, vya kati na viwanda vikubwa na maeneo ya wafanyabiashara wadogo;
xiii) Kusimamia na kuwezesha uendeshaji wa ngazi za msingi na maeneo ya kutolea huduma katika Halmashauri;
xiv) Kuendelea kusimamia matumizi ya fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Mfuko;
xv) Kuratibu shughuli za usafi wa mazingira na utunzaji wa vyanzo vya maji;
xvi) Kusimamia na kuratibu shughuli za Mipango Miji na Matumizi ya Ardhi; na
xvii) Kubuni mikakati ya uanzishaji wa viwanda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**E. MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA OR-TAMISEMI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20**

**Tume ya Utumishi wa Walimu**

**139. *Mheshimiwa Spika;*** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Tume ya Utumishi wa Walimu imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-
i) Kutoa uamuzi wa mashauri ya nidhamu, rufaa na malalamiko ya Walimu kwa mujibu wa Sheria na kwa wakati;
ii) Kusimamia taaluma ya ualimu ili kuhakikisha uwepo wa Walimu wenye sifa na wenye kuleta tija na kuongeza ufanisi katika sekta ya elimu ili kutatua changamoto zinazolikabili Taifa;
iii) Kusimamia maadili na nidhamu kwa taaluma ya Ualimu kwa Shule za Msingi na Sekondari;
iv) Kuimarisha mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kusimamia masuala ya Walimu nchini; na
v) Kuratibu shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Tume Makao Makuu na Wilayani pamoja na kuendeleza rasilimali watu kwa kuwaongezea ujuzi na vitendea kazi.

**Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)**

**140. Mheshimiwa Spika;** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) utatekeleza shughuli zifuatazo:-
i) Kujenga uwezo wa Ofisi za Mikoa na Wilaya katika kutekeleza majukumu ya Wakala;
ii) Kufanya matengenezo ya kawaida **kilometa 13,098.61,** matengenezo ya maeneo korofi **kilometa 5,565.79,** matengenezo ya muda maalum **kilometa 2,860.64** na matengenezo ya makalvati madogo **2,403,** madaraja **113,** makalvati makubwa **273** na mifereji yenye urefu wa mita **82,627.81**.
iii) Kuhimiza Misingi ya Utawala Bora na Uwajibikaji kwa Makandarasi na Wafanyakazi wa TARURA;
iv) Kusimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za Wakala;
v) Kutunza mtandao wa barabara za Vijijini na Mijini ili zipitike kwa nyakati zote za mwaka;
vi) Kushiriki katika uhakiki wa mtandao wa barabara za Mijini na Vijijini;
vii) Kuendelea na matengenezo ya barabara za vijijini na mijini ili zipitike nyakati zote za mwaka kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara;
viii) Kusimamia utekelezaji wa kazi za ujenzi wa

# HOTUBA OFISI YA RAIS TAMISEMI

Barabara kwa Miradi ya Maendeleo kupitia Wadau wa Maendeleo (EU, DfID,USAID and Benki ya Dunia);

ix) Kushirikiana na Wadau wa Maendeleo kuwezesha matengenezo ya barabara za vijijini na mijini kulingana na miongozo inayotolewa;

x) Kufanya utafiti kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa mipango ya Wakala;

xi) Kuimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Matengenezo ya Barabara (DROMAS);

xii) Kuanzisha na kuendesha mizani ya barabara ili kudhibiti uzito wa magari katika barabara za vijijini na mijini;

xiii) Kuimarisha Mfumo wa Kudhibiti Matumizi ya Fedha katika Ofisi za Mikoa na Halmashauri; na

xiv) Kuimarisha Masuala Mtambuka katika maeneo yenye miradi ya ujenzi wa barabara kwa kutoa elimu ya Maambukizi ya Virusi vya Ukimwi, Rushwa, Jinsia, Watu Wenye Ulemavu, Vijana na Wazee, pamoja na Mazingira.

**Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam (DART)**

**141.Mheshimiwa Spika;** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka utatekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kushiriki katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya Awamu ya Pili inayotekelezwa kupitia Mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Ujenzi miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya Pili unahusisha barabara zenye urefu wa **kilometa 20.3** katika barabara za Kilwa, Kawawa, Sokoine, Gerezani, Bandari na Chang'ombe. Mradi huo utahusisha pia ujenzi wa barabara za juu (flyovers) katika makutano ya Chang'ombe na Uhasibu;

(ii) Kukamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi wa miundombinu ya mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya Tatu. Ujenzi wa miundombinu utahusisha barabara za Nyerere kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam hadi Gongo la Mboto, Bibi Titi na Mitaa ya Uhuru, Shaurimoyo, Lindi, Azikiwe na Maktaba.

(iii) Kufanya tathmini ya gharama za kuhamisha miundombinu ya kijamii na fidia kwa wananchi watakaopisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya Nne ambayo itahusisha ujenzi wa barabara za Bagamoyo hadi Tegeta, Bibi Titi, Ali Hassani Mwinyi na Sam Nujoma zenye urefu wa kilometa 25.9 na Awamu ya Tano itakayohusisha ujenzi wa barabara za Mandela kuanzia eneo la Ubungo kupitia TAZARA, Uhasibu kuungana na barabara ya daraja la Kigamboni na barabara ya kuanzia Tabata Relini hadi Segerea;

(iv) Ukamilishaji wa taratibu za ununuzi ili kumpata Mtoa Huduma kamili *(Service Provider-SP)* kwa Awamu ya Kwanza ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT). Mabasi yanayotarajiwa yatakuwa 305 na barabara za mlisho zitakuwa 11 ikilinganishwa na huduma ya mpito yenye mabasi 140 na barabara za mlisho mbili; na

(v) Kuendelea kusimamia kwa karibu Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato wa Serikali za Mitaa *(Local Government Revenue Collection Information System- LGRCIS)* katika ukusanyaji wa mapato kwa Awamu ya Kwanza.

**Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo**

**142.Mheshimiwa Spika;** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Chuo cha Serikali za Mitaa kitatekeleza shughuli zifuatazo:-

i) Kudahili wanafunzi wapya 5,000;

ii) Kuendeleza na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wa kozi za muda mrefu (kununua kompyuta 80 na vitabu 600) kutoa mafunzo ya muda mfupi yenye kuzingatia uhitaji;

iii) Kuanzisha kozi moja ya shahada ya Utawala na Menejimenti katika Serikali za Mitaa (Bachelor Degree in Local Government Administration and Management);

iv) Kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika masuala yanayohusu Mamlaka za Serikali za Mitaa;

v) Kutekeleza majukumu ya kuwa Chuo kiongozi cha mafunzo (Lead Training Institution) katika kusimamia ubora wa mafunzo yanayotolewa katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs);

vi) Kuendeleza watumishi katika ngazi mbalimbali za mafunzo;

vii) Usimamizi wa shughuli za uendeshaji wa Chuo;

viii) Kufanya mapitio ya Sera mbalimbali za Chuo ili ziendane na mazingira ya sasa mfano mitaala ya kufundishia na mafunzo na maendeleo ya watumishi.

ix) Kusimamia ukusanyaji wa mapato, matumizi na kudhibiti malimbikizo ya madai na madeni;

x) Ukarabati wa miundombinu ya Chuo na utunzaji wa mazingira yake;

xi) Ujenzi wa hostel ya wanafunzi wa kike yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200;

xii) Kuendelea na ujenzi wa ukumbi wa mihadhara (lecturer theatre) wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500;

xiii) Kuhamisha makaburi katika eneo la upanuzi wa Chuo,

xiv) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Chuo ikiwa ni pamoja na ununuzi wa kompyuta mpya 80; na

xv) Kupima na kufuatilia upatikanaji wa hati ya umiliki wa ardhi ya eneo la Chuo lenye ukubwa wa ekari **592** ikiwa ni pamoja na kurejea Michoro ya Mpango wa matumizi wa eneo hilo (Master Plan).

**Shirika la Elimu Kibaha**

**143.Mheshimiwa Spika;** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Shirika la Elimu Kibaha limepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i) Kuziwezesha shule zilizopo (Shule ya Chekechea moja, Shule ya Msingi moja na Shule za Sekondari tatu) kutoa elimu na malezi bora kwa wanafunzi **2,765** na kutoa huduma za maktaba kwa wadau **40,000;**

ii) Kuendelea kupambana na adui umaskini kwa kutoa elimu ya ufundi stadi kwa wanachuo **400,** kuendeleza shamba la ng'ombe wa maziwa na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau **400**; na

iii) Kupanua miundombinu ya Chuo cha Afya na Sayansi shirikishi kukidhi mahitaji ya utoaji wa mafunzo katika Chuo hicho.

**Shirika la Masoko Kariakoo**

**144.Mheshimiwa Spika;** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Shirika la Masoko Kariakoo litatekeleza shughuli zifuatazo:-

i) Kuboresha eneo la Mabucha lililoko ndani ya Jengo la Soko Kuu kwa kujenga maduka yapatayo hamsini na mbili (52);

ii) Kujenga maduka madogo yapatayo ishirini na mbili (22) eneo la Mtaa wa Tandamti;

iii) Kujenga Soko eneo la Mbezi Beach- Makonde;

iv) Kufanya ukarabati wa miundombinu ya Soko, Ofisi na nyumba za Shirika;

v) Kusimamia ukusanyaji wa mapato kwa kutumia Mfumo wa Kielektroniki na kubuni vyanzo vipya vya mapato pamoja na kuimarisha usimamizi wa matumizi ya rasilimali za Shirika;

vi) Kuboresha maslahi ya Watumishi ikiwemo kulipa stahiki za Watumishi kwa wakati;

vii) Kulipa madeni; na

viii) Kufanya uwekezaji wa ubia katika viwanja ambavyo vinamilikiwa na Shirika.

**Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

**145.Mheshimiwa Spika;** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i) Kupokea, kuchambua na kutoa mikopo kwa Halmashauri zitakazokidhi vigezo;

ii) Kuendelea kutoa mafunzo ya kuzijengea uwezo Halmashauri 84 kuandaa maandiko ya miradi bora inayokopesheka;

iii) Kuweka mkakati wa ufuatiliaji wa urejeshwaji wa mikopo na uwasilishwaji wa michango kutoka Halmashauri zinazodaiwa kwa lengo la kuongeza mtaji wa Bodi;

iv) Kubuni vyanzo vipya vya mapato; na

v) Kutoa elimu kwa wadau mbalimbali ili waweze kufahamu majukumu ya Bodi na huduma zinazotolewa.

**F. MALENGO MAHSUSI YALIYOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2019/20**

**146.Mheshimiwa Spika;** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza kazi maalum kama ifuatavyo:-

i) Kuanza ujenzi wa Hospitali mpya **27** za Halmashauri ambazo hazina Hospitali. Hospitali hizi zitajengwa katika Halmashauri za Karatu, Chalinze, Kondoa, Kongwa, Mbogwe, Biharamulo, Nsimbo, Kigoma, Kakonko, Liwale, Serengeti, Mbeya, Kilombero, Kaliua, Babati, Mvomero, Newala, Sengerema, Kwimba, Madaba, Msalala, Ikungi, Handeni, Mkinga, Halmashauri ya Mji wa Tunduma na Halmashauri za Manispaa za Sumbawanga na Tabora. Vilevile, Hospitali **67** za Halmashauri zilizoanza kujengwa katika mwaka wa fedha 2018/19 zitaendelea na ujenzi katika mwaka wa fedha 2019/20. Katika mwaka wa fedha 2019/20, zimetengwa **Shilingi bilioni 46.5** kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali hizo za Halmashauri (***Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 6);***

ii) Ujenzi wa Vituo vya Afya vipya **52** katika baadhi ya Kata ambazo hazina vituo ili kuboresha huduma za uzazi kwa kuboresha huduma za Mama na Mtoto na hali ya utoaji wa huduma za afya kwa ujumla. Katika mwaka wa fedha 2019/20, zimetengwa **Shilingi bilioni 10.40** kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo vya afya ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 7);***

iii) Kuendelea kutekeleza Mpango wa Utoaji Elimumsingi Bila Ada kwa Shule za Msingi na Shule za Sekondari hadi Kidato cha Nne. Katika mwaka wa fedha 2019/20, zimetengwa **Shilingi bilioni 288.47** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Ada. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 134.31** zimetengwa kwa Shule za Msingi ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.8)*** na **Shilingi bilioni 154.16** zimetengwa kwa Shule za Sekondari ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.9);***

iv) Ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba **364** za walimu katika Shule za Msingi. Katika mwaka wa fedha 2019/20, zimetengwa **Shilingi bilioni 9.10** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizo za walimu ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 10);***

v) Kupitia Mpango wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP) zitajengwa Shule za Sekondari **26** maalum za wasichana sawa na shule moja kila Mkoa. Ujenzi wa shule hizo utafanyika sambamba na ujenzi wa maktaba kwa kila shule. Aidha, yatanunuliwa magari **26** kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa shule hizo **26;**

vi) Kupitia Mpango wa Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R), kazi zituatazo zitatekelezwa:-

a) Ujenzi wa Vyumba **800** vya Madarasa ya Shule za Sekondari;

b) Ujenzi wa Mabweni **300** ya Shule za Sekondari;

c) Ujenzi wa matundu **1,000** ya vyoo ya Shule za Sekondari;

d) Ujenzi wa majengo **50** ya utawala ya Shule za Sekondari;

e) Ujenzi wa kumbi **200** kwenye Shule **100** za Sekondari;

f) Ukarabati wa Shule kongwe **15** za Sekondari;

g) Ununuzi wa vifaa maalum vya maabara katika Shule 70 za Sekondari;

h) Ununuzi wa magari **40** kwa ajili ya Halmashauri zenye mazingira magumu;

i) Ujenzi wa vyumba **1,200** vya madarasa ya Shule za Msingi,

j) Ujenzi wa matundu ya vyoo **2,000** katika Shule za Msingi;

k) Ujenzi wa mabweni **10** katika shule **10** za Elimu maalum;

vii) Kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala katika Halmashauri **62** zinazoendelea na ujenzi. Katika mwaka wa fedha 2019/20, zimetengwa **Shilingi bilioni 56.50** kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya utawala kwenye Halmashauri hizo ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 11);***

viii) Kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala

## HOTUBA OFISI YA RAIS TAMISEMI

katika Mikoa mitano (5) ambayo ni Simiyu, Katavi, Geita, Songwe na Njombe. Aidha, Mkoa wa Mbeya umetengewa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la utawala;

ix) Halmashauri kumi na tatu (13) za Wilaya ambazo ni Nsimbo, Kakonko, Mbogwe, Nyang'hwale, Kigoma, Mlele, Buhigwe, Busokelo, Gairo, Madaba, Bumbuli, Ileje na Mbulu zimepewa kipaumbele cha ununuzi wa magari ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2019/20;

x) Kuendelea na utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati katika Halmashauri zilizokidhi vigezo. Jumla ya **Shilingi bilioni 70** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 12);***

xi) Kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa **kilometa 21,525.04** na matengenezo ya makalvati madogo **2,403,** madaraja **113,** makalvati makubwa **273** na mifereji yenye urefu wa mita **82,627.81.** Jumla ya **Shilingi bilioni 224.94** zilimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo kupitia fedha za Mfuko wa Barabara (***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 13).***

xii) Vilevile, kwa mwaka wa fedha 2019/20, Mfuko wa Barabara umetengewa **Shilingi bilioni 22.44** kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami **kilometa 15.1,** ukarabati wa barabara za changarawe **kilometa 185.7** na ujenzi wa **madaraja 23** ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 14).***

xiii) Katika Mwaka wa Fedha 2019/20, jumla ya kilometa **25.69** za barabara zitajengwa kwa kiwango cha lami kupitia mradi wa DMDP pamoja na ununuzi wa vifaa vya kuzoa taka ngumu katika Manispaa za Ilala, Temeke na Kinondoni. Jumla ya **Shilingi bilioni 90.50** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi wa DMDP;

xiv) Kuendelea kutoa mikopo kwa vikundi vya Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu. Katika mwaka wa fedha 2019/20, zimetengwa **Shilingi bilioni 62.25** kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 15).***

### G. SHUKRANI

**147.*Mheshimiwa Spika;*** kabla ya kuhitimisha Hotuba yangu, natumia fursa hii kukushukuru sana wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi imara katika kutekeleza shughuli za Bunge. Vilevile, naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa inayoongozwa na Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, na Makamu wake Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kazi nzuri katika kusimamia utendaji wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

**148.*Mheshimiwa Spika;*** nichukue fursa hii pia kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa wanaoendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI katika kutekeleza mipango na programu mbalimbali katika kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Washirika hao wa Maendeleo ni pamoja na Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), Jumuiya ya Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Ubelgiji (BTC), *Global Partnership for Education,* Shirika la Maendeleo la Uingereza (DfID), Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi (UN-Habitat), UNEP, *CAMFED,* Africities, Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), *World Food Programme (WFP),* Nchi ya Sweden, Shirika la Mapinduzi ya Kijani Afrika (AGRA), Shirika la DALBERG na Nchi zote zinazochangia kupitia Mfuko wa Pamoja wa Kusaidia Bajeti ya Serikali. Ofisi ya Rais-TAMISEMI inaahidi kuendelea kushirikiana na Wadau mbalimbali wa Maendeleo katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI yaliyojikita katika kuboresha utoaji huduma za kijamii na kiuchumi ili kupunguza umaskini. Aidha, ninawashukuru Wananchi kwa mchango mkubwa katika utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mafanikio katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI yametokana na ushirikiano mzuri baina ya Wadau wa Maendeleo, Wananchi na Viongozi katika ngazi mbalimbali za usimamizi.

**149.*Mheshimiwa Spika;*** napenda kutambua mchango mkubwa wa Viongozi wenzangu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Kipekee nawashukuru Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege (Mb.) na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara (Mb.) kwa msaada mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Mhandisi Joseph M. Nyamhanga, Naibu Makatibu Wakuu Bw. Tixon T. Nzunda na Dkt. Dorothy O. Gwajima na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Bi. Winfrida Rutaindurwa. Aidha, nawashukuru Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Wakurugenzi wa OR-TAMISEMI na Wakurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

**150.*Mheshimiwa Spika;*** nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru Viongozi wenzangu katika Ofisi ya Rais wakiongozwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa George Huruma Mkuchika na Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais- Menjeimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais. Aidha, nawashukuru sana Dkt. Laurean Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Dkt. Francis Michael, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano wao.

**151.*Mheshimiwa Spika;*** kipekee nawashukuru wananchi wa Jimbo la Kisarawe kwa kunitia moyo katika utekelezaji wa majukumu haya ya Kitaifa. Ninawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, naishukuru familia yangu kwa uvumilivu muda wote nilipokuwa mbali nao katika utekelezaji wa majukumu haya ya Kitaifa.

### H. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20

**Maduhuli na Makusanyo ya Mapato ya Ndani**

**152.*Mheshimiwa Spika;*** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, OR - TAMISEMI, Taasisi zilizo chini yake, Mikoa 26 na Halmashauri 185 inaomba idhini ya kukusanya maduhuli na mapato ya ndani jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Nane na Mbili, Milioni Mia Moja Sitini, Mia Nne Tisini na Nane Elfu, Mia Moja Sitini na Nne (Shilingi 802,160,498,164.00).** Makusanyo hayo yatatokana na mauzo ya vifaa chakavu, nyaraka za zabuni, faini mbalimbali, ada za wanafunzi, marejesho ya masurufu na mishahara na kodi na ushuru mbalimbali unaotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Mchanganuo wa makusanyo ya mapato hayo ni kama ifuatavyo:-

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Maduhuli na Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/20**

| OFISI/TAASISI | MAKADIRIO |
|---|---|
| OR – TAMISEMI | 20,000,000.00 |
| Taasisi | 36,444,195,252.00 |
| Mikoa | 213,302,912.00 |
| Halmashauri | 765,483,000,000.00 |
| | **802,160,498,164.00** |

**153.*Mheshimiwa Spika*;** sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 jumla ya **Shilingi Trilioni Sita, Bilioni Mia Mbili na Saba, Milioni Mia Tisa Tisini na Mbili, Laki Saba na Sabini na Tisa, Mia Saba Sitini na Tisa (Shilingi 6,207,992,779,769.00)** kwa ajili ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI Fungu Na. 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Na. 02 na Mafungu 26 ya Mikoa yanayojumuisha Halmashauri 185. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na.2.**

**Jedwali Na.2: Muhtasari wa Makadirio ya Mpango na Bajeti ya OR – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2019/20**

| AINA YA MATUMIZI | FEDHA ZINAZOOMBWA |
|---|---|
| **OR - TAMISEMI** | |
| **Mishahara** | |
| Makao Makuu | 10,836,663,200.00 |
| Taasisi | 33,385,105,800.00 |
| **Jumla Mishahara** | **44,221,769,000.00** |
| | |
| **Matumizi Mengineyo** | |
| Makao Makuu | 7,896,530,195.00 |
| Taasisi | 1,318,870,805.00 |
| **Jumla Matumizi Mengineyo** | **9,215,401,000.00** |
| **JUMLA OR - TAMISEMI** | **53,437,170,000.00** |
| | |
| **Tume ya Utumishi wa Walimu** | |
| Mishahara | 9,899,012,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | 6,002,155,000.00 |
| **Jumla** | **15,901,167,000.00** |
| | |
| **MIKOA** | |
| Mishahara | 83,654,030,000.00 |
| Matumizi Mengineyo | 41,803,829,000.00 |
| **Jumla** | **125,457,859,000.00** |
| | |
| HALMASHAURI | |
| Mishahara | 3,669,329,614,000.00 |
| Matumizi Mengineyo (SK) | 190,390,615,000.00 |
| Mapato ya Ndani (OS) | 460,539,000,000.00 |
| **Jumla Ndogo** | |
| | |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | |
| OR - TAMISEMI | 463,563,123,910.00 |
| Mikoa | 67,333,480,032.00 |
| Halmashauri (SK) | 857,096,750,827.00 |
| Mapato ya ndani (OS) | 304,944,000,000.00 |
| **Jumla Miradi ya Maendeleo** | |
| **JUMLA KUU** | |

***SK –** Serikali Kuu **OS –** *Own Source*

**154.Mheshimiwa Spika,** pamoja na hotuba hii yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya OR-TAMISEMI, Taasisi, Mikoa na Halmashauri.

**155.Mheshimiwa Spika,** hotuba hii inapatikana pia kwenye Tovuti ya OR-TAMISEMI ambayo ni www.tamisemi.go.tz

**156.Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.





Balozi wa Yemen hapa nchini, Fikri Alsakf, akizungumza jijini Dar es Salaam mapema wiki hii, wakati wa harambee ya kuchangia fedha kwa watoto wa Yemen kutokana na machafuko yanayoendelea nchini humo, ambapo milioni 20 zilipatikana katika harambe hiyo. Kulia ni Sheikh Said Ahmed Abri. **PICHA: KHAMISI MUSSA**

# Wenye ulemavu kuandaa mpango kutambua changamoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BARAZA la taifa la watu wenye ulemavu limetakiwa kuandaa mpango mkakati ambao utahakikisha linatekeleza majukumu yake vizuri kuzitambua changamoto zote zinazowakabili watu wenye matatizo ya aina hiyo.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mihayo Juma Nhunga wakati akizungumza katika kongamano lililowahusisha maofisa na jamii ya watu wenye ulemavu kwa ajili ya kujenga mikakati na kuzipatia ufumbuzi changamoto zote.

Alisema Serikali imeanza kuzipatia ufumbuzi changamoto zote zinazowakabili watu wenye ulemavu, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa umoja wa mataifa wa malengo.

Alisema suala la ajira, tayari serikali imetoa agizo kuhakikisha kwamba wizara zote za serikali na taasisi zake kuona walemavu wenye sifa wanaajiriwa.

"Suala la ajira kwa watu wenye ulemavu tayari serikali imelipatia ufumbuzi wake.... lipo agizo la kuajiri walemavu wenye sifa katika taasisi za serikali"alisema

Naye Mkurugenzi wa watu wenye ulemavu Abeda Rashid Abdalla aliipongeza Serikali kwa kuanza kuzipatia ufumbuzi zinazowakabili watu wenye ulemavu ikiwamo ajira katika taasisi za Serikali na Wizara.

Alisema moja ya kikwazo kikubwa kilichokuwa kikiwakabili walemavu ni kushindwa kutambuliwa rasmi katika mfumo wa ajira ikiwamo serikalini na sekta binafsi.

"Walemavu tunaipongeza Serikali kwa kuanza kutekeleza baadhi ya maagizo yetu ikiwamo suala la ajira kwa watu wenye ulemavu"alisema.

Alieleza kazi kubwa inayofanywa kwa sasa ni idara ya walemavu ni kufanya usajili wa walemavu wote Unguja na Pemba kwa ajili ya kuwatambuwa mahitaji yao.

Alisema hadi sasa idadi kamili ya watu wenye ulemavu na mahitaji yao haifahamiki na hivyo inakuwa vigumu sana kutatua matatizo yao au kuwafikia na kuzipatia jibu changamoto zao.

"Kazi ya usajili wa walemavu wote Zanzibar imeanza ambayo hiyo ni muhimu itatusaidia kuweza kujua mahitaji yao kwa ujumla, " alisema.

# Serikali yaagiza idara ya Mufti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Katiba na Sheria imezitaka idara ya Mufti na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kufanya kazi kwa uadilifu katika kusimamia majukumu yao na kutatua migogoro mbalimbali inayotokea kwa mujibu wa sheria

Waziri wa wizara hiyo, Khamis Juma Mwalimu, aliyasema hayo wakati akizungumza na wafanyakazi wa ofisi ya mufti mkuu na kamisheni ya wakfu na mali amana.

Alisema migogoro isipotatuliwa mapema inaweza kusababisha uvunjifu wa amani hivyo Ofisi hizo zisiridhike na kupokea migogoro wakiwa maofisini bali wafanye ziara za mara kwa mara katika kukaguwa misikiti, madrasa pamoja na kuendeleza kutoa elimu ya ndoa ili kuthibiti wimbi la talaka.

Alisema migogoro hiyo ni vyema kuitatua kwa kutumia hekima na busara kwani migogoro huanza taratibu ni vyema kutatuliwa mapema badala kusubiri tatizo limeshakuwa kubwa.

Akizungumzia kuhusu suala la udhalilishaji kwa wanafunzi wa madrasa unaofanywa na baadhi ya walimu wasio waaminifu alieleza kuwa ni vyema kuwapo na taarifa za walimu hao ili kudhibiti udhalilishaji kwa kuchukuliwa hatua za kisheria.

"Wapo baadhi ya walimu wa madrasa wanaowadhalilisha watoto, huhama madrasa moja na huenda madrasa nyingine hivyo kama hawatodhibitiwa na huko wataenda kuwadhalilisha wengine"alisema.

Waziri huyo aliitaka Ofisi ya Mufti kuhakikisha inazisajili madrasa zote na walimu wanaofundisha katika madrasa ili kuwalinda watoto na udhalilishaji.

Aidha, aliipongeza ofisi hiyo kwa jitihada wanazozifanya katika kutoa elimu juu ya muongozo wa Madrasa na vipindi mbalimbali vinavyotayarishwa na Ofisi hiyo.

Hata hivyo aliwataka watendaji hao kutoridhika na kiwango cha elimu walichonacho na badala yake wajiendeleze kielimu zaidi.

Waziri huyo aliishauri kamisheni ya wakfu kufanyika kwa mapitio ya mara kwa mara na kuzihakiki mali za kamisheni hiyo ili ofisi iendelee kuwa na sifa ya usimamizi mzuri.

Aliitaka kamisheni hiyo kutowaonea haya na kutowafumbia macho wale wote ambao hawalipi ama wenye malimbikizo ya madeni iwe taasisi ama watu binafsi na walipe kwa mujibu wa utaratibu na mikataba waliojaza wakati wakipewa dhamana ya kuishi ama kusimamia .

Naye Mufti Mkuu wa Zanzibar Sheikh Omar Kaabi, alisema Ofisi yake inajukumu la kuratibu na kusimamia masuala ya dini ya kiislamu, kwa kutoa fatwa, miongozo na kulinda maadili mema.

Alieleza kuwa wanaendelea kutoa mafunzo kwa walimu wa madrasa juu ya kutumia muongozo kuhusu mbinu bora za kujenga nidhamu ya wanafunzi ili kupunguza na kuondosha kabisa vitendo vya udhalilishaji ikiwemo ubakaji na kupunguza adhabu kali wanazozitoa baadhi ya walimu kwa wanafunzi.

Kwa upande wake Kaimu Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Sheikh Ismail Asaakheir alisema kamisheni hiyo imejipanga vyema katika kuimarisha utoaji wa huduma za mirathi , ustawishaji wa mali za wakfu na amana pamoja na uratibu wa shughuli za Iddi , Hijja na misaada inayotolewa ili zikidhi mahitaji ya wakati tuliopo.

# RC awataka wanafunzi waache anasa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud, amewataka wanafunzi wa kidato cha sita na nne kuacha anasa na kufuatilia masomo yao kwani wanakabiliwa na mitihani ya taifa hivi karibuni.

Akizungumza na wazazi, wanafunzi wa kidato cha sita na nne na walimu, alisema kuwa wanafunzi hao wanakazi kubwa ya kushughulikia masomo yao ili kuweza kupata matokeo mazuri.

Mkuu wa Mkoa huyo aliwaahidi wanafunzi hao kwa atakaepata ufaulu wa daraja la kwanza atawazawadia zawadi mbalimbali ikiwemo lactop na fedha.

Alisema mikakati ya mkoa huo ni kuboresha kiwango cha elimu na kutokomeza ziro katika mitihani hiyo.

"Niwaahidi mwanafunzi atakaepata daraja la kwanza la ufaulu nitamzawadia laptop na shilingi laki mbili kila mmoja"alisema.

Alisema maendeleo ya elimu ya mkoa wake yataendelea kuimarika kila mwaka kwa lengo la kuyafikia matarajio yaliyokusudiwa ya kuongeza kiwango cha ufaulu katika mitihani ya taifa ya kidato cha nne na sita.

Amesema serikali ya mkoa wake imekuwa ikiendelea kufanya jitihada mbalimbali katika kuongeza kiwango cha ufaulu katika mitihani hiyo ya taifa na kwamba hata hivyo ukosefu wa ushirikiano kati ya wanafunzi, walimu na wazazi umekuwa ukirudisha nyuma juhudi hizo.

Alieleza kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964, ilitangaza elimu bila ya malipo ili kila mwananchi kuweza kupata elimu bila ya ubaguzi.

"Ni vyema wanafunzi mkafahamu kuwa dakika moja kwenu kwa sasa ni muhimu kwa mustakabi wa maisha yenu hivyo wakati huu si wa kushinda katika mitandao ya kijamii bali ni kuongeza juhudi katika kusoma," alisema Mkuu wa Mkoa huyo

Ayoub aliwapongeza wadau mbalimbali waliojitokeza katika kuunga mkono maendeleo ya elimu ili kuongeza kiwango cha matokeo mazuri katika mkoa huo.

Aidha, alipokea msaada wa chakula kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo kwa ajili ya wanafunzi hao wa kidato cha nne na sita ambapo kwa sasa wapo shule kwa muda wote.

Kwa upande wao wanafunzi hao, walimuahidi mkuu wa mkoa huyo kuwa watafanya vizuri katika mitihani yao ili kuongeza kiwango cha ufaulu.

Jumla ya wanafunzi 1648 kutoka shule za serikali na binafsi wanatarajiwa kufanya mtihani ya kidato cha sita ifikapo Mei mwaka huu.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 8 April**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 9 April**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 10 April**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 11 April**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 12 April**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 13 April**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Iljimae
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Night of terror
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 14 April**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Series rpt: Iljimae
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 8 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Kesho Leo
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 9 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 10 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Documentary
22:00 Kipindi Maalum: Tatu mzuka
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 11 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Elininyo
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Elininyo
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Sanaa na wasanii rpt
13:30 Kipindi Maalum: TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Riziki
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 12 April**
05:30 Uwanja wa Ma0zoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: Tanesco
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi rpt
13:45 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
13:55 Habari za saa
14:00 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Shamba shape up
19:00 Uchumi na biashara
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 13 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Elininyo
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 14 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Illegal sisters
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Illegal sisters 2
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)

## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

| TIME | MONDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

| TIME | TUESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | WEDNESDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | THURSDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | FRIDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

| TIME | SATURDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

| TIME | SUNDAY PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |


EATV
eNewz

**LEO JIONI SAA 12:00**

**ALHAMISI**
11:00 DADAZ (live)
12:00 Mpya
15:00 FUNGUKA
16:00 Bongo Hits
16:30 #HASHTAG
17:00 5SELEKT
17:55 Kurasa
18:00 eNewz
18:30 Music
19:00 EATV SAA 1
19:30 MJADALA
21:00 Bongo Hits



**eNewz** Kupata fununu, udaku na habari zote za mjini kuhusu wasanii na maisha yao, ulimwengu wa wasanaa, burudani na pia matukio yaliyotokea siku kama hiyo kwenye historia ya sanaa.

**eastafrica RADIO**
05:00 EA Breakfast
09:00 Supamix
12:00 Kipenga Xtra
13:00 Planet Bongo
16:00 EA Drive
20:00 Kipenga
21:00 The Cruise

**88.1FM DAR ES SALAAM**


## CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
## FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

## HABARI KIMATAIFA

## Waandamana kumpinga rais wa muda Algeria

**ALGIERS,** Algeria

JESHI la Polisi Algeria limetumia mabomu ya kutoa machozi kuwatawanya waandamanaji, hasa wanafunzi katika mji mkuu wa Algiers, ambao wamekuwa wakimpinga Rais wa muda aliyeteuliwa.

Tukio hilo limetokea ikiwa zimepita wiki saba tangu aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Abdelaziz Bouteflika kuachia madaraka.

Waandamanaji hao walijitokeza kufuatia wito wa muungano wa vyama vya wafanyakazi kuandamana ili kupinga kuchaguliwa kwa spika wa baraza dogo la bunge, Abdelkader Bensalah kuwa rais wa muda.

Vyama vya upinzani pia vinapinga kuchaguliwa kwa Bensalah, ambaye alikuwa mshauri wa karibu wa Rais Bouteflika, kufuatia kishinikizo la wananchi. Jana Rais wa muda Bensalah alilihutubia taifa na kuahidi kufanyika kwa uchaguzi wa huru na wa haki katika muda wa siku 90 na kuwataka watu kuacha maandamano.

Lakini wanafunzi wamekuwa wakiandamana huku wakipaza sauti zao wakisema: "hawajatusikia na tutaendelea kuandamana."

Wanafunzi, vyama vya kisiasa, pamoja na vyama vya wafanyakazi wanataka kuwapo na kipindi cha mpito kitakachofanya mageuzi makubwa ya utawala na kupanga uchaguzi ulio huru na haki. **VOA**

## Netanyahu njiani kutetea kiti chake

**JERUSALEM,** Israel

WAZIRI Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu anaelekea kuwa katika nafasi nzuri ya kupata ushindi wa muhula wa tano baada ya matokeo ya awali ya uchaguzi kuonyesha chama chake cha Likud kipo katika nafasi nzuri ya kupata ushindi na hivyo kuunda serikali ya mseto.

Hadi kufikia jana asilimia 97 ya kura zilikuwa zimeshahesabiwa huku chama chake kilionyesha kuwa na viti sawa na chama cha Blue na White kinachoongozwa na mkuu wa zamani wa jeshi, Benny Gantz.

Likud na washirika wake wanaweza kupata viti 65 katika bunge lenye viti 120. **VOA**

# Akutwa na nyuki wanne ndani ya jicho

**TAIPEI,** Taiwan

MWANAMKE mmoja nchini Taiwan amekutwa na nyuki wanne wa sukari waliokuwa wakiishi ndani ya jicho lake, tukio hilo ni la kwanza kutokea katika kisiwa hicho.

Mwanamke huyo mwenye umri wa miaka 28, aliyejulikana kama He, alikuwa aking'oa mizizi shambani, ndipo nyuki hao walipoingia katika macho yake.

Daktari wa Chuo Kikuu cha Hospitali ya Fooyin, Hong Chi Ting alisema kwamba alishangazwa wakati alipowatoa wadudu hao kwenye macho ya mwanamke huyo.

Inaelezwa kuwa He ameshatolewa hospitalini na anaendelea vizuri, kwa mujibu wa daktari amesema atapona.

Daktari Ting alisema kuna nyuki wanaovutiwa na jasho na mara nyingine huwarukia watu ili kunywa jasho. Pia hunywa machozi ili kujipatia protini kulingana na utafiti uliofanywa na chuo kikuu cha kansas kuhusu wadudu.

**Niliushika mguu huo na polepole nikamtoa nyuki mmoja na baadaye nikamuona mwengine na mwingine na mwingine na wote walikuwa wazima.**

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa He alikuwa akipalilia makaburi ya watu wa jamii yake wakati nyuki hao waliporuka na kuingia katika jicho lake la kushoto.

He alisema nyuki hao walimuingia wakati upepo ulipompiga usoni mwake akidhani kwamba ni uchafu uliokuwa umeingia machoni.

Alisema alikuwa akitembelea kaburi hilo kuadhimisha sherehe ya ufagiaji wa kaburi la Qing Ming ambayo huadhimishwa kwa kufagia makaburi ya watu unaowaependa.

Alisimulia kuwa lakini saa chache baadaye macho yake yalikuwa yamefura yakiwa na uchungu mwingi, suala lililomshinikiza kwenda hospitalini ili kupata matibabu kusini mwa Taiwan.

"Hakuweza kufunga jicho lake kabisa, niliatazama kwa kutumia darubini na kuona kitu cheusi kilichofanana na mguu wa mdudu," alisema Daktari Hong ambaye ni profesa aliyesomea magonjwa ya macho katika hospitali hiyo na kuongeza:

"Niliushika mguu huo na polepole nikamtoa nyuki mmoja na baadaye nikamuona mwengine na mwingine na mwingine na wote walikuwa wazima".

Picha za nyuki hao zilionyeshwa katika runinga ya Taiwan.

Dk. Hong aliongezea kuwa nyuki hao huenda walipeperushwa ndani ya jicho lake na upepo uliochanganyika na vumbi na kusalia ndani ya jicho la mwanamke huyo.

"Nyuki hawa huwa hawashambulii binadaamu lakini wanapenda kunywa jasho, hivyo basi ndio wakapewa jina hilo, aliongezea. He alikuwa na bahati kwamba hakufuta macho yake wakati nyuki hao walipoingia ndani. Alikuwa akivaliia miwani inayoshikana na macho hivyobasi kuweza kuharibu miwani hiyo. Iwapo angejaribu kujikuna jicho angewafanya wadudu hao kutoa sumu, pengine angekuwa kipofu," alisema Dk Hong.

Dk. Hong alisema nyuki hao bado ni wazima kwa sasa na watafanyiwa utafiti. **BBC**



Waandamanaji nchini Sudan wanaoupinga utawala wa Rais Omar Al- Bashir wakiwa wamekusanyika nje ya makao makuu ya jeshi mjini Khartoum, wakishinikiza Rais huyo kujiuzulu. **PICHA: AP**

# Polisi wapigwa 'Stop' kuwashambulia waandamanaji

**KHARTOUM,** Sudan

POLISI Sudan imewaamuru maafisa wake kutowashambulia maelfu ya waandamanaji waliopiga kambi nje ya makao makuu wa jeshi mjini Khartoum tangu Ijumaa, ambao wanamtaka Rais Omar Al Bashir ajiuzulu.

Awali milio ya risasi ilisikika nje ya makao ya jeshi na ripoti zinaeleza kuwa maaskari wanaotoa ulinzi kwa waandamanaji walipigwa risasi na maafisa wa serikali.

Katika taarifa iliyotolewa na msemaji wa polisi ilieleza kuwa: "Tunatoa amri kwa vikosi vyote visiingilie maandamano ya amani au kuwashambulia wananchi. Tunamuomba Mungu asaidie kuleta utulivu nchini mwetu... na kuwaunganisha Wasudani... na kufikiwa kwa makubaliano yatakayosaidia kupokezana madaraka kwa amani"

Waziri wa Mambo ya Ndani wa nchi hiyo alisema waandamanaji saba waliuawa siku ya Jumatatu na wengine 15 kujeruhiwa, huku maafisa 42 wa vikosi vya usalama nao wakijeruhiwa.

Mmoja wa wandamanani , Ahmed Mahmoud, alieleza kuwa maafisa wa kitaifa wa upelelezi walitumia mabomu ya kutoa machozi na risasi dhidi ya waandamanaji.

Alisema maaskari wamewatengea eneo salama waandamanaji karibu na makao makuu ya jeshi la taifa.

"Hakuna haja ya Omar Al-Bashir kututumia majangili wake kutuondoa barabarani, hatuendi popote," alisema.

Mwandamanaji mwingine alieleza kuwa sio kila mwanajeshi ana unga mkono vugu vugu la maandamano, na kwamba maafisa wa ngazi ya juu jeshini wanaunga mkono serikali iliyopo madarakani, huku wale wa ngazi ya chini wakiunga mkono waandamanaji.

Siku ya Jumatatu kuliibuka video inayowaonesha maafisa wakifyatua risasi kuelekea sehemu ambayo waandamanaji hao walikuwapo .

Kumekuwa na kauli kutoka nchi za Marekani, Uingereza na Noway za kuitaka serikali ya Sudan kutotumia nguvu dhidi ya raia.

"Ni vyema serikali ishughulikie matakwa ya wandamanaji kwa njia ya uwazi na uwajibikaji, Kutofanya hivyo kutasababisha machafuko. Mamlaka nchini Sudan ina jukumu la kuzuia matukio kama hayo," ilieleza taarifa yao.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), António Guterres, alitoa wito kwa pande zote mbili nchini Sudan kuwa na subira ili kuzuia kuzuka kwa machafuko. **BBC**

# Viongozi wapewa angalizo la rushwa

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imewataka viongozi wake waandamizi wanaohitimu mafunzo ya utawala yanayotolewa na Taasisi ya Uongozi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kifini cha Aalto kinachotoa mafunzo hayo cha nchini Finland, kuwa chachu ya kupambana na tatizo la rushwa katika taasisi za serikali.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjerwa, wakati akizungumza katika sherehe za mahafali ya pili ya stashahada ya uzamili ya uongozi kwa watumishi waandamizi wa serikali.

"Mmefundishwa mafunzo ya kiwango cha kimataifa na tunatarajia kwamba na nyie mkatende kazi kwa kiwango hicho cha kimataifa. Mmefundishwa namna bora ya kuajiri wafanyakazi, namna ya kuendeleza vipaji, mmefundishwa maadili na utawala bora na athari za rushwa katika kutekeleza majukumu yenu," alisema na kuongeza:

"Kama watumishi wa umma, tunataka kuona utumishi ulio bora wenye misingi imara na dhati ya kiuongozi, hatutegemei kuona mnaowaongoza wakipokea rushwa na mkawafumbia macho. Ninyi ndiyo mnapaswa kuwa chachu na mstari wa mbele wa mabadiliko kwa sababu mmepata mafunzo."

Pia Mwanjerwa alipongeza Taasisi ya Uongozi kwa kuanzisha programu hiyo ya uongozi na kwamba inaisaidia kwa kiwango kikubwa kuwaandaa viongozi wa serikali katika utendaji bora wa kazi zao za kila siku.

Mwanjerwa alisema kazi ya kuwaandaa viongozi na kuwajengea uwezo siyo nyepesi kwa sababu inahitaji wanataaluma wenye uwezo mkubwa, wenye weledi pamoja na rasilimali za kutosha kulifanikisha.

Aliwataka viongozi hao kufanya kazi kimkakati kwa kiwango cha kimataifa kinachoendana na aina ya mafunzo waliyoyapata kwa kuleta matokeo chanya kwa kuwatumikia wananchi na kuwa mabalozi na chachu ya utawala bora katika utendaji wao wa kazi wa kila siku.



Ofisa Elimu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Hamis Lissu (kulia), akimkabidhi fedha taslimu Sh. milioni 10 Mkurugenzi wa Chama cha Wajane Tanzania (TAWIA), Rose Sarwat, jana, kwa ajili ya kuwasaidia kutatua changamoto zilizokuwa zikiwakabili, ikiwa ni ahadi aliyoitoa Mkuu wa Mkoa huo, Paul Makonda. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Serikali yatoa mil. 750/- kukarabati karakana SUA

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imetoa Sh. milioni 750 kwa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kwa ajili ya kukarabati karakana za uhandisi kilimo ili kuwafanya wanafunzi kujifunza kwa vitendo na kuzalisha wataalamu watakatoa mchango wa kuendeleza sekta ya uchumi wa viwanda ikiwa ni sehemu ya kumuenzi hayati Edward Moringe Sokoine.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, wakati wa uzinduzi wa wiki ya kumbukizi ya aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania, hayati Edward Moringe Sokoine iliyofanyika katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo mjini Morogoro.

Dk. Akwilapo alisema kuwa fedha zitatolewa kutoka katika mradi wa kukuza ujuzi na stadi za kazi kupitia wizara hiyo ili SUA iweze kutoa mchango wake katika kusaidia mkakati wa serikali wa kufikia uchumi wa kati kupitia sekta ya viwanda ifakapo 2025.

Alisema kuwa lengo la kutoa fedha hizo kwa ajili ya ukarabati wa karakana hizo ni ziweze kuwa za kisasa, ili kuendana na sifa la jina la hayati Sokoine katika kutetea maslahi ya wanyonge pamoja na taifa kwa ujumla.

Alisema kuwa SUA ina jukumu kubwa la kuzalisha wataalamu wa sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi na kutoa elimu ya matumizi ya teknolojia za kilimo pamoja na mbegu bora ili kubadilisha kilimo kuwa cha kisasa zaidi na kuchangia katika pato la taifa.

Alisema kwa sasa bado kilimo kina mchango mdogo wa asilimia 3.3 na lengo la serikali ni kufikia zaidi ya asilimia nne ifikapo mwaka 2020 ili kukuza uchumi wa nchi.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu hicho, Profesa Raphael Chibunda, alisema SUA imekuwa ikiandaa kumbukizi hiyo toka mwaka 1992 na ya mwaka huu ni 16 ambayo inalenga kukuza uzalishaji katika kilimo na viwanda kama ilivyoainishwa katika programu ya maendeleo ya sekta ya kilimo na Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano awamu ya pili.

"Kumbukizi ya mwaka huu inahusu mada ambayo ni "Uzalishaji wa Kilimo na Viwanda kwa Maendeleo ya Tanzania, mambo ya kujifunza kutoka kwa hayati Sokoine na Matarajio ya siku zijazo," alisema Prof. Chibunda.

Mwakilishi wa familia ya hayati Sokoine, Edward Ole Ekalo, aliipongeza SUA na taasisi nyingine za serikali kwa kumuenzi kwa vitendo waasisi wa taifa la Tanzania akiwamo hayati Sokoine.

Ele Ekalo alisema familia ya Sokoine inaunga mkono kwa dhati juhudi zinazofanywa na serikali ya awamu ya tano na inaamini Tanzania yenye neema inakuja na kuvishauri vyuo vikuu nchini kuandika machapisho yanayoelezea historia ya viongozi mbalimbali ili yaweze kutumiwa na vizazi vya sasa na vijavyo.

## Agizo vigogo wakamatwe

**Na Anthony Gervas,** MARA

MKUU wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa mkoani Mara (Takukuru), kuwakamata Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, akiwamo aliyewahi kuwa mweka hazina aliyehamishwa, wakikabiliwa na tuhuma za ubadhirifu wa Sh. bilioni 1.035.

Malima alitoa agizo hilo juzi katika kikao cha Baraza la Kamati ya Usalama wilayani Tarime kilichowashirikisha madiwani na watendaji wa halmashauri ya wilaya hiyo, aliwakabidhi watuhumiwa hao mikononi mwa Takukuru, ili washikiliwe na kuchunguzwa tuhuma hizo.

Alisema watuhumiwa hao ni pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Apoo Tindwa, akiwamo Mweka Hazina aliyehama, Julius Ndyanabo, Ofisa Mifugo aliyewahi kukaimu nafasi ya ukurugenzi, Dk. Peter Nyanja, pamoja na Ofisa Mipango, Samwel Magige.

Wengine wanaohusika na sakata hilo ni pamoja na aliyewahi kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Athumani Akalama, ambaye alibadilishwa kazi na kuhamishwa pamoja na Pentaleo Rwiza, aliyewahi kuwa Ofisa Elimu Sekondari, ambaye alishastaafu.

"Nawaagiza Takukuru Mkoa kuanzia sasa hivi Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hii Apoo Tindwa, akiwamo aliyekuwa mweka hazina, Julius Ndyanabo, ofisa mifugo Dk. Peter Nyanja, afisa mipango Samwel Magige, wakamatwe kwa upotevu wa fedha hizo Sh. bilioni 1.035 ambazo hazijathibitika katika matumizi yake," alisema.

"Wengine ni Athumani Akalama, aliyewahi kuwa mkurugenzi mtendaji wa halmashauri ya wilaya hii akahamishwa, wakamatwe na washikiliwe kwa uchunguzi na wasimamishwe kazi wote wanaotuhumiwa, siwezi kukubali upotevu wa fedha za miradi ya maendeleo ya wananchi," Malima alisema.

Aidha, mkuu huyo wa mkoa aliitupia lawama kamati ya fedha iliyokuwa ikihusika kugawa fedha za miradi ya maendeleo kwa kila kata, ambayo ilishindwa kutenda haki na kugawa baadhi ya kata mamilioni ya shilingi, huku akimtaka mkaguzi wa ndani naye achukuliwe hatua za kisheria.

Alidai vigogo hao wametafuna fedha hizo ambazo ni makusanyo yanayotokana na vyanzo vya mapato ya ndani ya miaka mitatu na nusu kuanzia Julai 1, 2015 hadi Desemba 31, 2018, yakiwamo makusanyo ya sehemu ya mgodi wa North Mara (ACACIA).

Aidha, kubainika kwa ubadhirifu wa fedha hizo kumetokana na kamati ya mkoa ya ukaguzi wa kina iliyoundwa kuchunguza fedha za mapato na matumizi ya ndani ya halmashauri ya wilaya hiyo, chini ya mwenyekiti wake, Dotto Nenetwa.

Awali akisoma taarifa ya uchunguzi huo, katibu wa kamati hiyo, Okayo Chacha, alibainisha kuwa fedha zilizohujumiwa ni makusanyo ya ndani ya miaka mitatu na nusu toka Julai 1, 2015 hadi Desemba 31, 2018 na kamati hiyo ilikagua mapato ya ndani ya Sh. bilioni 18.2.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## VIWANJA/MASHAMBA

**VIWANJA VILIVYOPIMWA VINAUZWA** KWA BEI NAFUU Viwanja vilivyopimwa na mashamba vinavyofikika kwa urahisi. Vipo Kimbiji karibu na kwa Charle na Morris. Piga simu namba 0652 876 085 au 0745 665 955.

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA

## KUPOTEA KWA CHETI



**Issack Charles Kihwele** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0385-0171** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2015 katika shule ya Sekondari Ujiji.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**KGT/RB/5156/18**

115169002

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**NDG. WILGOD ABRAHAM** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA BLUE KADI YA GARI YAKE YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 602 CDD**, AINA YA TOYOTA PRIMIER, RANGI YA SILVER. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ANAOMBWA ARIPOTI KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. RIPOTI YA POLISI: **SMT/RB/540/2019.**

115170102

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**JUDICA GODFRAY UROKI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 331 DET** Aina yake **TOYOTA** IPSUM.Yenye chasis namba **ACM210056500** na injini namba **2AZ5212098.**

Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi,

Taarifa ya Polisi:
**MOR/TR/RB/217/2019.**

115170302

## KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

**YUSUPHU M.MUSHEHE**

anatangaza kupotelewa na kadi pikipiki yenye namba za usajili **T 746 BUG. Aina yake SANLG.**

**Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi,**

**Taarifa ya Polisi:**
**MOR/RB/12287/2017.**

215168602

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**Aloyce Robert Assenga** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA LAND CRUISER** yenye namba za usajili T 984 ADA Chassis No. BJ6022255,

Engine No. 3B1028545
Yenye rangi NYEUPE.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa Polisi.

Taarifa ya Polisi:
MOS/TR/RB/334/2019

215169402

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu:+255 26 2324455
Fax: +255 26 232233
Barua Pepe ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

## TANGAZO


1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Alhamis tarehe 11-04-2019 kampuni ya **SIMBA LOGISTICS EQUIPMENT SUPPLY LIMITED.** itasafirisha Mizigo yake yenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea MTWARA** kupitia **NANGURUKURU,** gari hilo lenye namba za usajili:1.
   **1.T 181 DNC/ T254 DMW**
   **2.T915 DGZ/T145 DMU**
   **3.T230 DET/T237 BEL**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu - mita 18.00
   Upana - mita 4.00
   Kimo - mita 4.60
   Gari zitasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215170402

## KUPOTEA KWA VYETI



**JACKLINE JOHN** amepotelewa na vyeti vya elimu ya kidato cha nne alivyosomea ktk shule ya **KENI SECONDARI SCHOOL,** alichomaliza mwaka 2011 na chenye **index namba S3101-0023.** Na cheti cha kurudia elimu ya kidato cha nne alichosomea ktk shule ya HIGH **SCORE TRAINING CENTRE**, alichomaliza mwaka 2013 na chenye **index namba P.4450/0007.**

**Kwa yeyote atakae viona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.**

**Taarifa ya polisi;**
**TAB/RB/962/2019.**

115169802


## KUPOTEA KWA VYETI



**JACKLINE JOHN** amepotelewa na vyeti vya elimu ya kidato cha nne alivyosomea ktk shule ya **KENI SECONDARI SCHOOL,** alichomaliza mwaka 2011 na chenye **index namba S3101-0023.** Na cheti cha kurudia elimu ya kidato cha nne alichosomea ktk shule ya HIGH **SCORE TRAINING CENTRE**, alichomaliza mwaka 2013 na chenye **index namba P.4450/0007.**

**Kwa yeyote atakae viona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.**

**Taarifa ya polisi;**
**TAB/RB/962/2019.**

115169802


*Kwa matangazo, madogo madogo,*

*Tupigie 0767 223311*

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# KANE KUMALIZIA MSIMU HUU BENCHI




**LONDON,** England

NYOTA wa Tottenham, Harry Kane, huenda akaukosa msimu mzima uliosalia wa Ligi Kuu ya England kutokana na kupata majeraha hapo juzi kwenye mchezo wa robo fainali ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester City.

Tottenham katika mchezo huo iliibuka na ushindi wa bao 1-0 na kujiweka kwenye nafasi nzuri kuelekea mchezo wa pili.

Kocha Mauricio Pochettino ameingiwa na hofu ya kukosekana kwa nyota wake huyo kwa msimu huu unaoelekea mwishoni.

Nahodha huyo wa Timu ya Taifa ya England alipata majeraha baada ya kukanyagwa kwenye kifundo cha mguu kupitia beki wa kushoto wa Man City, Fabian Delph, mwanzoni mwa kipindi cha pili kwenye mchezo huo wa robo fainali.

Alipoulizwa kuhusu, Kane kama atakuwa nje kwa kipindi chote cha msimu, Mauricio Pochettino, alisema, "Tunahitaji kuangalia hilo kesho, lakini inavyoonekana na matatizo yanayofanana."

"Najisikia vibaya, na kukatishwa tamaa na tutakuwa kwenye wakati mgumu kwenye kipindi hiki cha mwishoni mwa msimu.

"Ni imani yetu si tatizo kubwa, lakini itachukua muda kurudi kwenye hali yake ya kawaida."

Majeraha ya kifundo cha mguu aliyopata Kane safari hii, siyo kama aliyopata dhidi ya Manchester United Januari 13 ambayo yalimuweka nje ya uwanja kwa zaidi ya mwezi mmoja.



# Klopp amhofia nyota wa Porto

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesisitiza kwamba atalazimika kumtazama kwa jicho la ziada mshambuliaji wa Porto, Moussa Marega wakati watakaposafiri kwenda Ureno kwenye mchezo wa marudiano wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

'Wekundu' hao waliibuka na ushindi wa mabao 2-0 kwenye dimba la Anfield Jumanne usiku kwa mabao ya kipindi cha kwanza kutoka kwa Naby Keita na Roberto Firmino.

Marega alionekana kuwa mwiba zaidi kwa safu ya ulinzi ya Liverpool wakati alipopiga mashuti kadhaa yaliyookolewa na golikipa, Alisson.

Licha ya ushindi huo, Klopp amesema kwamba mshambuliaji huyo wa Porto mwenye umri wa miaka 27 anatakiwa kutazamwa kwa jicho la ziada.

"Tulilazimika kulinda mipira kadhaa na yeye alikuwa ndio tishio kubwa zaidi kwetu. Ukimuangalia mshambuliaji kama Marega ni hatari zaidi.

"Alikuwa nyota kwao, naamini mchezo ujao nchini Ureno utakuwa mgumu na yeye ndio mtu wa kumchunga zaidi."

## Arsenal, Spurs vitani kwa Perisic



**LONDON,** England

WAPINZANI wa Kaskazini mwa London, Arsenal na Tottenham wanaweza kuingia kwenye vita wakati wa usajili wa dirisha la kipindi cha majira ya joto, kwa kuwa zote zinamwania mshambuliaji wa Inter, Ivan Perisic.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 raia wa Croatia amekuwa akihusishwa na mpango wa kwenda kwenye Ligi Kuu ya England, huku Manchester United chini ya Jose Mourinho ilikuwa ya kwanza kumuwania kipindi cha majira ya joto mwaka 2017, kabla ya Arsenal na Spurs kuingia kwenye mbio hizo Januari.

Wakati usajili wa mkopo ulishindwa kufanyika wakati wa kipindi cha baridi, lakini sasa Perisic ni wazi kwamba anataka kundoka na kuelekea nchini England.

Kwa mujibu wa Gazeti la Corriere dello Sport, limedai kwamba Arsenal na Spurs wameingia kwenye vita ya kutaka kumsajili mshambuliaji huyo.

Inter, kwa sasa ipo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, ikiwania nafasi ya kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Perisic alituma maombi ya kutaka kuondoka Januari, lakini Arsenal na Spurs walishindwa kufika bei na matokeo yake akabakia hapo San Siro, ambapo amefunga mabao matatu kwenye mechi 27 msimu huu.

# MAKOCHA SOUTHAMPTON KUWANOA 40 WA BONGO



**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha soka la Tanzania linakua, Kampuni ya Michezo ya Kubashiri ya SportPesa imethibitisha kuwaleta makocha kutoka Klabu ya Southampton ya Uingereza ili kuja kuwanoa makocha wazawa na kuwaongezea ujuzi maradufu.

SportPesa wataendesha kliniki hizo kupitia washirika wao wa kimataifa, wa klabu za Arsenal, Southampton na Hull City chini ya mwamvuli wa kampeni yao inayokwenda kwa jina la "Coaches To Count On".

Kliniki hiyo ya siku mbili itafanyika katika nchi tatu tofauti barani Afrika ambazo ni Afrika Kusini, Tanzania na Kenya, zikiendeshwa na makocha hao wenye uzoefu wa hali ya juu.

Akizungumza kuhusu ujio huo, Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa Kampuni ya SportPesa, Tarimba Abbas (pichani), alisema kwa upande wa Tanzania, kliniki hiyo itaendeshwa kuanzia Mei Mosi hadi Mei 2, mwaka huu, katika Uwanja wa Taifa ikiongozwa na jopo la makocha kutoka Klabu ya Southampton ambao ni washirika wa Kampuni ya SportPesa inayoongoza kwa michezo ya kubashiri barani Afrika.

"Kliniki hiyo itahudhuriwa na makocha 40 kutoka Tanzania ambao watachaguliwa na Shirikisho la Soka nchini (TFF), kutoka kote nchini, ambapo watakaopata nafasi ya kuhudhuria kliniki hiyo ni wale wenye leseni za Caf Daraja A, B na C huku wakifundishwa na mkufunzi mwenye leseni ya Uefa Daraja A.

"Huu utakuwa ni mwendelezo wa jitihada tunazozifanya SportPesa za kuleta maendeleo ya soka kwa wadau mbalimbali wa mchezo huo pendwa barani Afrika na duniani kote," alisema Tarimba.

Mbali na kliniki za makocha, SportPesa pia imewahi kufanya kliniki na wachezaji wa timu za vijana za Simba na Yanga ambazo zilisimamiwa na makocha kutoka Klabu ya Everton, mara ya mwisho klabu hiyo ilipofanya ziara nchini Tanzania Julai 2017.

Ukiachilia mbali nchini Tanzania, SportPesa pia imeshafanya kliniki za wachezaji vijana nchini Kenya Aprili 2017 kwa kuwaleta makocha kutoka Klabu ya Southampton bila kusahau kliniki zilizofanyika Mei mwaka jana nchini Kenya, pia wakati jopo zima la timu ya Hull City lilipotembelea nchini humo.

## TFF ilivyoibana Arusha United

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limesema lililazimika kutokubali uamuzi wa kujitoa kwa timu ya Arusha United kwenye Ligi Daraja la Kwanza kwa sababu uamuzi huo ulikuwa unaua mchezo wa soka.


Kwa sasa timu hiyo ambayo ilinunuliwa na wadau wa soka wa Jiji la Arusha, imerejeshwa kwa mmiliki wake wa awali ambaye ni JKT Oljoro na inaendelea na ligi hiyo.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Rais wa TFF, Wallace Karia, aliwaomba wachezaji wote waliosajiliwa na timu hiyo kuendelea kuitumikia mpaka mwishoni mwa msimu na atakayegoma atajiweka kwenye nafasi mbaya.

Karia alisema kilichopo kwa sasa ni mabadiliko ya uongozi na wachezaji wa timu hiyo wanatakiwa kuendelea kuitumikia mpaka mwishoni mwa msimu.

"Maombi hayakuwa halali, yalikuwa yanalenga kuua mpira, tuliwakatalia, na wameikabidhi timu kwa wenyewe, walikoichukua... napenda kuwaambia wachezaji wa Arusha United kumaliza msimu wao, atakayekataa kucheza, atajiweza pabaya katika hatima ya kipaji chake," alisema Karia.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi, Stephen Mnguto, alisema wanafahamu kuwa ligi hiyo ina changamoto mbalimbali, lakini kubwa ikiwa ni kukosa fedha za kujiendesha.



# *Rashford akaribia kusaini mkataba mpya Man Utd*

**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Marcus Rashford, ameanza mazungumzo kwa ajili ya mkataba mpya hapo Old Trafford, ambao utamfanya kulipwa kiasi kikubwa cha fedha kama Wayne Rooney kabla hajaondoka mwaka 2017.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, amefurahia msimu wake bora zaidi hapo United, akifunga mabao 13 katika mashindano yote na amekuwa nguzo ya kocha, Ole Gunnar Solskjaer.

Rashford amefunga katika mechi zake mbili za mwisho na alifunga penalti iliyoiondoa Paris Saint-Germain na kuipeleka United kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, licha ya kiwango chake hicho bora katika klabu yake hiyo ya nyumbani, Rashford amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Real Madrid na Barcelona, huku mkataba wake wa sasa pale Man Utd unamalizika mwaka 2020.

Gazeti la The Mirror sasa limeripoti kwamba, Rashford anakaribia kusaini mkataba mpya wenye thamani ya pauni milioni 78 ambao utakuwa ni wa miaka mitano na atakuwa akilipwa pauni 300 kwa wiki.

DO DO SOKA
M AZE LAYA



# GUARDIOLA: KUPOTEZA 1-0 NI BORA KULIKO 0-0

●●● Unajua dhahiri nini unatakiwa kufanya, unakwenda kushambulia ama kuzuia, lakini...

**LONDON,** England

PEP Guardiola amesema Manchester City kupoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Tottenham kunaweza kuthibitisha kuwa bora zaidi kuliko wangetoka sare tasa kwenye mechi yao ya mkondo wa kwanza ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, kama kikosi chake "kinajua nini kinapaswa kufanya" ili kusonga mbele.

Bao la kipindi cha pili kupitia kwa Heung-Min Son, linaiweka Tottenham katika nafasi nzuri, huku mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu England wakiondoka kaskazini mwa London bila bao la ugenini, hivyo kujenga matumaini katika mechi ya marudiano Jumatano ijayo.

Lakini Guardiola alisema: "Inatuacha katika hali hii kwenye mechi ya marudiano, ila mara nyingine 1-0 inaweza kuwa bora kuliko 0-0 kwa sababu unajua dhahiri nini unatakiwa kufanya.

**"Kwa 0-0, unajua kama unakwenda kushambulia ama kuzuia, lakini tuna jua tunapaswa kufunga mabao. Tutachambua matokeo, lakini kwa sasa ninajisikia vizuri kuhusu namna tulivyocheza - tulitawala mchezo na pengine wiki ijayo hilo litakwenda kufanya kazi."**

Kikosi hicho cha Guardiola kilimudu kupiga shuti moja tu lililolenga goli mbali ya penalti yao iliyookolewa na kipa Hugo Lloris katika dakika ya 13, lakini kocha huyo wa City, anatazama katika kutwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya tatu akiwa kocha, akisema bado walikuwa bora zaidi. Alisema: "Kuna nafasi chache ambazo waliruhusu, baadhi ya mashambulizi ya kushtukiza, lakini tulitawala mchezo, tulicheza vizuri sana. Tutaona katika mchezo ujao namna gani tunajaribu kulibadili hilo na wachezaji wetu, mashabiki na familia nyumbani.

"Kama hatukucheza vizuri nitalizungumza hilo, lakini sikuwa na hisia hiyo. Mara nyingi, vipindi vyote, tulikuwa timu iliyojipanga vizuri, kugusa sana, hawakulifanya hilo.

"Tuliwaona wachezaji wetu katika nafasi hizo, lakini katika robo ya mwisho na zaidi katika kipindi cha pili, tuliingia ndani ya boksi ila wao waliweza mara moja- na ubora waliokuwa nao walifunga kutokana na nafasi hiyo."

## ZISIKUPITE

### KUJIFUNGA KWA MIL.78

STRAIKA wa Manchester United na England, Marcus Rashford, 21, anakaribia kusaini mkataba mpya na klabu hiyo wenye thamani ya pauni milioni 78. ***(Mirror)***

### AWANIWA SPURS, ARSENAL

ARSENAL na Tottenham zote zinavutiwa kumsajili kiungo wa Inter Milan na Croatia, Ivan Perisic, 30. ***(Corriere dello Sport, via Sport Witness)***

### CONTE ATOA MASHARTI INTER

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Antonio Conte yupo tayari kuwa kocha mpya wa Inter Milan - kama klabu hiyo itamfanya Mtaliano huyo kuwa kocha anayelipwa zaidi Serie A. ***(Mail)***

### ALDERWEIRELD BADO LULU UTD

MANCHESTER United ipo tayari kufika dau la pauni milioni 25 zinazohitajika ili kuvunja mkataba wa beki Mbelgiji Toby Alderweireld na Tottenham, lakini bado haijafanya mawasiliano kuhusu mpango huo. ***(Sun)***

### NEVES AMKUNA KOCHA LIVER

LIVERPOOL inavutiwa na kiungo wa Wolves na Ureno, Ruben Neves. Kocha msaidizi wa Liverpool, Pep Lijnders amesema ameona "ufundi na utaalamu" kwa mchezaji huyo. ***(O Jogo - in Portuguese)***

### ATABIRIWA KUTUA JUVENTUS

JUVENTUS inaonekana kuwa sehemu sahihi kwa kiungo wa Real Madrid, Mcolombia James Rodriguez, 27, kutokana na mshambuliaji wa Chelsea, Eden Hazard kuwa na uwezekano wa kutua Bernabeu. ***(Marca)***

### HAZARD KUKATAA MKATABA

NYOTA wa kimataifa wa Ubelgiji, Eden Hazard, 28, atakataa kusaini mkataba mpya na Chelsea, hata kama klabu hiyo itaamua kuingia vitani na Real. ***(Telegraph)***

### BALE HANA MPANGO NA EPL

WAKALA wa Gareth Bale, amesema mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales mwenye umri wa miaka 29 kwa sasa, ni mwenye furaha hapo Real Madrid na kwamba winga huyo hana mpango wa kurudi Ligi Kuu England, EPL. ***(Mirror)***

### KUMPELEKA POGBA MADRID

REAL Madrid inaweza kufunga safari kwenda kumsajili kiungo Mfaransa Paul Pogba, 26, kama Manchester United haitafuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya na kurudi kwenye Europa League. ***(Sun)***

### OBLAK KUFUNGWA UPYA

ATLETICO Madrid inamatumaini ya kutangaza dili mpya na kipa Jan Oblak, 26. Kipa huyo wa kimataifa wa Slovenia atawekewa kipengele kitakachomruhusu kuvunja mkataba wake kwa euro milioni 100, na inadhaniwa lengo ni kuizuia Manchester United ambayo imemuweka katika orodha yake ya kuziba pengo la Mhispania David de Gea, 28, anayewindwa na Real Madrid. ***(Marca)***

### WACHEZAJI UTD KUKATWA 25%

WACHEZAJI wa Manchester United watakatwa asilimia 25 kwenye malipo yao, endapo hawatafuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. ***(Sun)***

## HABARI MICHEZO

# JKU mawazo yote ubingwa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya JKU inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, imesema inatamani kutwaa ubingwa wa ligi hiyo wa msimu huu ambayo inaelekea ukingoni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Hassan Ramadhani, alisema kuwa licha ya kuwapo kwa ushindani kwenye ligi hiyo, kikosi chake kimejiandaa kupambana mpaka mechi yao ya mwisho.

Ramadhani alisema timu yake imebakiza mechi sita ili kukamilisha msimu huu na anaamini wanaweza kunyakua ubingwa wa ligi hiyo kama hawatapoteza mchezo hata mmoja.

"Tunatamani kunyakuwa ubingwa wa msimu huu ili kukamilisha ndoto yetu ambayo tulijiwekea tangu mwanzo mwa msimu, na hatuoni sababu ya kuukosa ubingwa wa msimu huu," alisema Ramadhani.

Kocha huyo aliongeza kuwa ushindani uliopo katika kila mechi unasaidia kuwajenga wachezaji wake ambao anawakumbusha kujituma kwa sababu wanatofautiana pointi chache kati ya timu moja na nyingine.

"Tunajituma kwa hali ya juu ili kuhakikisha michezo yetu sita iliyobakia tunapambana na kutopoteza hata mchezo mmoja, hii itatufanya tujihakikishie kwa asilimia kubwa kutangazwa mabingwa," alisema kocha huyo.

Maafande hao wa JKU ambao wana pointi 67, wako katika nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo yenye timu 19, wakati vinara ni KVZ wenye pointi 70.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 30 | 22 | 5 | 3 | 48 | 20 | 71 |
| 2. Azam | 30 | 18 | 9 | 3 | 48 | 18 | 63 |
| 3. Simba | 22 | 18 | 3 | 1 | 48 | 7 | 57 |
| 4. Lipuli | 33 | 12 | 12 | 9 | 30 | 28 | 48 |
| 5. Mtibwa Sugar | 31 | 13 | 6 | 12 | 32 | 24 | 45 |
| 6. TZ Prisons | 32 | 10 | 12 | 10 | 26 | 25 | 42 |
| 7. Kinondoni MC | 31 | 9 | 14 | 8 | 32 | 23 | 41 |
| 8. Coastal Union | 32 | 9 | 14 | 9 | 28 | 31 | 41 |
| 9. JKT Tanzania | 32 | 9 | 12 | 11 | 19 | 26 | 39 |
| 10. Singida United | 32 | 10 | 9 | 13 | 24 | 32 | 39 |
| 11. Ndanda | 30 | 10 | 9 | 11 | 20 | 29 | 39 |
| 12. Stand Utd | 33 | 11 | 6 | 16 | 30 | 41 | 39 |
| 13. Mbeya City | 30 | 10 | 7 | 13 | 30 | 33 | 37 |
| 14. Mwadui | 33 | 10 | 7 | 16 | 37 | 43 | 37 |
| 15. Alliance | 32 | 9 | 10 | 13 | 23 | 33 | 37 |
| 16. Mbao | 33 | 9 | 10 | 14 | 19 | 33 | 37 |
| 17. Kagera Sugar | 30 | 8 | 12 | 10 | 24 | 29 | 36 |
| 18. Ruvu Shooting | 33 | 8 | 12 | 13 | 28 | 39 | 36 |
| 19. Biashara Utd | 31 | 8 | 10 | 13 | 22 | 29 | 34 |
| 20. African Lyon | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |

# SERENGETI BOYS HAKUNA 'KIJEBA', KARIA AFUNGUKA

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, amesema hana wasiwasi na umri wa wachezaji wanaounda kikosi cha Serengeti Boys kwa sababu waliwafanyia vipimo mapema ili kujiridhisha.

Serengeti Boys na timu nyingine saba zinazotarajia kuchuana kuwania ubingwa wa Afrika wa vijana wa umri chini ya miaka 17 (Afcon U-17), wanaendelea kufanyiwa vipimo vya kubaini umri sahihi na jopo la madaktari wa Shirikisho la Soka Afrika (Caf).

Karia alisema jana kuwa kabla ya kikosi cha Serengeti Boys kwenda Uturuki kujifua, waliwafanyia vipimo wachezaji wote na waliobakia ni wale ambao wanaruhusiwa kushiriki michuano hiyo.

**"Tulifanya vipimo wenyewe kwa tahadhari, ila vipimo bado vimekuwa na changamoto, hiyo inatokana na maumbile ya baadhi ya wachezaji, kama ambavyo kuna timu yenye wachezaji mapacha, mmoja amepita na mwenzake ameonekana mkubwa, kwa upande wetu wachezaji wako salama," alisema Karia.**

Kiongozi huyo alisema pia anamshukuru Rais John Magufuli kwa kumpa kibali cha kuruhusu Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda na Kamati yake ya Ushindi ya Taifa Stars kuendelea kufanya hamasa kwa Serengeti Boys.

Alisema anaamini kamati hiyo ilichangia kuifanya Taifa Stars icheze kwa kiwango kikubwa na hatimaye kufuzu kucheza fainali za Afrika (Afcon 2019).

"Tunaamini hamasa itaisaidia Serengeti Boys kufanya vizuri, kama sio kuchukua kombe, basi ipate nafasi ya kwenda Brazil kwenye fainali za Dunia," alisema Karia.

Pazia la fainali za Vijana za Afcon U-17, litafunguliwa Jumapili kwa wenyeji Serengeti Boys kutoka Kundi A, kuwakaribisha yosso wenzao wa Nigeria, mchezo utakaochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam majira ya saa 10 jioni.




Baadhi ya wafanyakazi wa Benki ya Exim makao makuu jijini Dares Salaam, wakionyesha ishara ya ushangiliaji jana wakati wa uzinduzi wa kampeni maalum inayofahamika kama 'Afconika na Exim', ambayo inatoa fursa kwa wateja wa benki hiyo kulipiwa gharama zote za safari na malazi, ili waweze kushuhudia mechi za Timu ya Taifa, Taifa Stars katika fainali za Kombe la Mataifa ya Africa (Afcon) 2019 nchini Misri. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Benki Exim yatafuta wakuliamsha Afcon

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim imezindua kampeni maalum inayofahamika kama 'Afconika na Exim' ambayo inatoa fursa kwa wateja wake kulipiwa gharama zote za safari na malazi ili waweze kushuhudia mechi za Timu ya Taifa, Taifa Stars katika michuano ya fainali za Kombe la Mataifa ya Africa (Afcon) 2019 nchini Misri.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Huduma ya Rejareja wa Benki ya Exim, Andrew Lyimo, alisema kampeni hiyo ya miezi miwili itakamilika mwanzoni mwa Juni na ipo wazi kwa wateja wapya na wale ambao tayari wana akaunti katika benki hiyo.

"Kampeni hii inakuja ikiwa ni mwendelezo wa mkakati wa Benki ya Exim katika kusimamia ustawi wa wateja unaofahamika kama 'Exim kazini leo, kwa ajili ya kesho' (Exim at Work today, for tomorrow) unaoendana na dira na mwelekeo wa benki hii. Ni kampeni inayothibitisha nia ya Benki ya Exim katika kutafuta kesho iliyo bora kwa wateja na jamii inayoizunguka," alisema.

Alisema washindi wa kampeni hiyo watapata fursa ya kipekee ya kufurahia mchezo wanaoupenda huku pia wakipata fursa ya kuungana na Taifa Stars katika mashindano hayo, huku wakiwa wamelipiwa gharama zote za safari ikiwamo gharaza na Visa, tiketi ya ndege, gharama za tiketi ya kushuhudia mechi hizo pamoja na fedha za kujikimu.

"Jumla kutakuwa na washindi watano, ambapo washindi wawili watapatikana katika mwezi wa awali wa kampeni na washindi wengine watatu watapatikana katika mwezi wa mwisho wa kampeni hii," alisema.

Kwa mujibu wa Lyimo, ili kushiriki katika kampeni hiyo, wateja wapya wanapaswa kufungua Akaunti ya Akiba na kuhakikisha kila mwezi ina kiasi kisichopungua Sh. 500,000 au zaidi au kufungua Akaunti ya Current/Biashara ikiwa na wastani wa kila mwezi wa Sh. 10,000,000 au hifadhi ya amana maalum (Fixed deposit) yenye thamani isiyopungua Sh. 5,000,000.

Kwa wateja ambao tayari wana akaunti ya benki hiyo, Lyimo alisema wanachotakiwa kufanya ni kuongeza akiba kwa kiasi cha Sh. 500,000 au zaidi kwa Akaunti za Akiba au kuongeza kiasi cha Sh. 10,000,000 kwenye akaunti zao za Current/Biashara au kuwa na hifadhi ya amana maalum (Fixed deposit) yenye thamani isiyopungua Sh. 5,000,000.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim, Stanley Kafu, alisema kampeni hiyo ni fursa adimu ambapo itatoa nafasi kwa washindi hao kuweza kushuhudia Taifa Stars ikitimiza ndoto zake za kushiriki katika mashindano ya Afcon baada ya zaidi ya miaka 30 kupita.

Kwa mujibu wa Kafu, kampeni hiyo ni sehemu ya mkakati wa kibenki katika kutafuta kesho bora kwa wateja wake na jamii kwa ujumla, ambapo pamoja na mambo mengine benki hiyo imekuwa ikiunga mkono agenda za kitaifa ikiwamo suala zima la michezo.

# Michezo

Alhamisi Aprili 11, 2019

Nipashe




## Guardiola: Kipigo 1-0 ni bora kuliko 0-0

UKURASA 30

**BASI TENA...**



Beki wa Manchester City, Fabian Delph (kushoto), akimchezea ndivyo sivyo mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane, na kumsababishia majeraha ya kifundo cha mguu ('enka') yanayoelezwa yanaweza kumuweka benchi hadi mwishoni mwa msimu huu. Tukio hilo lilitokea juzi katika Uwanja wa Tottenham Hotspur wakati Spurs ikishinda 1-0 kwenye mechi ya mkondo wa kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. **Habari UK. 28**

## Simba wang'atwa sikio vs Mazembe

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEWAHI kuwa mfadhili wa Simba, Azim Dewji, licha ya kuitabiria makubwa klabu hiyo katika mchezo wake wa marudiano wa hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ambao utachezwa Jumamosi mjini Lumbumbashi, ameing'ata sikio kuhusu mbinu za kuibuka na ushindi.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Dewji, alisema Simba ya mwaka huu ni 'moto' na ina uwezo wa kuwang'oa TP Mazembe na kusonga mbele katika mashindano hayo kutokana na kuwa na wachezaji wenye vipaji na ari ya kupambana kupata matokeo chanya.

Dewji ambaye alipokuwa akiidhamini Simba ilicheza hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika (Caf) mwaka 1993, alisema kitu pekee kinachopaswa kufanywa na wachezaji na viongozi wa klabu hiyo ni kuondoa hofu kuelekea mchezo huo wa marudiano na badala yake kuelekeza nguvu katika mchezo tu.

"Ni kweli TP Mazembe ni timu ngumu na kongwe. Ukiangalia ina historia kubwa Afrika na ndani ya miaka hii 10 tumeshuhudia ikitwaa ubingwa wa michuano tofauti ya Caf mara tano. Ni rekodi bora sana, lakini pamoja na ubora wao, nikiangalia ubora na uthubutu wa wachezaji wa Simba, naona vijana wetu wanaweza kufanya kweli.

"Wachezaji wa sasa wa Simba nawafananisha na nyota wa enzi zile tunafika fainali ya Caf, walikuwa wanajituma sana uwanjani. Na hawa ukiwaangalia wana kila kitu kinachoweza kuwaduwaza Mazembe kwao. Angalia walivyowakimbiza hapa Dar es Salaam, kwa kawaida Mazembe si wa kujiangusha hivyo, lakini uliona katika mchezo wa kwanza, walizidiwa sana ila bahati haikuwa kwa Simba," alisema Dewji.

Alisema wale wanaombeza mshambuliaji wa timu hiyo, John Bocco kukosa penalti si wanamichezo kwa sababu tukio hilo ni la kawaida katika mchezo huo.

"Usishangae kuona mpira umetangulia Lubumbushi na wachezaji wanakwenda kumalizia kazi ya kuandika historia zaidi kwa soka la Tanzania," Dewji alisema akionyesha kutania.

Kuhusu kitendo cha Caf kubadilisha mwamuzi wa mechi ya Jumamosi, amewataka wachezaji wasiondoke mchezoni na waongeze umakini.

# TFF YAIJIBU YANGA VIPORO SIMBA

**Na Somoe Ng'itu**

## ●●● Zahera aisoma ratiba, ageukia mechi ya Kagera Sugar Kirumba leo, asema...

WAKATI Bodi ya Ligi Tanzania ikiwataka wadau na klabu kuacha "kuumiza kichwa" kuhusiana na idadi ya "viporo" vya ligi hiyo walivyonavyo Simba, vinara wa ligi hiyo, Yanga wanatarajia kuwakaribisha Kagera Sugar katika mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM, Kirumba jijini Mwanza.

**Mara baada ya kuichapa African Lyon kwa mabao 2-0 Jumatatu wiki hii, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera alipaza sauti akilalamikia kitendo cha baadhi ya timu kubakiza mechi tano wakati timu kama Simba ikiwa na mechi 16 mkononi, huku timu yake na Azam FC zikibakiza mechi nane kwenye ratiba ya Ligi Kuu.**

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Boniface Wambura, alisema kuwa hakuna timu iliyoandaliwa kutwaa ubingwa na mabadiliko ya mechi zote za Simba za Ligi Kuu yalitokana na ratiba ngumu waliyokuwa nayo katika mashindano ya kimataifa.

Wambura alisema pia Simba italazimika kuwa na ratiba ngumu ya mechi za Ligi Kuu ili kuhakikisha kalenda ya msimu haivurugiki na vile vile kuangalia maslahi ya kitaifa.

"Kesho (leo) tunatarajia kutangaza ratiba ya mechi zote za Simba zilizosalia, hapo ukijumlisha na viporo kama kile cha JKT Tanzania ambacho kilitokana na mvua kubwa kunyesha, ...itakuwa na changamoto, lakini watalazimika kuifuata ili kalenda nyingine pia zisivurugike," alisema Wambura.

Simba ambayo imecheza mechi 22, imebakiza michezo 16 ili kumaliza msimu huu, wakati Yanga yeye alama 71 imecheza mechi 30 sawa na Azam FC wenye pointi 63 walioko katika nafasi ya tatu.

Kuelekea mchezo huo dhidi ya Kagera, Kocha Mkuu wa Yanga, Zahera, amesema wachezaji wake wako katika hali nzuri na anafahamu wazi mechi ya leo itakuwa ngumu na yenye ushindani.

Zahera alisema kuwa wamejiandaa kuendeleza mapambano kwa lengo la kupata ushindi na kujiweka katika mazingira ya kutwaa ubingwa wa ligi hiyo.

"Tumefanya maandalizi ya kutosha ya siku mbili, miili ya wachezaji iko vizuri, tunajua itakuwa mechi ngumu kuliko ile ya African Lyon, ndio maana tulijipanga kuwaweka tayari wachezaji wa ajili ya mechi hiyo," Zahera alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, alisema kuwa mechi ya leo haitakuwa nyepesi kwa timu zote kwa sababu kila upande unahitaji kujiweka mahali salama.

"Hatujafanya vizuri msimu huu na mechi zetu zilizopita, tumeshaona tulipokosea na kesho (leo) tunataka kujirekebisha, nafasi yetu si nzuri," alisema beki na nahodha huyo wa zamani wa Stars na Mtibwa Sugar.

Ratiba ya awali ilionyesha kuwa msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara utamalizika ifikapo Mei 26, mwaka huu na baada ya hapo Taifa Stars ambayo imefuzu kucheza fainali za Afrika (Acon 2019) itaingia kambini kuanza kujinoa kuelekea michuano hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >